

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**BUNGE LA KUMI NA MOJA**

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini na Nane – Tarehe 15 Juni, 2017**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu tunaanza na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina swali la ufafanuzi nataka kujua sisi tunaokaa katika Mikoa ya mipakani hususan Kigoma, Kagera, *recently* nimeambiwa na Mtwara limekuwepo tatizo kubwa la wananchi wetu kuambiwa siyo raia linapokuja suala la uandikishwaji wa vitambulisho vya Taifa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi hawa wako Tanzania na kama unavyofahamu nchi yetu wananchi wake wengi wako mipakani mwa nchi yetu.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Nini tamko la Serikali kuhusu hali hii na namna gani Serikali yako itajipanga kuhakikisha kuwa wananchi hawa wanapewa haki sawa kama wananchi wengine wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kujibu swali la Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mambo mawili, uandikishaji na utaratibu wake pia vikwazo vya uandikishaji kwenye mikoa ya pembezoni, hasa kwenye mikoa ambayo umeitaja, Kigoma ambapo Mheshimiwa unatoka, Kagera, Mtwara, Kilimanjaro pia hata Arusha kwa Wilaya za Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Taasisi yetu ya *NIDA* inaendelea kufanya kazi ya uandikishaji wa kutoa vitambulisho vya Kitaifa, kitambulisho ambacho ni muhimu sana kwa Mtanzania kukipata, lakini katika utoaji wake lazima tuwe makini kwa sababu ni kitambulisho ambacho tukifanya makosa tunaweza kujikuta tunakabidhi vitambulisho vya Utaifa kwa watu wa Mataifa mengine. Kwa hiyo, *NIDA* tumewataka wawe makini sana na kazi hiyo wanaifanya kwa umakini ukubwa na zoezi hili la utoaji vitambulisho linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa takwimu zinaonesha zaidi ya mikoa tisa imeishakamilika ingawa walikuwa wanaenda mkoa mmoja mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo umelieleza la mkanganyiko wa raia wa Tanzania na wageni na hasa kwenye mikoa ya pembezoni Kigoma ikiwemo maeneo haya lazima tuwe makini sana katika uandikishaji, tumeona makundi mengi ya Mataifa ya nje wakiingia nchini na hasa nchi jirani, kwa nafasi ile ya kwamba wao wanazungumza lugha yetu, wakijifunza kidogo wanaingia huku halafu

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wanaleta mkanganyiko wa namna ya kutumia lugha akishamudu kuzungumza lugha inakuwa tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Kigoma, Kigoma ni mpakani mwa Tanzania na Burundi na Warundi wengi wanazungumza Kiswahili na wananchi wa Kigoma kwa Kabila lao wanazungumza lugha moja na Burundi, kwa hiyo ni ngumu sana ukifanya jambo hili kwa haraka unaweza kukuta unatoa vitambulisho kwa Warundi walioko nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunatakiwa kuwa makini na Serikali tumejipanga kuwa makini kupitia Taasisi yetu ya *NIDA*. Wananchi walioko kwenye Mikoa hii wasione usumbufu pale tunapohoji na kutumia njia zetu za kiintelijensia kujua huyu kama ni Mtanzania au laa na wakaona wanachelewa, wengi wanaolalamika kwamba tunachelewesha ni hao wanaotaka uraia kwa haraka, kwa hiyo tuko makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge zoezi hili ni lazima mtuvumilie hasa kwa mikoa ya pembezoni kwa sababu lazima tuwe makini. Kule Mtwara, Watanzania wanaokaa Mtwara ni Wamakonde, lakini kule Msumbiji walioko mpakani ni Wamakonde pia na wanazungumza lugha moja, kwa hiyo lazima tuwe makini. Halafu kule Loliondo, mimi nimeenda Loliondo wananchi wengi ni Wamasai lakini mpakani Kenya wanaoishi kule ni Wamasai, kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuwa makini. Kwa hiyo, hata tunapofanya shughuli zetu za Kiserikali tunakuwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba, zoezi la uandikishaji linaendelea, lakini kwa umakini mkubwa ili vitambulisho viende kwa Watanzania tu na sio raia wa nje ili kupunguza idadi kubwa ya watu wa nje kuingia ndani na kufanya idadi ya wanaokaa nchini kuwa wengi, mwisho Serikali tutakuwa tunalaumiwa kwa kutomudu kutoa huduma, kumbe sisi tumepanga bajeti ya Watanzania wale milioni 50, lakini tunajikuta tuko milioni 55 kwa sababu ya kuwaachia wananchi wa kutoka nchi nyingine kuingia hapa

nchini. Hivyo, tutaendelea kutoa vitambulisho katika mikoa yote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru kwa ufafanuzi huo nina swali moja dogo tu nalo la ufahamu vilevile. Maafisa wa Uhamiaji wamekuwa na tabia ya kuvamia watu kwenye *disco* usiku, wamekuwa na tabia ya kuvamia watu kwenye masoko, kwenye magulio, eti wanasaka watu ambao sio raia. Je, mnaweza mkaelekeza vizuri ili Maafisa Uhamiaji wetu hasa katika Mkoa wa Kigoma watumie weledi zaidi wanapokuwa wanajiridhisha na uraia wa wananchi walioko mipakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ukweli kwamba maeneo hayo aliyoyataja kwenye masoko, kwenye minada, kwenye *disco* ni maeneo ya mikusanyiko ambayo ni rahisi sana wageni kutoka nje kwenda kujichanganya wakijua kwamba ni ngumu kwa taasisi kama yetu kuingia pale kwenda kufanya ukaguzi. Tunachofanya ni kwamba kutumia utaratibu wetu tulionao wa ndani wa kujua nani ni nani, tukijua huyo mtu kama yuko kwenye *disco* yuko sokoni tutamfuata hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na msisitizo wa kwamba tunapofanya kazi watumishi wa Serikali tufanye kazi kwa weledi mkubwa, lakini lazima tutakwenda popote alipo endapo tutagundua kama huyo hajafanya matendo yanayokwenda sambamba na sheria ya nchi na taratibu za nchi, bado tumesisitiza weredi katika kufanya kazi yetu, hakuna haja ya kusumbua wananchi badala yake nenda kwa unayemtaka mchukue, mwambie kwa nini nimekuchukua ili ajue na aweze kupata nafasi ya kujitetea, huo ndio utaratibu ambao tumeusisitiza Serikalini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Jamii yoyote maendeleo yake yanatokana na mfumo wake wa elimu, ni tunda la mfumo wake wa elimu, Sera ya Mafunzo ya Elimu ya mwaka 2014 inaelezea kuwawezesha rasilimali watu kuwekeza kwenye akili za mwanadamu ili waweze kuendana na karne hii ya sayansi na teknolojia katika nyanja zote. Je, ni nini nguvu ya Sera hii ya Elimu ya 2014 ukilinganisha na Sera ya Elimu ya 1995 katika kudhibiti ubora wa vitabu vya kiada na ziada. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tunayo Sera ya Elimu na Sera hii ya Elimu ndiyo ambayo tunaifuata katika kuendesha shughuli zote za elimu kuanzia ngazi ya Awali, Msingi, Sekondari hata Elimu ya Juu. Ni mwongozo ambao tunatakiwa tuufuate ili kufikia malengo tunayoyataka. Sasa nini nguvu ya Sera ya Elimu ya sasa na ile ya miaka iliyopita ni kwamba nguvu yake ni pale ambapo Sera inakwenda inakidhi matakwa ya sasa kulingana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia katika kupata rasilimali watu yenye uwezo wa kutekeleza shughuli ambazo sasa tumejipangia ili ziweze kuleta matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya mwaka 1995 ambayo ameieleza pamoja na uzuri uliokuwepo katika utekelezaji wake na malengo yake kwa miaka hiyo na hii ya sasa nikiri kwamba tunayo mabadiliko ya kisera, ndani ya nchi ambayo yanataka Sera iweze kukidhi matakwa ya wakati huo, wakati huu sasa msisitizo wa elimu yetu ni wa sayansi na teknolojia ili tuweze kwenda sambamba na mabadiliko yetu.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nguvu ya sera ni pale ambapo inatoa matokeo tunayoyatarajia na kama ambavyo nimesema sasa matarajio yetu ni kuzalisha wanasayansi wengi. Leo hii Tanzania Serikali yetu imesema tunataka kuendeleza viwanda, kwa hiyo Sera yetu ni lazima ijielekeze kwenda mashuleni kuwaandaa vijana, kuwaandaa wasomi ambao wataweza kuingia kwenye ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia pia kuendesha viwanda mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu ni kufanya maboresho ya sera, kufanya mapitio ya kupitia wataalam wetu walioko Vyuho Vikuu, Walimu ambao wako kazini, lakini na wadau wengine ili tuone kama je, sera tuliyonayo inakidhi mahitaji ya sasa na mabadiliko hayo ndiyo ambayo yanaweza kuleta nguvu ya kuleta rasilimali watu ambayo kweli itakidhi mahitaji ya sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na majibu yako ya nguvu ya sera hii, nikikwambia kwamba sera hii ndiyo imezalisha vitabu vibovu ambavyo havijawahi kuonekana katika historia ya Tanzania, ambavyo vimegharimu zaidi ya bilioni 108. Je, ni nini wajibu wa Serikali kwenye ubovu wa vitabu hivi vya sasa viondoke kwenye mzunguko kwa sababu ni sumu inayolishwa Taifa la Tanzania na kuua nguvu ya sayansi na teknolojia katika Taifa la Tanzania? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimjulisha Mheshimiwa Mbatia kwamba sera ni kitu kingine na kitabu ni kitu kingine, ingawa vitabu vinaandaliwa kutokana na sera. Kwanza lazima uwe na sera, sera itakwenda kuandaa mtaala, mtaala ndio ambao unaandaa *syllabus*, *syllabus* ndiyo inapendekeza somo hili liandaliwe vitabu gani vya kiada na ziada.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu vya kiada ni vile vitabu vya msingi na vya ziada ni vile ambavyo vinasaidia katika pia katika kuelimisha somo hilo. Kwa hiyo, sasa *syllabus* iliyotokana na mtaala na hiyo Sera, *syllabus* ndiyo inayopendekeza somo fulani liandaliwe kitabu gani kwenye mada zipi ili zitoe matokeo gani. Kwa hiyo, ile *syllabus* ambayo inapendekeza kitabu sasa ndiyo unakusanya wataalam wanaandaa kitabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ubovu wa kitabu uko huku kwenye maandalizi, huyu anayeandaa kitabu kile ndiye anayeweza kuleta ubovu. Wito wangu ni kwamba ndani ya Serikali tunayo Taasisi ya Elimu Tanzania ndiyo ambayo inao wajibu sasa wa kuandaa vitabu, nataka nikujulishe tu kwamba awali suala la uandaaji vitabu tuliwaachia watu mmoja mmoja kutunga vitabu na sisi tunavichukua, tuliona vitabu hapa vya Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza muda Mheshimiwa Nyangwine alikuwa na Waandishi wengine, kwa hiyo kila mmoja alikuwa anaandika kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukagundua liko tatizo kidogo, ndiyo yake tumeamua kurudisha katika Taasisi yetu ya Elimu ambayo yenyewe imekusanya wataalam wengi tu wasomi wa kila fani ambao sasa wanatakiwa watengeneze vitabu kutokana na matakwa ya *syllabus* ya somo hilo ili viweze kutumika mashuleni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama liko tatizo, tatizo litakuwa ni la mtengenezaji, yule ambaye anatunga, ile *panel* ambayo inatunga, labda kwenye uchapishaji, ndiyo kunatoa hayo matokeo ya mwisho. Kwa hiyo, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tutafanya marekebisho makubwa kwenye Taasisi yetu ya Elimu na Waziri wa Elimu amefanya marekebisho hapa baada ya kumwajibisha Mtendaji Mkuu wa Taasisi, tunataka Taasisi iwe makini kwa kujua matakwa ya somo na kitabu ambacho kimependekezwa na ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaamua sasa kutumia wasomi wetu wa Vyuo Vikuu waliojikita kwenye fani,

tuwapeleka Taasisi ya Elimu ili wao watutengenezee vitabu vinavyotosha kufundisha kwa mujibu wa mtaala na kutosheleza sera ya nchi. Huo ndio mkakati wetu kwa hiyo nimhakikishie tu kwamba tutafanya marekebisho na marekebisho yameendelea kufanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania ni nchi ambayo ina mifugo mingi sana na wafugaji wetu wengi ni wale wafugaji wa kuhamahama. Jambo hili limetuletea migogoro sana ya ardhi mpaka kusababisha mauaji. Sasa kumezuka mtindo wa mikoa ile ya wafugaji tayari watu wanahama sasa wanaenda katika mikoa ambayo sio ya wafugaji kwa asili, maana yake ni kwamba hapa sasa migogoro sasa ya mauaji haya ya wafugaji na wakulima tunayahamishia kwenye hiyo mikoa ambayo siyo ya wafugaji. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kusambaza haya mauaji ya wakulima na wafugaji katika mikoa ambayo siyo ya wafugaji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali linataka nini mpango wa Serikali wa kupunguza mauaji yanayotokana na migogoro ya wakulima na wafugaji kwenye maeneo kadhaa. Jambo hili Serikali tumekuwa tukifanya utaratibu wa kuona namna nzuri ya kundi hili la wafugaji na mifugo yao, pia wakulima waendeleo na shughuli zao za kilimo kwa kuanza zoezi la uandikishaji wa mifugo tuweze kuitambua, kijiji gani, kina nani, ana mifugo kiasi gani ya aina gani, ili tuweze kuona kama je, mifugo hiyo inatosha kukaa kwenye eneo hilo,



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

baada ya kuwa vijiji vyetu vyote vimefanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri leo nimeita Maafisa Mifugo wa nchi nzima wako hapa na Saa Tano nitakutana nao pale Chuo cha Mipango. Waheshimiwa Wabunge, Wafugaji na Wakulima yapo mambo ambayo lazima watuvumilie, Serikali sasa lazima tuchukue mkondo wetu. Tunahitaji sasa tuanze kujua utaratibu mzuri wa ufugaji na kwamba Taifa hili tunataka tupate wafugaji ambao kweli ni wafugaji wanaofuga, ambao wako *serious* kwenye ufugaji, ufugaji huu lazima uendane na maeneo ya kulisha ili kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji yanayopelekea kwenye mauaji ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kikao changu na Maafisa Mifugo ambao watakaa leo na kesho kujadili namna bora, tutatoka na azimio ambalo nchi nzima lazima litatakiwa lifuatwe kwa namna bora ya kufuga mifugo yetu. Tunataka sasa Maafisa Mifugo washiriki kikamilifu kwa kuwasaidia wafugaji namna bora ya kufuga mifugo yao ili tupate mifugo ambayo ina tija kwa yeye mfugaji binafsi lakini pia hata kwa mapato ya Kitaifa. Hatuwezi kuwa tunajilinganisha na nchi ya Botswana ambayo ina ng'ombe wachache kuliko Tanzania, lakini wenzetu wana mapato makubwa ya Kitaifa, Tanzania tuna mapato kidogo ingawa tuna ng'ombe wengi, maana yake hatufugi kwa utaalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kikao changu cha leo na Maafisa Mifugo nitatoka na maazimio ambayo nitakuja kuyatamka hapa siku ya mwisho ya Bunge ili Taifa twende na utaratibu ambao kweli mifugo hii itakuwa inaweza kuratibiwa vizuri na kufugwa vizuri ili itoe matokeo ambayo tunayatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa utaratibu huo umefanywa, mfano ipo mikoa ambayo siyo ya wafugaji kwa asili na utaratibu huu unaosema kutenga maeneo kwa mfano kama Halmashauri yetu ya Liwale tumetenga yale maeneo, lakini kutokana na hawa wafugaji kuwa na pesa nyingi wamekuwa wakiwahonga Viongozi wenye mamlaka, matokeo yake kijiji ambacho kimepangiwa idadi fulani ya mifugo utakuta idadi ile inaongezeka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unawaeleza nini hawa watu wenye mamlaka mbalimbali kwanza, kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na hata Wenyevitwa wa Vijiji ili wafuate ile sheria kama kijiji kimepangiwa mifugo 200 basi iwe ni 200 na kama ni 1,000 basi iwepo 1,000. Je, nini kauli yako juu ya hawa wenye mamlaka za kuwaruhusu hawa wafugaji? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa umuhimu ni kuweka utaratibu na kila mmoja mwenye dhamana kutekeleza wajibu kwa dhamana ambayo amepewa. Baada ya kikao chetu nitatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa walioko kwenye maeneo yetu, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Maafisa wenyewe ambao wanashughulikia sekta hii ya mifugo kila mmoja lazima awajibike inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo yale tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yenu, tuone kwamba matamko yetu ya Serikali yanakwenda kwa Watendaji ili kusaidia kuondoa migogoro, migongano ambayo sio muhimu tuweze kuifuatilia ili nayo pia itusaidie katika kuona kwamba sekta hii nayo pia inaweza kutoa mwelekeo ambao tunautarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya haya yote na yale ambayo tutayapata baada ya mjadala ambao

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

tutauweka, tunafikiria pia kama ambavyo Wizara imependekeza kuandaa *zone* za shughuli za mifugo tukitambua Mikoa ambayo imejikita katika ufugaji tuwape nguvu zaidi ya kufuga zaidi ili na Serikali tuongeze nguvu ya kuwasaidia wafugaji kwenye maeneo ambayo tunadhani yanafaa zaidi kuimarisha mifugo. Yale maeneo ambayo hayana mifugo hatuwezi kum-*limit* mtu ambaye anataka kuweka ng'ombe wake watano, sita. Muhimu zaidi, lazima uwe na idadi ya ng'ombe wanaotosha kwenye eneo ulilionalo la kuwalisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante.  
Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sera ya Serikali kuhakikisha kwamba miundombinu katika maeneo mengine mengi ya nchi hii inapitika, lakini unafahamu kwamba Mkoa wa Dar es Salaam tuna mradi mkubwa wa *DMDP* ambao ni dola milioni 75, takriban bilioni 158. Fedha hizi zinatakiwa zifanye kazi ya kusaidia miundombinu katika Manispaa zote tano Mkoa wa Dar es Salaam ikiwemo Jimbo la Ukonga na Ilala ambalo tunaweza kupata bilioni 43.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mradi huu umekuwa ukisuasua sana, Jimbo langu la Ukonga lina Kata mbili Kata ya Ukonga mitaa yote minne na Kata ya Gongo la Mboto barabara zile zimeshindwa kutengenezwa kwa sababu fedha imechelewa kutolewa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu unafahamu hali mbaya ya miundombinu baada ya mvua kubwa Dar es Salaam ikoje, nini kauli ya Serikali juu ya kuwezesha miradi hii mikubwa iendelezwe na fedha kupatikana ili kupunguza adha kwa wananchi wa Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo kumbukumbu kwamba tuliwahi kukutana Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, moja kati ya mambo ambayo tuliyazungumzia ni huu mradi wa Dar es Salaam *Metropolitan* kitu kama hicho, ambao pia unanufaisha Manispaa zetu zote tatu za Kinondoni, Ilala pamoja na Temeke kwa ujenzi wa miundombinu iliyoko kwa fedha ambayo tumeipata kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulishatoa maelekezo kwa Manispaa zote za Mkoa wa Dar es Salaam, tulitoa maelekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam kuhakikisha kwamba fedha hii ambayo tumeipata kutoka Benki ya Dunia itumike kikamilifu. Nilihakikishiwa kwamba usimamizi huo utafanywa na utekelezaji wa miradi hiyo utafanywa ni vile sikujua kama swali hili litakuja hapa ningeweza kufanya mawasiliano ya haraka ili kujua namna ambavyo wanatekeleza sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi kwamba baada ya hapa nitawapigia simu kujua utekelezaji ukoje, kwa sababu fedha tunayo, maeneo yaliyoharibika yapo na mahitaji ya matengenezo ni muhimu kwa barabara zetu na hasa kwenye Jimbo lake la Ukonga na maeneo mengine, Mheshimiwa Mwenyekiti pia ni mnufaika wa mradi huu wa *DMDP* ambao pia tungehitaji pia naye aweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba, baada ya kikao hiki nitapiga tena kwa Katibu Tawala anipe mrejesho wa namna hiyo. Pia Waziri wa TAMISEMI yuko hapa, ataanza kuwahi kupiga simu kule kujua nini kinafanyika, halafu atanipa mrejesho hapa Bungeni. Kama jambo hilo halijakamilika, basi tutafanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana kwa majibu hayo na nafikiri watu wa Dar es Salaam watakuwa wamefurahi kusikia kwamba umetoa maelekezo sasa maalum ya kufuatilia mradi utekelezwe mapema iwezekanavyo. Nina swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ukonga ni Jimbo jipya na ni Majimbo ya Mjini Vijijini, lakini barabara yangu ya Kitunda, Kivule, Msongola imekuwa na hadi zaidi ya miaka 25 sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, naomba ukae. Hilo swali lako sio la kisera lakini vile vile katika pesa hizo hizo za *DMDP* zipelekwe huko huko kwenye barabara hiyo.

Ahsante, naomba ukae, maana hata hizo *DMDP* na mimi nimo humo. Tunaendelea na Mheshimiwa Gulamali. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na matukio ya ukamataji katika maeneo mbalimbali hasa Wilaya ya Igunga na maeneo mengineyo ya nchi hasa kukamatwa kwa mifugo, mifugo hii inapokuwa inakamatwa wakati mwingine katika hifadhi huwa inapigwa minada pasi na kuwashirikisha wale ambao ng'ombe wao wamekamatwa, tayari kunakuwa na watu tayari ambao wanatoka Dar es Salaam kuja kununua ile mifugo katika yale maeneo, wale ambao ng'ombe wao wamekamatwa wakienda kutaka kununua wale ng'ombe hawaruhusiwi na watu wa hifadhi. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya ukamataji hovyoywa ng'ombe katika maeneo haya yetu pia juu ya kauli tata ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili kwa wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake eneo ambalo nimeweza kulipata vizuri ni pale ambapo anataka Serikali itoe tamko juu ya ukamataji wa mifugo. Suala la mifugo linafanana na swali ambalo limeulizwa hapa awali na nimetoa maelekezo kwamba leo hii nakutana na Maafisa Mifugo wote nchini kufanya mapitio ya udhaifu na upungufu. Pia kuimarisha utaratibu ambao tutaweza kuutoa kwa sekta ya mifugo nchini ambayo imeweza kupelekea matatizo mengi, kuwa na migongano ya wakulima na wafugaji, migongano ya wafugaji na maeneo yetu yaliyohifadhiwa kisheria, lakini tuna migongano tu ya wafugaji wenyewe kwa kuchanganya ng'ombe na vitu vya namna hii na iko migogoro mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua Serikali inasema nini juu ya ukamaji wa hovy. Kimsingi iko sheria inayoelekeza mifugo, shughuli za kilimo zifanywe kwenye maeneo gani. Kwa hiyo, kama kunakuwa na ukiukwaji lazima kutakuwa na ukamatwaji. Kwa hiyo, hilo walijue kwamba maeneo yote haya tumeyaratibu na tumeyawekea sheria ya namna kila mmoja anatakiwa kuyatumia, unapokwenda kinyume lazima utakamatwa. Kwa hiyo, hilo ndilo jibu la msingi la kwamba lazima kutakuwa na kukamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni udhaifu gani umejitokeza katika ukamataji kama ambavyo nimeshauri jambo hili niachiwe kwa sababu leo nakutana na Maafisa wanaoshughulikia mifugo kwenye Halmashauri zote ikiwemo na Halmashauri yake ya Igunga ambayo pia ina wafugaji, ina wakulima ili tuweze kuondoa matatizo hayo.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hatuhitaji kuwa na migogoro kati ya makundi yetu huko ya wafugaji, wakulima na watumishi wetu wa hifadhi pale ambako kila mmoja angehitaji kupata huduma. Sasa tunataka tuweke utaratibu wa nani, wakati gani na kwa namna gani, unaweza kupata huduma kutokana na shughuli unayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali yamekwisha. Nakupongeza, Wazungu wanasema *man of all seasons*, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali ya kawaida, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Omari Shekilindi.

Na. 394

**Huduma za Afya kwa Makundi Maalum**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Wilaya ya Lushoto ni Kongwe na ina wananchi wapatao 550,000; kati ya hao kuna wenye ulemavu mbalimbali, wajane na wazee na wengi wao wapo vijijini na hawajawahi kupata huduma za msingi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia makundi hayo ili nao waweze kupata huduma muhimu kama watu wengine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi wa watu wenye ulemavu wapatao 699 umefanyika, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 3,471 wametambuliwa na wazee 8,511 wametambuliwa. Zoezi hili ni endelevu kwa Halmashauri zote kwa ajili ya kutumia takwimu hizo katika mipango na bajeti kila mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa sera ya utoaji huduma bure kwa makundi maalum, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto hivi sasa imefanikiwa kutoa kadi za CHF kwa wazee 3,991 na watoto wanaoishi katika mazingira magumu 1,619 wamepewa kadi za msamaha wa gharama za matibabu. Aidha, dirisha maalum limefunguliwa kwa ajili ya huduma za wazee katika vituo vyote vya afya vya kutolea huduma za afya. Serikali itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa makundi maalum yenye msamaha wa matibabu kwa kutenga bajeti kila mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kila Kata kitajengwa kituo cha afya; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga vituo vya afya vinne kwenye vituo hivyo 150 ambavyo Serikali itavijenga nchi nzima hasa katika Kata ya Ngwelo, Makanya, Malibwi na Kata ya Gare. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mimi kama Mwakilishi wao naomba nimhakikishie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba makundi haya hayapati huduma



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

aliyoiongelea hapo pamoja na kwamba majibu yake ameyajibu kitaalam. Je, yupo tayari kwenda au kutuma timu yake ili ikapate uhalisia wa kuwa makundi hayo hayapati huduma hiyo ipasavyo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika mpango mkakati wa ujenzi wa vituo vya afya jambo hili tumelipa kipaumbele zaidi. Mheshimiwa Mbunge Shekilindi anafahamu hata tulivyokwenda pale tuliangalia Halmashauri ya Lushoto na ndiyo maana tukaona kwamba kwa sababu Lushoto ina changamoto kubwa sana aliyoizungumza hapa katika ujenzi wa hivi vituo vipya tunavyoenda kuvijenga, lakini sasa hivi tunaenda kufanya ukarabati mkubwa katika kituo hicho cha Mtao katika Halmashauri ya Lushoto japokuwa kiko katika Jimbo la Mheshimiwa Shangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba ni mpango wa Serikali na hasa Lushoto ukiangalia changamoto yake, ile barabara kwanza hata mvua ikinyesha huduma inakuwa ni changamoto kubwa. Naomba nimhakikishie kwamba tutaipa kipaumbele kwa kushirikiana naye na Halmashauri yake, kuhakikisha kwamba Lushoto inapata huduma nzuri za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kwamba watu hawapati huduma hii inayokusudiwa na ameniomba niweze kufika tena. Naomba nimhakikishie kwamba nina zoezi la *Q and A's (questions and answers)*, mara baada ya kuwapatia Watendaji mbalimbali wa Halmashauri maelekezo, zoezi la pili ni kwenda kufanya *verification*, jinsi gani wamefanya *compliance* ya yale ambayo tumeelekezana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba tutafika Lushoto, hata hivyo, nilivyofika katika hospitali ambayo iko pale nimekuta dirisha la wazee lipo.

Namhakikishia tutakwenda mimi mwenyewe na tutashirikiana na yeye kufanya *verification* kuona jinsi gani sasa wananchi hawa wanapata huduma hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la walemavu nchi hii limekuwa sugu kwa miaka mingi lakini Serikali bado haijaweka mpango mkakati wa kuwasaidia walemavu wao. Kwa mfano, ndani ya Jimbo langu la Mlimba kila siku napata maombi ya walemavu wakiomba vifaa na wengine watoto wadogo hawana uwezo kabisa wa kwenda kwenye shule maalum za walemavu. Je, Waziri yuko tayari sasa kutoa mpango mkakati wa kusaidia walemavu hawa, kuorodhesha Halmashauri zote ili wasaidiwe kwa mpango maalum? Maana tatizo hilo limekuwa sugu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kiwanga ni kweli inawezekana huko nyuma tulikuwa hatufanyi vizuri zaidi, lakini katika Serikali ya Awamu ya Tano tumefanya mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tulishuhudia Waziri Mkuu akipokea vifaa maalum kwa ajili ya kundi hili la watu wenye ulemavu ambapo vifaa vile tutavipeleka sehemu mbalimbali, lengo kubwa ni kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sasa hivi kuna *database* maalum inaandaliwa katika zoezi hilo. Kwa hiyo naomba nimtoe shaka, Serikali imejipanga, tutafanya kila liwezekanalo, lengo letu kubwa ni kuhakikisha kundi hili la watu walemavu linapata huduma. Vile vile kwa sababu tulikubaliana baada ya Bunge hili tutafika kule katika Jimbo lake, katika haya nayo tutaangalia katika muktadha mpana

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

sana, katika eneo gani na jinsi gani tufanye, kama kuna jambo *specific* katika eneo hilo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Tendega.

Na. 395

**Kuboresha Maslahi ya Walimu Nchini**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Miaka ya 1980 kulikuwa na ushindani mkubwa uliojitokeza kati ya shule binafsi na za Serikali ambapo Walimu bora wote walipatikana katika shule za Serikali kutokana na maslahi bora ikiwemo posho zaidi nje ya mshahara kama vile posho ya ufundishaji, posho ya kupanga, posho ya usafiri na posho ya mazingira magumu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya Walimu kama ilivyokuwa miaka ya 1980 ili kuendana na dhana ya elimu bure lakini bora?

(b) Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuboresha zana za kufundishia ili kwenda sambamba na ukuzaji wa ujuzi wa stadi za taaluma wanazosoma?

(c) Kwa kuwaombea Walimu wapande mabasi bure kwenda kazini kama ombaomba kama ilivyotokea Dar es Salaam; je, huku sio kuwadhalilisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

elimu nchini, Serikali imeanza kutoa posho kila mwezi kama motisha kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata ili kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafanya mapitio ya majukumu ya watumishi wote wakiwemo Walimu ili kuboresha maslahi ya watumishi wote kwa kuzingatia uzito wa kazi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechapisha na kusambaza vitabu, chati na miongozo mbalimbali ya kufundishia na kujifunza zipatazo 8,359,868 kwa ajili ya darasa la kwanza na la pili na tayari vimeshasambazwa katika shule zote za msingi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji wa vitabu hivyo, umeboresha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kutoka uwiano wa 1:3 hadi 1:2, lengo likiwa ni kufikia uwiano wa 1:1 kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Vile vile, Serikali imefanikisha kununua na kusambaza vifaa vya maabara vyenye thamani ya shilingi bilioni 16 ili kuboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwawekea utaratibu Walimu kupanda mabasi bila kulipia siyo azma ya Serikali kuwadharau Walimu na kuwafanya kuwa ombaomba, bali ni njia ya kuthamini kazi nzuri inayotekelezwa na Walimu hapa nchini. Naomba kutoa rai kwa viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu kubuni utaratibu wa kuwapatia motisha watumishi ili kuwapa ari ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri amesema katika majibu yake kwamba Serikali imechapisha vitabu na kusambaza vitabu milioni 8,359,868, Je, katika vitabu hivi ndivyo vitabu ambavyo Bunge letu lilishuhudia ni vitabu vile ambavyo vina upungufu wa

kisarufi pamoja na kimaudhui? Je, hawaoni kama wanaenda kulisha sumu watoto wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema Wabunge twende tukafanye utaratibu wa kuwapa motisha watumishi katika maeneo yetu. Ikumbukwe kwamba Mbunge ni Diwani katika Halmashauri zetu na hivi majuzi tu Wizara ya Fedha wamesoma bajeti yao na tumeona katika bajeti ile vyanzo vya mapato katika Halmashauri vimechukuliwa na Serikali Kuu. Je, Serikali iko tayari kurudisha vyanzo vya mapato katika Halmashauri zetu ili tuweze kuipanga bajeti na kuwa na posho za ziada kwa watumishi wetu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, mengine tumia uzoefu wako tu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru dada yangu kwa swali zuri ambalo ukizungumza suala la elimu na bahati nzuri hapa kuna swali lingine ameuliza Mheshimiwa Mbatia liligusa suala zima la elimu. Naomba nikiri wazi kwamba ndiyo maana Bunge hili lilifanya maazimio maalum kuhusu vile vitabu ambavyo vilikuwa na changamoto na ndiyo maana hivi sasa Wizara ya Elimu imeshaunda timu kufanya *verification* ya yale makosa ilimradi mwisho wa siku tuje kufika katika sehemu muafaka ambako Taifa letu hili linakwenda. Kwa hiyo, naomba aondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali suala hili iko katika kulifanyia kazi kwa kina kwa maslahi mapana ya elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la vyanzo vya mapato ambapo Waziri wa Fedha alizungumza hapa kwamba vyanzo hivi sasa vingine vimerudi Serikali Kuu. Naomba niwaambie, leo hii hapa ninapozungumza kwa sababu sisi ni Serikali za Mitaa kuna baadhi ya Halmashauri zingine uwezo wake ni mdogo zaidi. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kufanya tathmini pana lengo ni kukusanya mapato kwa kiwango kikubwa halafu kuyarudisha katika Halmashauri.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *commitment* ya Serikali hivi sasa na Waziri wa Fedha atakapohitimisha hapa atazungumza wazi kwamba fedha hizi zitakapokusanywa hata zile *property tax*, fedha hizi naomba niwahakikishie Wabunge kwamba zitarudi katika Halmashauri zetu ili mipango yetu ya bajeti ambayo imepangwa iweze kutekelezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chatanda, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Mboni Mhita.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, Ili Walimu waweze kufanya vizuri kwa kutulia, wanahitaji wasikilizwe kero mbalimbali ndogo ndogo ambazo zinawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya Walimu ambao wake zao au waume zao wako mbali na wao, wameomba uhamisho kwa muda mrefu hawajafanikiwa wenzi wao kwenda kwenye maeneo yale ambayo wanatakiwa kufanya kazi. Kwa mfano, kule Korogwe kuna Mwalimu ambaye yupo Korogwe lakini mke wake yuko Mtwara. Je, Serikali, ili kupunguza kero ndogondogo watakuwa tayari sasa kuwasaidia Walimu ili kuwahamisha wake zao waende kwenye maeneo ambayo wapo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili najua kwamba lina maslahi mapana kwa sababu ndoa za watu ni maisha ya watu. Zoezi hili la uhamisho limekuwa tofauti na miaka mingine lilisimama kwa sababu tulikuwa na zoezi kubwa sana la kufanya *verification* hapa ambapo ninyi mmebaini wazi kwamba suala la watumishi hewa, suala la vyeti feki, jambo hili ndio lilisababisha maeneo mengi sana hasa suala zima la uhamisho liweze kusitishwa.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hili lipo katika utaratibu wa mwisho, litakamilika, baadaye tutatoa maelekezo rasmi sasa ya jinsi gani uhamisho huu utaanza, kwa sasa lilisimama kwa maslahi mapana ya nchi yetu, litaendelea mara baada ya zoezi zima la uhakiki wa vyeti feki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo, jandae Mheshimiwa Mboni.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nimesikitishwa sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Sera ya Elimu ni kitu kingine na vitabu ni kitu kingine, naomba niulize swali sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali lako acha mambo mengine.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Sawa nauliza swali Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Utakaa chini sasa hivi hapo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize swali Mheshimiwa Naibu Waziri hasa la vitabu, pamoja na kwamba Kamati imeundwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, lakini nimepita kwenye shule mbalimbali bado vitabu vilevile vyenye makosa ndivyo vinavyotumika. Nilitegemea Wizara ingevitoe waendele kutumia vitabu vya zamani. Je, sasa hawaoni kwamba kuendelea kutumika kwa vitabu hivyo, ni makosa makubwa na wanapanda sumu kwa watoto wetu na ni lini wataviondoa vitabu hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, limejibiwa na Waziri Mkuu hapa vilevile, endelea.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bahati nzuri wakati wa bajeti yetu wewe ulikuwa una-*chair* na suala la vitabu

tulilijadili na Bunge likawa limetoa maelekezo kwamba baada ya Serikali kukamilisha, taarifa tutaiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanyia kazi na niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa sasa hivi wanafunzi wapo likizo, suala la kusema wanaendelea kutumia vitabu kwa sasa hivi wapo likizo. Hata hivyo, si vitabu vyote ambavyo vina makosa na kama Serikali ilivyokwishasema baada ya Kamati za Wataalam kukamilisha, maamuzi ya Serikali yatawasilishwa kama ambavyo tayari Kiti chako kilikuwa kimeelekeza. Kwa hiyo, ningepomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira, waiachie Serikali ifanye suala hili kwa umakini unaotakiwa na muda unaotakiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mboni.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kuna uhaba mkubwa sana wa nyumba za watumishi katika Jimbo la Handeni vijijini, japo Halmashauri, wananchi pamoja na Mbunge wamejitahidi sana kwa hali na mali kuweza kupunguza changamoto hii. Je, Serikali ina mpango gani ya kuweza kupunguza au kumaliza kabisa changamoto hii ya nyumba za Walimu katika maeneo ya vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna changamoto hizi za nyumba za Walimu na nawashukuru kwanza Waheshimiwa Wabunge tulivyokuwa tunajenga zile nyumba karibuni 229 ambazo ni *six unit in one* nilipata ushirikiano wa kutosha sana katika ofisi yetu kuhakikisha kwamba tunatoa maelekezo na mpaka nilivyofika mwezi wa 12 tulifanikisha kujenga zile nyumba zote ndani ya MMES // ambazo ni kwa ajili ya Walimu wetu wa sekondari.



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika mpango wa sasa tunaendelea katika bajeti ya mwaka huu, tutajenga nyumba kadhaa katika maeneo mbalimbali. Naomba nikiri wazi kwamba ni kweli Jimbo lake lina changamoto ya nyumba, naomba nimhakikishie kwamba Serikali tutaangalia nini tufanye, tutafanya kila liwezekanalo nipende kuwaomba hasa Wakuu wa Wilaya mbalimbali tuweze kuiga Mkuu wa Wilaya ya Lushoto anavyofanya kazi katika maeneo yake. Nimepita kule Lushoto kuna mambo mengi sana ya mfano yanafanyika, naamini tukifanya haya tutaweza kupata mafanikio makubwa sana katika miundombinu hasa katika sekta ya elimu na sekta ya afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara na hiyohiyo, Mheshimiwa Mussa Ntimizi kwa niaba yake Mheshimiwa Almasi.

Na. 396

**Kujenga Mabwawa ya Maji Jimboni Igalula**

**MHE. ALMAS A. MAIGE (K.n.y. MHE. MUSA R. NTIMIZI)**  
aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa ya maji katika Jimbo la Igalula hasa ikizingatiwa kuwa Jimbo hili lina maeneo mazuri ya kutega mabwawa ya maji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa bwawa katika Kijiji cha Igalula unaohusisha ujenzi wa miundombinu ya maji. Utekelezaji wa mradi huu wenye

thamani ya shilingi milioni 365.47 unaendelea na mkandarasi anakamilisha kazi hiyo ifikapo tarehe 23 Agosti, 2017 ikiwa ni mkataba wa miezi minne (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya juhudi kubwa kwa kuangalia fursa mbalimbali za miradi ya maji ili kupunguza shida ya maji katika Jimbo la Igalula na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almasi.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Musa Ntimizi na wananchi wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa vile, Jimbo la Igalula halitapatwa kabisa maji ya Ziwa Victoria; je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza mradi wa kuchimba mabwawa katika Vijiji vya Igalula, Goweko na Loya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile Wilaya nzima ya Uyui haina maji chini; je, Serikali ina mpango gani tena wa kuchimba mabwawa katika vijiji vya Jimbo la Tabora Kaskazini vya Kanyenye, Majengo na Izugawima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili analozungumza Mheshimiwa Mbunge kweli kuna changamoto hii ya maji, ndiyo maana pale kuna miradi ya mabwawa. Kuna moja ambalo inafanyika *design* pale lakini kuna mradi mwingine upo katika maandalizi ya hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sababu inaonekana kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Uyui na Mbunge anafahamu siku ile tulipokuwa kwenye vikao vya Halmashauri miongoni mwa shida kubwa aliyozungumza pale kwa niaba ya wananchi wake ni shida ya maji katika

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Wilaya nzima ya Uyui. Serikali katika mpango wake hivi sasa, licha ya masuala ya mabwawa imefanya uwekezaji mkubwa sasa wa kutenga fedha nyingi za kutosha na hasa zingine kutoka wahisani wetu kutoka India, sasa fedha nyingi zinapelekwa katika suala zima la mradi wa Ziwa Victoria na bahati nzuri mnafahamu mradi ule umezinduliwa rasmi. Naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule kupitia Wizara ya maji utatekelezwa kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Uyui na Mkoa mzima wa Tabora kama ulivyokusudiwa wakati wa uzinduzi wa mradi ule.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu umekwisha, tumebakiwa na dakika 10 tu na bado tuna maswali. Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

Na. 397

**Ulinzi na Udhibiti wa Misitu Nchini**

**MHE: YUSSUF SALIM HUSSEIN** aliuliza:-

Kuongezeka kwa idadi ya watu na ukosefu wa ajira kwenye sekta nyingine kumechangia sana jamii kubwa ya watu kujikuta kwenye shughuli zinazosababisha uharibifu wa misitu kwa ajili ya kumudu maisha yao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza udhibiti na ulinzi pamoja na upandaji miti nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na ongezeko la vitendo vya baadhi ya wananchi kuvamia na kutumia maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori kinyume cha sheria na kufanya shughuli za kibinadamu kama vile kulima, kufuga, kuchimba madini na kuvuna mazao ya misitu kama vile mbao na magogo kwa visingizio mbalimbali ikiwemo ukosefu wa maeneo ya kufanya shughuli hizo.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kutumia Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kudhibiti hali hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya doria za mara kwa mara, kukamata wakiukaji wa sheria na kuwachukulia hatua mbalimbali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuboresha usimamizi wa misitu na kusisitiza kuhusu mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara inaendelea kuboresha utekelezaji wa jukumu hili kwa kuongeza idadi na umahiri wa watenda kazi wa uhifadhi, kuongeza vitendea kazi na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo za Serikali za kuimarisha ulinzi kwa kutumia Askari wa Uhifadhi, Wizara inasisitiza kuwa njia bora zaidi ya kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya misitu na bidhaa za misitu ni kwa wananchi kushiriki katika vita hii kwa utaratibu wa uhifadhi shirikishi. Hivyo, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa jamii na kutoa wito kwa wananchi wote kushiriki katika vita hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la upandaji miti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), imeandaa mkakati wa kuhifadhi mazingira na kupanda miti ambao utashirikisha wadau wote nchini. Serikali itaendelea kuhimiza utekelezaji wa agizo la kupanda miti kwa Halmshauri za Wilaya kote nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf Salim.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya upandaji miti katika nchi hii imeanza miaka mingi sana iliyopita, tokea miaka ya 1980 kwa miradi mikubwa ya wafadhili ambayo

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ilikuwa ni miradi ya *HASHI* na *HADO* lakini bado nchi yetu inaendelea kuwa jangwa. Hebu Mheshimiwa Waziri atuambie, hiyo mikakati hasa ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, suala la malezi bora kutoka utotoni sio kwa wanadamu tu, lakini hata kwa miti na pale miti, katika miaka mitatu ya mwanzo inapopandwa ndio inahitaji hasa kulelewa na utalaam unahitajika pale, leo Chuo cha kutoa wataalam wa Misitu cha Olmotonyi kimetelekezwa mpaka inafikia hatua mwanafunzi anajilipia mwenyewe ndio asome. Je, Mheshimiwa Waziri hii miti inayopandwa ni asilimia ngapi ambayo ina-*survive* ili nchi yetu isiendelee kuwa jangwa? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa kwamba kasi ya uharibifu wa mazingira kwa maana ya uharibifu wa misitu ni kubwa sana. Takwimu zinaonesha kwamba kiasi cha hekari 372,000 cha misitu kinaangamia kila mwaka na kutokana na takwimu hizo za uharibifu wa kiasi hicho ili tuweze kurudi katika hali ya kawaida, ili tuweze kwenda sambamba katika mkakati wa kukabiliana na hali hii tunapaswa kuwa tumepanda jumla ya hekari 185,000 za miti, hii ni sawa na miti milioni 280 kwa kila mwaka, kwa sababu zile hekari 185,000 kwa muda wa miaka 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mikakati hiyo ni ipi. Mkakati una mambo mengi, lakini kwa sababu ya muda huu nilionao kwa majibu ningeweza kusema kwamba utekelezaji wa mkakati huo utafanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote 181, kwenye vijiji vyote 3,692 na mitaa 6,538. Mahali ambako kinachofanyika ni uhamasishaji, lakini pia kutoa elimu na kuwezesha kwa namna mbalimbali ili zoezi hili liweze kufanyika kwa ushirikiano wa wananchi wote kwa ujumla nchi nzima, tuweze kufikia viwango hivyo vya kuweza kurudisha misitu katika hali yake ya kawaida baada ya uharibifu ambao nimezungumza hapo awali.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili ambalo anazungumzia malezi bora ya tangu awali, kwamba anazungumzia miti inavyopandwa iweze kupandwa na kusimamiwa mpaka iweze kukamilika. Hoja yake ya msingi ni kwamba unaweza kupanda miti, lakini ukisha panda usipoitunza humo katikati miti mingi inapotea na ili uweze kufikia malengo hayo unahitaji kuwa na wataalam watakaoweza kusimamia, pamoja na kushirikisha wananchi lakini lazima uwe na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kwa sasa hivi Serikali kwa namna ilivyojipanga kwanza tunatambua *gap* hiyo ya wataalam ni kubwa kiasi gani, kutokana na ukubwa wa misitu tuliyonayo tungepaswa kuwa na jumla ya wataalam 9,600 na ukiangalia idadi ya wataalam tulionao tuna *gap* kama 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tutatumia Vyuo vyetu kikiwemo hicho cha Olmotonyi, kwamba tunakiboresha Chuo cha Olmotonyi ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi, pia kuboresha mazingira ambayo yatawawezesha kujifunza waweze kuhitimu wakiwa na huo ujuzi na si suala la kujaza idadi tu. Kama nilivyosema kwenye jambo langu la msingi tunatakwa wawe wengi, lakini tunataka pia wawe na ujuzi ambao tunaohitaji ili waweze kwenda kushiriki katika kukamilisha malengo tunayokusudia.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu umekwisha kabisa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 398

**Hitaji la Chuo cha VETA Geita**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Mkoa wa Geita hauna Chuo cha Ufundi (*VETA*):-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA katika Mkoa wa Geita?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu Swali Na. 48 tarehe 4 Novemba, 2016 kuhusiana na ujenzi wa Chuo hiki, Serikali inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Chuo hiki kwa Mkopo wa Fedha toka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chagula.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kututia moyo wananchi wa Mkoa wa Geita, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuliona hilo tatizo letu la kutokuwa na Chuo cha VETA Mkoa wa Geita na kuweza kupanga na kuanza kujenga, sasa niulize ni lini sasa utekelezaji wake ili Chuo hicho kiweze kukamilika kwa wakati ili wananchi na watoto wetu walio wengi, vijana waweze kupata ujuzi na kujiajiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mkoa wa Geita hauna kabisa Chuo chochote cha Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kujenga vyuo vyote kwa pamoja kikiwemo Chuo cha Madini na ikizingatiwa kwamba Mkoa wa Geita ni wadau wakubwa wa madini? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa shukrani alizotupa kwa niaba ya Waziri wangu. Vilevile katika swali lake niseme tu kwamba utekelezaji huu unategemeana sana na masharti ambayo yanaendana na mtoa mkopo huo ambaye ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hatua mbalimbali zinaendelea sasa hivi tupo kwenye hatua za mwisho za kumpata Mshauri Elekezi. Hata hivyo, lazima niseme kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu kwamba sisi hatujaridhishwa na namna ambavyo taratibu za ujenzi wa vyuo hivi hususani vinne vya Kimkoa unavyoendelea, tunaona hatua zimekuwa ni za taratibu sana. Kwa hiyo, tayari tumeshawaita wenzetu ili tukae tujadiliane ili tuone namna bora ya kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na kutokuwa na chuo, nafahamu kwamba Geita tunacho Chuo Kikuu Huria. Pia katika suala la madini hii *VETA* tunayotegemea kuijenga Geita sehemu kubwa ya fani zake itakuwa ni kushughulikia masuala ya madini kwa kuwa maeneo hayo ndio chimbuko kubwa la madini katika nchi yetu kwa sasa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu suala la msingi la Geita linafanana na suala ambalo nauliza katika Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera ni Mkoa ambao una Wilaya zaidi ya saba, Majimbo nane hakuna hata dalili za kuwa na Chuo cha *VETA*. Je, Serikali inatumbiaje kuhusu Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Mzazi



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ni kweli tunahitaji kuwa na chuo kikubwa cha VETA chuo mahiri, lakini kwa sasa tunayo VETA pale Bukoba Mjini. Pia kuna chuo cha KVTC ambacho kipo Karagwe nacho tunakifanyia ukarabati mkubwa ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi, vilevile kuna mkakati wa kujenga chuo cha Kimkoa pale Muhengele ambapo tuna tatizo la barabara pamoja na miundombinu ya umeme, wafadhili wapo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba Mheshimiwa Mbunge Rweikiza ambaye anafuatilia amesema kwamba ameahidiwa kuondolewa hizo changamoto ili na sisi tuanze ujenzi mara moja. Vilevile kuna Gera ambayo pia sasa hivi imeshafanyiwa ukarabati Chuo cha Wananchi na kinaendelea kutoa mafunzo ya ufundi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha. Jana wachangiaji watatu hawakupata nafasi kwa sababu ya muda.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Ukumbini, mpaka sasa hivi orodha kamili sijaipata, lakini ipo orodha ya Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini ana wageni wake wanakwaya 35 kutoka Mbalizi Mbeya na wanachuo kumi wa UDOM wa kutoka Wilaya ya Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 64 inayosema:

*“Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge.”*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiunganisha Kanuni ya 68 inayohusu jambo lililotokea mapema ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Bunge lako Tukufu lilitoa maagizo kwamba tusiwajadili Viongozi Wastaafu, lakini kwa mujibu wa Sheria ya *The Parliamentary Immunities Powers and Privilege*, sisi kama Wabunge tuna *immune* ambazo zinatupa mamlaka tukiwa ndani ya Bunge ku-*dialog* na kujadili mambo mbalimbali yanayolihusu Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 100 inazungumza uhuru wa mawazo ndani ya Bunge. Kwa hiyo sisi kama Wabunge, uhuru wa mawazo ndani ya Bunge hili siyo *powers* ambazo tunapewa na mtu, tunanyang'anywa halafu tunarudishiwa ni *powes* za Kikatiba, ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatupa hizo *powers*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zetu zinasema hivyo kwamba tunaruhusiwa kujadiliana, Katiba inaruhusu na hizi *immune* tunazo na majadiliano tunayoyafanya haya, hatuamui kuwaondoa watu madarakani ni kushauriana ili kuliongoza Taifa tuangalie tulikosea wapi, twende wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba kwa kutuzuia tusiwajadili baadhi ya watu je, Wabunge tunanyang'anywa hizo *powers* na *immunities* ambazo tumepewa kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa kanuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hili suala linajirudia sana. *Ruling* niliyotoa jana ndio *final*. Kwa lugha ya Kibunge *ruling* niliyotoa jana ndio *final* na haina mjadala ndani ya Bunge, isipokuwa unaweza vilevile kurudi kwenye hiyo Katiba Ibara ya 100, ambayo inatoa fursa hiyo ukishuka chini, Katiba hiyo hiyo imetoa fursa kwa Bunge kujitungia

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kanuni zake za kuendesha Bunge na Kanuni za kuendesha Bunge tumezipitisha hapa na Mheshimiwa Msigwa na wewe ulikuwa ni mmoja wa Wabunge waliopitisha Kanuni zetu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, *the ruling stands*. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, orodha wa wageni imekuja. Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Dunstan Kitandula ambao ni wanafunzi na Walimu kutoka shule ya Msingi St. Joseph Millenium ya Mkoani Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 62 na Walimu Sita kutoka Shule ya Msingi Marangu Hills, iliyopo Wilaya ya Marangu, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Vile vile wapo wanafunzi 50 na Walimu watano kutoka Shule ya Msingi Mazengo iliyopo Mkoani Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 75 kutoka Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili wa Afrika Mashariki (CHAWAKAMA) Tawi la Chuo Kikuu cha St. John kilichopo Mkoani Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja za Serikali, ni Waziri wa Fedha na Mipango. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita mchangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Riziki Said Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza na Mwenyezi Mungu anijalie hilo nitakalolizungumza liwe ni haki na ukweli. Tukisimamia haki tutafikia mahali ambapo nchi hii tutaitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge inabidi turudi Majimboni kwetu tukawaombe radhi wananchi wetu. Bunge hili ndilo tulipitisha haya mambo, lakini leo wanaichukulia hii hoja kuwa ni hoja ya sehemu moja, kuona wao ndio wana hoja hii, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie kitu na Wabunge wote wanielewe, tuliapa kwa kushika *Quran*, tuliapa kwa kushika Biblia, hivi vitabu ni vya Mwenyezi Mungu na vitabu hivi havitakiwi kudanganya na kuvifanyia uwongo, mbele yetu kuna Mwenyezi Mungu. Unapoishika Biblia ukasema naapa na kumtanguliza Mungu katika Biblia halafu ukaja hapa ukazungumza uwongo ni dhambi kubwa, inabidi tukaombe radhi hiyo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unashika *Quran*, ukasema naishika *Quran* kwa kuahidi na kuilinda kwa mujibu wa Sheria na Katiba halafu baadaye ukaja kuibadilisha kwa kuzungumza vingine hii ni laana kubwa. Kila siku unasema tumerogwa na nani? Imeturoga *Quran*, imeturoga Biblia. Mara nyingi ukiwa mkweli, unakuwa hukubaliki mahali popote pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi ni Mwenyekiti kipindi cha tatu hapa ndani na baadhi ya Wabunge tupo ndani kwa muda mrefu tunayaona haya.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Hata hivyo, kuna wakereketwa na wanaharakati walionyesha hii hali kuwa hali ya madini ni ngumu, nataka niwataje kwa majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla Ubunge wake ulikuwa wa tabu kwa vile aliyasimamia kwa dhati kuhakikisha madini haya hayaharibiwi wala hayachakachuliwi, alipigwa mabomu, akadhallishwa inabidi aombwe radhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kafulila alisimamia kwa dhati akaitwa tumbili humu ndani. Mheshimiwa Zitto Kabwe alikuja na hoja nzito ambazo zina mashiko lakini siku ya mwisho ndio inakuwa hapana na hapana inakuwa ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Rais ameonesha ushujaa kwa kukubali maamuzi na matakwa ya Wanaharakati hawa na akayafanyia kazi ndiyo hayo unayoyaona maamuzi mazuri yanakuja sasa hivi. Hivyo siyo hoja ambayo imeletwa na upande mmoja, hii ni dhambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, jina nililopewa ni jina la sura pana, mnalikumbuka au hamlikumbuki Wabunge? Maana yake nilikuwa nasema kuna baadhi ya Wachina walikamatwa Arusha na madini ya *Tanzanite* ikasemekana hawajui Kiswahili na Kiingereza, wakaachiwa yale madini. Tulikuja kuhoji hapa ndani mwisho wa siku tukasema ndio akapita Mchina akaenda zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikamatwa Wachina na pembe za ndovu Rukwa, shahidi ni Mheshimiwa Jenista Mhagama nilikuwa naye katika ziara. Lori la pembe alilokamatwa nalo yule Mchina ikasemekana hajui Kiswahili na Kiingereza, Mheshimiwa Jenista ni shahidi na tulikuwa na Mheshimiwa Lekule Laizer, lakini mwisho wa siku tukasema ndio na hapana ikawa hapana. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikie mahali, juzi nilitoa taarifa nikasema mtakuwa tayari wenzetu penye ndio kusema hapana? Maana yake msiburuzwe kwa ndiyo wakati kuna hapana ndani yake. Kulikuwa na baadhi ya Wabunge walikuwa wanaona hiki kama tunachokifanya hiki ni dhambi kwa wananchi, sasa leo mnailetaje hoja hii ikawa ni hoja ya upande mmoja? Haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ni ya Magufuli na wanaharakati na msichukulie kama hoja ya kisiasa Wabunge wote iwe wa Upinzani, iwe wa CCM tushirikiane kwa hili. Unapoleta uchumi bora, huleti kwa upande mmoja ni kwa Watanzania wote, leo tunaiona Bulyankhulu watu ni maskini, unaiona Geita watu ni maskini, lakini umaskini huu umesababishwa na mikataba yetu mibovu na sisi wenyewe kusema ndio wakati ni hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tumeumbuka, kwa aibu hii hatuna haja ya kufumba macho na kupepesa macho, tuwaombe radhi wananchi. Narudia tena Wabunge tumeumbuka kwa hili, hakuna haja ya kupepesa macho, wala kumwambia mwenzako kumkodolea kwamba ni hoja ya CCM au hoja ya CUF au hoja ya CHADEMA, ni hoja ya Wabunge wote tumekosea humu ndani. Watu wengi walikuwa wanaangalia *conflict of interest* na *conflict of interest* ikajengea hoja tunaitana pembeni jamani tukubali, wakati unajua kabisa hiki ni hapana, hizi ni dhambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa idhini ya Sheria za Bunge tutoe hii Kanuni ya kushika *Quran* na Biblia itatulaani humu ndani. Tunashika Biblia wakati Biblia haitamki uwongo, tunashika *Quran* haitamki uwongo, leo tunatamka uongo halafu baadaye tunakula matapishi, tunageuza leo, tunabeza na kukebehi na kuona wenzetu hawana hoja. Nani humu ndani atamwomba radhi Mheshimiwa Kafulila? Nauliza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba radhi Kafulila kwa vile Mheshimiwa Kafulila ameonewa wakati alikuwa analeta hoja ya kuisadia nchi hii. Tulikuja na hoja ya *Tanzanite*,

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*Tanzanite* inatoka Tanzania, mimi nilikuwa New York pale karibu na *UN* nje kuna maduka ambayo yanauza madini, *Wallah* *Tanzanite* hiyo inaonekana inatoka Kenya, inatoka India, inatoka South Africa, niliuliza kwani hakuna *Interpol*? Jibu halipatikani, lakini leo hapa watu wanataka kufumua mapafu kuzungumza uwongo, dhambi kubwa sana na itatulaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimshukuru na nimpongeze Rais Magufuli kwa vile amethubutu na sisi wote tuungane kwa pamoja bila unafiki kumpongeza kwa kazi anayoifanya kubwa na inahatarisha maisha yake. Hivyo kila Mtanzania amwombe huruma kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo nakuja katika hoja iliyopo mezani. Leo tunasema tunataka uwekezaji wa viwanda, katika viwanda tumeona *A to Z* imekuja kufanya semina ngapi hapa ndani? Wanakuja wageni wanaingiza vyandarua bure, hawana tozo, yeye analipa bilioni 17 wale watu wameachiwa vilevile waingize vyandarua hakuna mahali palipobadilishwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wa Fedha tulikuwa naye katika semina ,akasema atalifanyia kazi, lakini nimeangalia katika vitabu hawa *A to Z* wameachwa hivi hivi, kiwanda chao kinakufa, wanalipa kodi, wana madeni na marekebisho hayajafanywa. Naomba Serikali hii kama tunavyosema ni Serikali sikivu iangalieni *A to Z* ili angalau yale maombi yao yasikilizwe yafanyiwe kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko humu ndani ya Bunge miaka mingi tumezungumzia suala la *Dinosaur*. *Dinosaur* yupo Ujerumani sisi hatutaki mjusu aje Tanzania lakini je, hata mrabaha haiwezekani? Tunakimbizana na mama lische, tunakimbizana na watu wa mitumba, leo kuingia ndani ya *exhibition* unatoa *Euro* 24 kwa watu wazima na *Euro* 12 kwa vijana lakini watu wa ndani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna orodha ya wageni ambayo tumeipata sasa hivi, Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, ana wageni wake kutoka Tanga ambao ni *Al-madrasatul Shamsiya* au *TAMTA* Tanga wako ukumbini. Karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Gekul ajiandae Mheshimiwa Ngeleja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nichangie machache katika bajeti ya Serikali ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Wabunge tunapokaa katika ukumbi huu kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali, lakini kwa bajeti hii ambayo iko mbele yetu ni vizuri Serikali ikawa wazi ili tuishauri na tuisimamie. Hata hivyo, kama mtaleta vitu kwa mafungu na bila kufanya *analysis* ya kina maana yake hamtupi nafasi ya kuwashauri ili mfanye vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii ambayo tunaitumia sasa ni wazi kwamba Serikali imefikia malengo kwa asilimia 70 ya makusanyo, lakini kwenye makusanyo hayo ambayo mlikuwa mnategemea trilion 29, trilion 11 mmekusanya ya kodi lakini leo mnaleta trilion 31 wakati makusanyo yetu yako asilimia 70. Mngetuambia tu ukweli, kwamba ni wapi mmekwama? Kwa sababu gani na mnarekebishaje? Kwa haya mnayotuletea kwamba kila mwaka mnakuza bajeti ambayo haitekelezeki mnawadanganya Watanzania siyo kweli. Ni bora msemi ni wapi mmekwama na tuishi *according to* bajeti ambayo tunaweza tukakusanya na tukapeleka kwenye miradi ya maendeleo, lakini kama mnataka tufanye biashara kama biashara mtapitisha bajeti hii lakini utekelezaji haupo. (*Makofi*)



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu ni bahati mbaya sana leo Serikali mnawaza kuzimisha kabisa Serikali za Mitaa. Makusanyo yenu yote mmekusanya huko mmeshindwa, mnakwenda kuchukua vyanzo vya Halmashauri zetu sasa ni kitu kinachosikitisha na nilishawahi kusema kwenye Bunge hili. Mwaka 1980 Baba wa Taifa alijuta suala zima la kufuta Serikali za Mitaa na kuondoa nguvu za Serikali za Mitaa. Wakati huo barabara zilikwama, zahanati zetu zilikwama kwa sababu fedha zilikuwa haziendi baada ya Serikali Kuu kukusanya. Hii bajeti mnyotuletea leo ni ya kuua Serikali zetu za Mitaa kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili mwaka jana mlitufukuza hapa mkapitisha bajeti, lakini mkaondoa chanzo cha kodi ya majengo. Mpaka hivi tunavyoongea mpaka leo Serikali haijakusanya, TRA haijakusanya kodi ya majengo ni bora mngetuachia Halmashauri tukakusanya. Kama hilo halikutosha hamkufanya tathmini ndiyo maana nasema mnaleta bajeti kama biashara tu kwamba muda wa kuleta bajeti umefika mnaleta bajeti hamjafanya tathmini. Leo Serikali mngelikiri tu kwamba mlishindwa kukusanya na mlifanya maamuzi mabaya kuondoa chanzo hiki katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo haitoshi kodi ya ardhi mmechukua, kodi ya mabango mmechukua, uko kwenye minada mmefuta. Naomba Waziri wa Fedha aniambie ukweli wakati anajibu hivi wana mpango gani na Halmashauri zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea mimi Halmashauri ya Mji wa Babati, nitoe tu mfano, wametuachia vyanzo viwili tu, ushuru wa soko na ushuru wa stendi. Wakati huohuo wanasema kwamba, Halmashauri zetu tuorodheshe idadi ya wazee, tuwalipie bima ya afya, wauna watu tunawalipa mishahara madereva na ma-*secretary* pale wasaidizi zile kada ambazo Halmashauri zetu zinaajiri, lakini hakuna chanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana hizi

fedha tunazoambiwa kwamba, leo naomba tu nichangie hii sehemu ya Serikali za Mitaa. Hizi fedha ambazo Serikali mnasema mtakusanya mtatuletea ni uwongo mtupu. Ninavyoongea hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nilikwenda nikamwona pale kwenye Kiti nikamweleza hata OC hawatuletei kwenye Halmashauri zetu, hivi ninavyoongea tangu bajeti hii imeanza ya trilioni 29 Halmashauri ya Mji wa Babati wametuletea OC ya milioni 26 tena ya mitihani! Hela ya Walimu wanaoenda kusimamia mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Halmashauri ukienda watu wanaandamana hakuna fedha, hatuna makusanyo, fedha zote wamechukua. Ile asilimia 30 ya kodi ya ardhi ambayo tunakusanya hata hawarudishi tena kwa Wizara ya Ardhi hawatuletei tena! Halafu wao watu wa Mungu binadamu wanasema kwamba, kila kitu kifanyike kwenye Halmashauri, miradi ya maendeleo hawaleti fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Mheshimiwa Waziri kwenye hiki kitabu, fedha zote wamepeleka zaidi ya milioni 500 kwa Jeshi. OC wanazopeleka ni za Jeshi, Polisi, ndiyo hela wanazolipa, lakini huku hawapeleki! Hakuna hela ambazo wanatuletea, leo tutawaaminije kwamba, wao tukiwaachia hivi vyanzo wataturudishia kwenye halmashari zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu wajitafakari, ni bora wakaacha Halmashauri zikakusanya kwa sababu, wao vipaumbele vyao ni tofauti na walivyoviahidi. Kwenye Uchaguzi Mkuu wakaja wakatuahidi wakasema milioni 50 kwa kila kijiji, hakuna chochote huku Mheshimiwa Waziri. Tena hajaongelea chochote! Mwaka jana wakatenga mikoa sijui mingapi kama bilioni 59, hawakupeleka kabisa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekaa Wabunge tunaulizwa, Serikali imeahidi milioni 50 kwa kila kijiji ziko wapi? Hata kuzisema tu wamekwepa, hata kuziandika tu, mwaka jana walithubutu kuandika, mwaka huu hawajathubutu hata kuandika kutaja. Wanavyoviahidi tofauti na wanavyotekeleza! Ni nini kinawaroga? Ni nini

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kinawasahaulisha? Ni kitu gani ambacho kinawafanya wasifikirie waliyoyaahidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu wametuachia kitu cha ajabu sana, wamepandisha faini za mtu ambaye ametupa takataka, labda kimfuko cha malboro amekidondosha chini, kutoka Sh.50,000/=, wamepandisha mpaka Sh.200,000/= mpaka Sh.1,000,000/=! Eti ndio chanzo wanachotuachia Halmashauri. Ni aibu kwa Serikali ambayo inawaza eti *fine* ndiyo iendeshe Halmashauri. Yaani wamepandisha eti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ile ni *By Laws* ya Halmashauri zetu, *to be honest*, tuwe wa kweli, wala hakiwahusu hicho chanzo, halafu Serikali wanakaa wanafikiria, halafu kingine, ada ya uchafu unapozolewa sokoni wamefuta, hata kuzoa uchafu hawataki tu-charge. Halafu wanaweka faini kwa kitu gani, wakati hata hizo ada za kuondoa tu huo uchafu wameondoa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nasema wakae wafikirie. Waheshimiwa Wabunge kila mmoja hapa ana Halmashauri yake, Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa Viti Maalum tunaingia, hii bajeti wale wanaosema ni bajeti ya karne, wanajidanganya na watapiga makofi watapitisha, lakini kwa upande wa Halmashauri, Serikali Kuu imeamua kunyonga Halmashauri zetu, kuchukua vyanzo vyote, wanatuachia eti tukakimbizane na wananchi, mtu ametoka hospitali kawekewa *drip* ameenda haja ndogo hapo tukam-charge laki mbili! Nani anaweza kufanya hayo? Hatuwezi kufanya hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akae chini afikirie, ushauri wangu kwa Serikali na kwa bajeti hii, wakae chini wafikirie warudishe vyanzo vyote vya Halmashauri, ili tuwasaidie kufanya maendeleo kwa sababu barabara zetu hazipitiki, tunavyoongea hatuwezi kuchonga hizo barabara wala kukarabati. Tulishauri katika Bunge hili kwamba, asilimia 70 wanazopeleka *TANROAD* wapeleke kwenye Halmashauri, 30 iwe *viceversa* kwa sababu barabara

nyingi za mikoa wameshaunganisha kwa lami. Sasa hivi waturudishie hivyo vyanzo, wabadilishe, hawakutaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachotokea sasa kwa sababu wameona kwamba, hawakusanyi huku juu mambo hayaendi, wakaunda *task force* ile ya TRA ambayo wameweka Usalama wa Taifa, wameweka Polisi huko wanakimbizana na madeni ya nyuma huko, wakati walisema hawatafufua makaburi, leo wanafufua makaburi! Wanaenda wanadai kodi ya 2011 hata wao hawakuwepo kwenye hizo nafasi! (Makofi)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbene, Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Serukamba wajiandae.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa hii. Naanza kwa kuwashukuru sana viongozi wa Wizara yetu hapa, Mheshimiwa Dkt. Mpango kama Waziri, Naibu Waziri wake Dkt. Kijaji, Katibu Mkuu pia Doto James, Naibu Katibu Mkuu, Wataalam wote wanaoongoza Tume ya Mipango na Watendaji wote katika Wizara hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili bajeti hii sisi ni wawakilishi kutoka maeneo mbalimbali. Mojawapo ya mambo yanayotungoza kutafakari na hatimaye ama kuikubali ama kutoikubali bajeti hii ni pamoja na kuona mambo ambayo yamezingatiwa katika maeneo yetu ya kazi tunakotoka pamoja na mambo ya Kitaifa. Naanza kwa kusema naungana na wale wote ambao wanaiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja kwa sababu, kule Jimbo la Sengerema ambako mimi nawakilisha, yako mambo ambayo yamejitokeza moja kwa moja kwenye bajeti hii na nitasema kwa ufupi sana. (Makofi)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwa nini naiunga mkono bajeti kwa sababu, naona sekta ya maji. Nampongeza sana Mheshimiwa Injinia Lwenge na Msaidizi wake kule Sengerema ule mradi mkubwa kabisa ambao unaongoza kwa ngazi ya Halmashauri na Wilaya Tanzania umeshakamilika sasa uko hatua za mwisho mno. Baada ya hapa nina hakika kwamba Viongozi Wakuu wa Serikali watakwenda kuuzindua na mimi nawakaribisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule sasa unapokamilika tunaanza kuufungua kuwafikishia maji wananchi wanaozunguka Mji wa Sengerema na maeneo mengine. Sio hivyo tu, kuna miradi kadhaa imebuniwa inayotokana na chanzo cha Ziwa Victoria. Kwa hiyo, hivi tunavyozungumza bajeti hii naiona Sengerema imezingatiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kufika Sengerema unapotokea Mwanza lazima uvuke Ziwa. Tuna barabara ya Lami ya Kamanga – Sengerema pale, nimezungumza na *TANROADS* wametuahidi kwamba, mwaka huu wa bajeti unaokuja, mwaka mpya wa fedha, wataanza kushughulikia ujenzi wa lami. Pia, tuna vivuko, kutoka Mwanza kwenda Sengerema unavuka kwa kutumia njia mbili, kuna Kamanga pale kwenda Sengerema, lakini pia kuna njia ya Busisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale Busisi kuna mambo mawili yanafanyika kuanzia Kigongo, Jimbo la Misungwi; kwanza kuna ununuzi wa kivuko kipya, naipongeza sana Serikali, lakini pia kuna *ferry* tatu zinafanya kazi pale, zinafanyiwa matengenezo na bajeti imeonesha hivyo. Ndio maana nasema katika mazingira hayo hakuna namna nyingine, isipokuwa kuiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maandalizi ya ujenzi wa daraja kubwa, kilometa 3.5 unafanyika pale kwenye kivuko kati ya Kigongo kwenda Busisi ambako ni Jimbo la Sengerema. Yote haya ni maandalizi yanayofanywa kupitia

bajeti hii ya fedha. Kwa nini wananchi wa Sengerema tusiunge mkono? Tuiunge mkono kwa sababu tunaona tunafaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ina mambo mengi, lakini lingine mojawapo ambalo ni baadhi ya mambo machache ambayo yamenifurahisha na mimi naungana na wenzangu ni kuwatambua rasmi wafanyabiashara ndogondogo, maarufu kama Machinga, lakini wanaofanya kazi za kujendeleza wenyewe na kuchangia uchumi wa Taifa. Ni jambo muhimu na lazima tuliheshimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imepunguza ushuru wa mazao, kwa sisi tulioko kule vijijini tunafahamu. Inawezekana tukaongea katika lugha tofauti kwa sababu tunatoka maeneo tofauti, watu wa mjini watatuuliza mambo ya mjini, lakini sisi tunaotoka Majimbo ya vijijini tunafahamu kero ambazo zimekuwa zikiwagusa wananchi eneo hili. Kushusha ushuru wa mazao mpaka mzigo uzidi tani moja ni jambo kubwa sana. Tunasema mazao ya biashara ni asilimia tatu na mazao ya chakula asilimia mbili, hili ni jambo kubwa tunaishukuru sana Serikali kwa kuja na mapendekezo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Sh.40/= pale, tumesema kwenye utaratibu wa *Road License* sasa ziende kwenye maji. Nasema tufanye uamuzi mgumu, lakini kwa sababu naiona neema inakuja labda tusifike huko, nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Shabiby juzi aliongea vizuri sana hapa, kwamba zile Sh.40/= tunazoziongeza zilikuwa kwenye utaratibu wa kawaida, lakini tumekuwa na kilio cha kuongeza Sh.50/= kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Maji kule. Sasa kwa sababu naiona neema inakuja saa nyingine tusifike huko, lakini ukiniuliza mimi ningesema ushauri wangu ni kwamba, hata ile Sh.50/= ambayo tulikuwa tumeikusudia, tuliyoichangia sana kabla ya bajeti hii tuiongeze kule ziende zote kwenye maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia na dunia nzima inafahamu, Bunge jana tumetoa pongezi kwa Mheshimiwa

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Rais kwa kazi kubwa aliyofanya katika kudhibiti na kuisimamia vilivyo bora zaidi sekta ya madini. Naungana na Watanzania wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi aliyofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nilichangia hapa nikasema kwa hali tuliyofikia sasa hivi tunahitaji tu maamuzi ya usimamizi wa sheria na sera tulizonazo. Moja ya jambo nililozungumza kupitia kile Kifungu cha 11 cha Sheria ya Madini kinaruhusu kabisa kuipitia mikataba hii, lakini nikasema hata ushiriki wa Serikali kuwa na hisa katika makampuni haya kupitia Kifungu cha 10 tunaweza kabisa kuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo haya na nazungumza mimi nikiwa na Kiapo cha Bunge, lakini pia niko chini ya Kiapo cha Serikali, nilishawahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini kwa miaka mitano na nusu. Nazungumza nikifahamu michakato, tungefuata utaratibu wa kawaida wa kuanza mchakato wa kuwaalika wawekezaji tushauriane namna ya kuboresha mikataba hii, ingetuchukua miaka. Mheshimiwa Rais ameturahisishia, jana tumesikia wote na dunia imeelewa kwamba, ndani ya wiki mbili hizi mazungumzo yataanza na upo uelekeo wa kuelewana katika hali ya kuwa na *win-win situation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumepitisha Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais JPM, lakini ilikuwa ni kabla ya Taarifa ya Mheshimiwa Rais. Kuna utamaduni umezoeleka duniani kwamba mambo makubwa yakifanywa na Viongozi Wakuu wa nchi kwa pamoja, kuna utaratibu na hasa kama hili Bunge, tunaweza sisi, sisi ndio wawakilishi wa wananchi Tanzania nzima. Wapo Wabunge hapa wana simu za kumpigia Mheshimiwa Rais moja kwa moja kumpa pongezi kwa kazi anayofanya, lakini wengine hata namba yake hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaowakilisha wawakilishi wa Watanzania, nilikuwa naliomba Bunge lako dakika moja, tumpe *standing ovation* Mheshimiwa Rais kwa

wale tunaoguswa kuonesha sisi kuguswa kwetu kwa namna ambavyo tumeunga mkono na tumhakikishie kwamba, tuko pamoja. Tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya, tumuunge mkono kwa niaba ya Watanzania wote tunaoguswa na jambo hili, tumhakikishie kwamba vita hii sio ya kwake peke yake ni ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hilo. Kwa kufanya hivyo, hatufanyi kwa sababu ya *favour*, lakini kwa sababu ya kutambua kazi kubwa anayoifanya. Kupambana katika sekta hii na mmeona katika mitandao inasemekana zipo familia mbili ambazo zimeamua kudhibiti madini yote duniani, lakini Mheshimiwa Rais anaungana na kundi la viongozi duniani ambao wana uthubutu na wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo la kwanza, tunafahamu historia ya Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere alivyopigana katika mawimbi mazito sana akaifikisha nchi hii hapa, lakini ukienda Marekani kuna Rais yule mnafahamu, Rais Franklin Roosevelt alikamata ile nchi akaongoza hata zaidi ya kile kipindi ambacho yeye kwa taratibu za Kimarekani kilikuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Franklin aliichukua nchi ikiwa katika hali ngumu sana na akaanzia pale ambapo Marais waliokuwa wamemtangulia, akaivusha Marekani mpaka kifo kilipomkumba. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli amejitoa muhanga kwa niaba yetu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda China, Mao Tse Tung kuanzia mwaka 1949 walivyofanya mapinduzi China aliongoza lile Taifa mpaka mwaka 1978 akaja kiongozi, Mwanamapinduzi, akaanzia pale alipokuwa ameishia Mao Tse Tung akaichukua ile nchi, anaitwa Deng Xiao Ping, aliichukua ile nchi ni miaka ishirini na kitu tu, China ikabadilika sana kuanzia mwaka 1978 mpaka 1989 alipokuwa anaachia



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

nafasi. Kwa hivyo, duniani kunawezekana. Nenda Singapore kuna yule Li Kuyan Yew ameichukua ile nchi akaibeba kutoka ilipokuwa ikafika hapa ilipokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, mambo haya yanawezekana. Mheshimiwa Rais Dokta John Magufuli...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Rais anaichukua nchi akijenga msingi kuwa...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nikasema ni muhimu sana kutambua mchango wake na...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngeleja subiri kidogo.

**TAARIFA**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba yeye ni miongoni mwa Wabunge waliotajwa katika kashfa hii ya makinikia. Sasa atuambie anapokuwa anachangia kidogo atoe ufafanuzi uhusika wake katika hili la makinikia kwa sababu amewahi kuwa Waziri. Naomba tu aweze kutoa ufafanuzi ili Watanzania waweze kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Mheshimiwa Ngeleja hiyo siyo taarifa, endelea. *(Kicheko)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mdogo wangu Mheshimiwa Haonga anafahamu kutuhumiwa siyo kupatikana na hatia, maisha yanaendelea na kazi inaendelea, tunazungumzia maslahi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini suala la *standing ovation* na *interception* ya Taarifa ya Mheshimiwa Haonga inalinda muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwa hii, hatua tulipofikia hapa ni nzuri sana. Pamoja na kwamba, hatujajua tutapata kiasi gani, lakini tunakoelekea ni kuzuri na Mheshimiwa Rais amethubutu na sote tunaungana kama Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye bajeti. Tunapozungumzia Tanzania ya Viwanda tunazungumzia yako mambo ambayo lazima yafanyike. Huwezi kuzungumzia nchi ya viwanda bila kuwa na umeme wa uhakika. Nataka niseme ninachokifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu sasa linakwenda kufumuka kwa maendeleo. Unasikia sasa hivi Mheshimiwa Rais jana ametuambia akiwa na Mwekezaji ambaye ni Rais na Mwenyekiti wa Barrick amesema kwamba, pamoja na mambo mengine ambayo tutayajadili ni pamoja na ujenzi wa *smelter*, kunahitajika umeme mkubwa sana, lakini nimesikia reli itakayojengwa itatumia treni inayoendeshwa kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Rais wa Rwanda kule amesema wanaisubiri reli hii inakwenda, unahitajika umeme mwingi sana. Unapozungumzia viwanda unazungumzia umeme mwingi, ushauri wangu kwa Serikali, lazima sasa kama ambavyo tumeji-*commit* kwenye bajeti hii, tuishirikishe sekta binafsi tusaaidiane na Serikali kuwekeza katika vyanzo vya kuzalisha umeme, kwa sababu vinginevyo hatutaweza kuhimili hiyo kasi inayokuja. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, hapa sasa hivi kuna miradi inatekelezwa pale Kinyerezi *One* mpaka Kinyerezi *Six*. Naomba, kama inawezekana kwa sababu, wapo Wakandarasi kwa mfano wanaomalizia ile Kinyerezi *One*, Serikali imeingia nao utaratibu wanajenga, naishauri Serikali wakati tunaishirikisha sekta binafsi pia, inaweza kuwa-*engage* hawa Wakandarasi kwa utaratibu kwa sababu, ndani ya miaka mitatu tunaweza kufanikiwa kumaliza mradi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba la gesi ambalo limejengwa miaka michache iliyopita na mimi ambaye nilisimamia katika eneo hilo nafahamu, sasa hivi wamesema limetumika asilimia sita tu asilimia 90 haijatumika, inahitaji vyanzo vingi vya kuzalisha huo umeme ili uwafikie wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hii tuna vyanzo vingi vya nishati, tusitegemee gesi peke yake kwa sababu, kwanza gesi ina bei juu kidogo kuliko vyanzo vya maji. Leo hapa tuna Bonde la Rufiji inafahamika, kuna mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge*. Nakumbuka mpaka mwaka 2012 tulikuwa tumeshaanzisha mazungumzo na Wabrazil walikuwa tayari kuja kuungana na sisi, una uwezo wa kuzalisha *megawatt* 2,100. Nchi hii kwa *potential* tuliyonayo kwenye sekta ya umeme unaoweza kuzalishwa kutokana na maporomoko ya maji ni zaidi ya *megawatt* 4,600. Naomba Serikali ifunguke kote kule twende tukatumie vyanzo vyote kuhakikisha kwamba, nchi hii inafikia lengo lililokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudie tena kusema umuhimu wa sekta binafsi ulivyojionesha, Mheshimiwa Waziri ameonesha utayari huo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Mbene, ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea. Nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wote kwa bajeti nzuri ambayo inaelekea sana katika mfumo mzima wa kuboresha viwanda katika nchi yetu. Napenda vilevile kumpongeza Rais wetu wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa hatua na ujasiri aliouchukua kusimamia rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuwa watu walewale ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakipigia kelele suala hili mara wamegeuka sasa wanaona kuwa ni vibaya lakini tuyaache hayo, wale wenye macho wameona, wenye masikio wanasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitishiwa hapa kama ambavyo Viongozi wa Afrika huwa wanatishiwa wanapojitokeza kupigania rasilimali za nchi zao kuwa, watahitakiwa, hii ni mikataba mikubwa sana, haya ni Mataifa makubwa sana, hamuwezi kuwachezea hawa, wanaweza wakawafanya hivi, wakawafanya vile!

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tumeona, huyo Rais wa *Barrick Gold* badala ya kutushtaki kaja mwenyewe, nginja-nginja na ndege yake mwenyewe kaja hapa anasema tuongee na hatujaambiwa, tumemsikia kwenye *youtube* anaongea! Tuongee tuangalie tunachotakiwa kuwalipa tuwalipe, sasa kiko wapi cha kushtakiana? Hatuwezi kuwa tunaishi kwa uwoga wakati rasilimali ni zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Magufuli endelea baba,

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

sisi wananchi wako tuko nyuma yako, tunakuamini na tunajua unalolifanya ni kwa ajili yetu sio kwa ajili ya binafsi yako na familia yako. Endelea kutetea maslahi hayo kwa sababu huu ndio wakati muafaka, hukuwekwa pale kwa bahati mbaya, Mungu kakuweka hapo akijua makusudi gani anayo juu yako wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaosema tunaendela kuibiwa, sijui kama wametambua kuwa katika yale mapendekezo ya Kamati ya Profesa Osoro kuna suala la kuzuia sasa madini yasisafirishwe nje moja kwa moja. Zinaenda kutengenezwa *clearing houses* na kila yanapoodolewa madini yatafanyiwa ukaguzi na asilimia moja itatozwa palepale kwa ajili ya ukaguzi huo kwa thamani ya madini yanayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kuiomba Serikali ni kuwa mfanye haraka hizo *clearing houses* ziwekwe na tayari hili zoezi lianze kusudi madini yasiendeleo kutoka. Siamini hawa jamaa wana ujasiri wa kuendelea kutuibia harakaharaka baada ya kuona eti kuwa sisi tunawadhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudi sasa kwenye masuala mazima ya hotuba yetu. Miradi ya kimkakati ni miradi ambayo imekuwa ikizungumzwa kwa miaka mingi sana. Hebu sasa Serikali amueni jambo moja, malizeni zile taratibu zote zilizobakia ambazo ni chache sana za mikataba ya uwekezaji, za maeneo ya uwekezaji, taratibu za ulipaji wa fidia, ili sasa hii miradi ya kimkakati ianze kufanya kazi kwa sababu moja kubwa, miradi hii ikitanza kufanya kazi suala zima la uchumi wa viwanda litakuwa dhahiri zaidi, maana hivi ndio viwanda mama vitakavyozalisha *input* za kuingia katika viwanda vyetu tunavyovitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme tayari tunao wa kutosha, miundombinu ya barabara imeshatengenezwa ya kutosha, reli imeshaanza, tunachongojea sasa ni hii miradi mingine ya kimkakati ambayo sasa itashirikiana katika kuhakikisha kuwa viwanda vyetu vinawezekana.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maeneo maalum ya kiuchumi. Serikali ilituanishia maeneo maalum ya kiuchumi karibu nchi nzima, ilikuwa ni jambo jema sana, yenyewe pia yamesimama kwa muda mrefu. Hebu Serikali waje sasa na bajeti hata kama watakwenda kukopa, wamalize masuala ya fidia na miundombinu muhimu katika maeneo haya, halafu wayatangaze kwa sekta binafsi ya ndani na ya nje waje wawekeze ili wananchi kwanza wapate ajira lakini vilevile wapate mapato na nchi yetu iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala la *PPP*, najua kuwa *PPP* labda ni dhana ambayo haijatambulika vizuri au haieleweki vizuri kwetu. Hebu tutafute jinsi ya kuboresha uelewa wetu wa *PPP* tupate mafunzo Serikalini na sisi Wabunge vilevile tupate mafunzo ya kutosha, tujue jinsi gani ya kushauriana na hawa wawekezaji wanaokuja kuingia mikataba hiyo na sisi ili tupate mikataba ambayo itatunufaisha sisi wote. Kwa hiyo naomba *PPP* isitupwe pembeni tu kwa sababu hatuifahamu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala zima la ukusanyaji wa mapato hasa kwenye Halmashauri. Tunashukuru sana Serikali kwa hatua ambazo wameziainisha ambazo wanaenda kupunguza tozo mbalimbali. Vilevile tunaomba sana kwa yale maeneo ambayo wamepunguzia Halmashauri uwezo wa kukusanya wenyewe, hebu watuhakikishie watakuwa wanaturudishia hizo fedha kwa muda mfupi kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wanavyofahamu hata sasa hivi Halmashauri zetu nyingi zinajiendesha kwa shida sana kwa sababu vyanzo vingi vilikuwa vimechukuliwa na Serikali Kuu. Wafanye hima watakapokusanya tu waturudishie, kama vile ambavyo kila mwezi wanatangaza wamekusanya kiasi gani basi mwezi huo huo watuambie na Halmashauri wanapeleka kiasi gani. Mambo yote sasa hivi ni kielektroniki, sioni kama kutakuwa kuna ugumu katika kurudisha hizo fedha kwa wakati. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya kupunguza kwa tozo, *crop cess*. Nafikiri katika Kamati ya Bajeti tulipendekeza kuwa kusema kuwa wanapunguza tozo peke yake na kuainisha kuwa mazao yawe ni chakula na mazao yawe ni biashara inaweza ikaleta mkanganyiko na vilevile ikatumika vibaya. Waweke tozo moja na kwa vyote ili ijulikane kuwa *whether* inatumika kwa chakula *whether* inatumika kwa biashara tozo ni hiyo moja. Wasitoe mwanya kwa watu kuanza kucheza na hiyo dhana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ufuatiliaji wa mapato na tathmini zake. Tumekuwa mara nyingi tukikadiria mapato tutapata kiasi gani kwa vyanzo mbalimbali, lakini je tunafanya tathmini labda ya miaka miwili, mitatu kuona kuwa pamoja na kuwa tulikuwa tumeweka maoteo fulani tumekuwa tumefikia kiwango hiki tu, ili itusaidie tunapopanga tupange kwa uhakika zaidi kwa uhalisia zaidi tusipange kwa vitu ambavyo pengine hatutaweza kufikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia masuala ya elimu ya walipakodi na hasa kwenye masuala ya sekta isiyokuwa rasmi. Sekta isiyokuwa rasmi ni kubwa na itaendelea kukua na itaendelea kuwepo. Ni muhimu sasa kuhakikisha kuwa pamoja na hili suala la kuanza kuwaorodhesha au kuwa-*register* basi tuanze kutoa na elimu ya kulipa kodi, tuanze kuwaelekeza kodi zitakuwa za namna gani, watazilipa kwa mfumo upi, watazilipia sehemu zipi. Maana kodi zilizopo ni nyingi na zina sehemu nyingi mbalimbali za kwenda kulipia. Huu kwanza ni usumbufu lakini vilevile inaleta hali ya mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana watakapokuwa wakitoa elimu ya kulipa kodi wahakikishe kuwa wajasiriamali hasa wadogowadogo wanatambua kwanza wajibu wao wa kulipa kodi lakini kuwa watalipa kodi za aina gani wapi na kwa mtindo upi. Hii inatuhakikishia kuwa watu wengi watalipa kodi wakijua kuwa ni wajibu wao na siyo za usumbufu. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata kwa walipa kodi wa kawaida kwa wengine bado elimu hii haijaenea ndio maana bado kuna *resistance*, lakini nafikiri kwa kuongeza juhudi za *TRA* za kutoa elimu badala ya kujikita kwenye redio na kwenye *TV* peke yake itasaidia zaidi. Ningependa vilevile, kupendekeza hata mashuleni sasa suala la elimu ya kulipa kodi lianze kuwekwa ili watoto wakue wakiamini kuwa kulipa kodi ni sehemu ya kuchangia maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia sana kuzungumzia suala la Ileje. Ileje ni Wilaya au hata Mkoa nzima wa Songwe ni mkoa ambao unazalisha sana mazao mbalimbali ya biashara na ya chakula. Mungu ametujalia kuwa na hali ya hewa nzuri sana, lakini hatuna masoko ya uhakika kwa mfano kahawa. Kahawa yetu lazima ipelekwe ikaweke kwenye mnada wa Kilimanjaro. Hiyo inatuletea.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, ajiandae Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya. Sisi wananchi tulioteseka na machimbo na wawekezaji wakubwa wa migodi tunamwomba aendeleo kukaza buti, sisi tuko nyuma yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatake Watanzania kuuona Upinzani wetu ulioko Tanzania kuwa ni kama maigizo. Watu wanaingia humu ni kwa sababu tu pengine ya kutafuta maisha, lakini hawana nia thabiti ya kulikomboa Taifa hili. Lingine wajiulize hawa ndio Wabunge wanaowatuma kuja kuwakilisha, badala ya kushughulika na matatizo yaliyoko kwenye Majimbo yao wanahangaika na kutetea wezi. (*Makofi*)



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliwahi kusema kwenye mchango wangu kwamba tunafahamu na wengine tumeshuhudia sikupata nafasi na kuwataja na wakiguna naweza kutaja, kwamba watu walivuna mpunga sasa mpunga ule jinsi ya kuurudisha inakuwa ni vigumu, kwa hiyo wanataka kufa na tai shingoni. *(Makofi\_*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais kazi aliyoifanya ni fundisho hata kwa Upinzani. Namshukuru Mama mmoja kule nyuma amesema suala hili liwe la wote. Hata mimi nakubaliana na tumekuwa tukiomba sana sisi Wabunge wa CCM kwamba, tumuunge mkono Rais kwa jitihada aliyoifanya wakawa wanatupinga. Toka mwanzo nilimsifu sana Mheshimiwa Ole-Millya yeye aliunga mkono. Wengine wote humu mlitolewa na Mheshimiwa Ester Bulaya kama watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa sababu imeonekana na Wazungu wamekubali kutulipa wanakuja humu kupiga makofi na kung'ang'ana na miongozo. Mimi niwaombe tu Wapinzani wa Tanzania mjifunze kwa kuona mfano kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia kwamba pamoja na kuhusiana na kodi za makinikia na sisi watu wa Geita *GGM* imetunyonya vitu vingi sana, tumepiga kelele muda mrefu, tunakosa *support* na bahati nzuri Mheshimiwa Rais anatoka kwenye Mkoa wetu. Ukiambiwa fedha tulizokwisha kulipwa kwa Geita dola milioni tatu kwa miaka miwili ukiangalia makorongo yaliyoko pale tunahitaji Serikali iunde timu ya uchunguzi kwenye mgodi pia wa *GGM* ambao upo Geita na watu wa Geita tunasema hatujafaidika kabisa na mgodi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani tulikuwa hatuna uwezo kama Halmashauri wa kuweza kupiga hesabu na Wawekezaji hawa. Tumekuwa tukilalamika sana, tunapewa pesa kama hisani na mtu anayetupa hesabu ndiyo *TMAA* ambao ni wezi wameshikwa na Mheshimiwa Rais kwamba hawafai. Kwa hiyo, tunamwomba pia Mheshimiwa

Rais aunde Tume ambayo itaenda kwenye migodi ile kuangalia kwa sababu wale tuliokuwa tunategemewa wanatupa hesabu sahihi ndiyo hao wameonekana kwenye ripoti ya Osoro kwamba hawafai, kwa hiyo, turudie hata migodi wa *GGM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie tu ninyi ambao hamuelewi migodini baada ya kauli za Rais na yule mkubwa wa Barrick kuja, jana watu wa *GGM* Geita walituita tukutane wanataka kutupa bomba la maji kwa mpango wa haraka. Tumekataa kwa nini mtupe bomba la maji, tunataka tupigiwe hesabu, haiwezekani Rais anachachamaa kushika wezi sisi tunapewa maji. Tutajitwisha ndoo kichwani tutabanana na Waziri humu, lakini Serikali iunde Tume kwenda kuchunguza mgodi mkubwa wa *GGM* ambao una mapato makubwa na una dhahabu nyingi kuliko hata Kahama. Kwa hiyo, naomba sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Profesa Osoro amekuwa jasiri, amewataja wezi, amewataja watu waliosababisha matatizo mengine tunao CCM. Tufike mahali tuambizane ukweli tuache mizaha. Ripoti imesomwa tumeangalia watu wote wenye *Degree* ma- *Professor* na wengine ambao hatukusoma na wananchi wetu kule vijijini. Halafu watu waliotajwa Bunge kutoka CCM wanaanza kuweka kwenye *twitter* wanasema mimi sihojiwi mpaka nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli wezi wana kinga gani? Kama wametajwa ni wezi haiwezekani hata kama yuko CCM. Hili siyo suala ya mzaha kuna maisha ya watu na watu tumeumia. Watu mmetajwa Wabunge wenzangu wa CCM humu halafu mtu anaanza na heshima zake, tunamheshimu kabisa Mzee wetu humu ndani ana-*twitt* kwenye *twitter* anasema mimi siwezi kuhojiwa mpaka nipelekwe Mahakamani, yeye ni nani? Kama tunataka kumaliza matatizo haya sisi wengine tuliburuzwa sana, tuliburuzwa sana miaka iliyopita watu wakafunga mikataba wakafungia Ulaya wakagawana hela na bado wanakuja kutuletea upinzani kule kwetu.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kuna uwezekano wa hawa watu kama ni Mbunge kama ni nani wakamatwe. Wanaotusumbua humu ni hawa ni hao hao wametajwa kwa professa Osoro, katajwa Mheshimiwa Kafumu, katajwa Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Chenge, wana kinga gani kama wezi? Kwani Magereza yamewekwa ya akina Babu Seya peke yake. Tufike mahali tulipigania Taifa hili, CCM siyo kichaka cha kuja kujificha wezi. Kila mwaka mtu anatajwa, kila tuhuma, yeye ni nani. Tufike mahali tuwese*serious* na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nimesoma kwenye kitabu cha Waziri, ukurasa wa 55, ukisoma pale kipengele kinasema atatoza kodi ya asimilia tano kwenye dhahabu kwa wachimbaji wadogo. Halafu Mheshimiwa Waziri akasema mwishoni, anategemea kukusanya milioni 88. Hivi anaendaje kufanya *pressure* ya kuhangaika na wachimbaji wadogo ambao kimsingi huwezi kuishika ile dhahabu. Akiweka haya masharti kuna asilimia nne ya *TMAA* kuna asilimia tano ya kwake na kuna asilimia moja ya kusafirisha dhahabu, karibia asilimia 10 wakati ukienda Kampala ni *one percent*. Sasa kwa nini Waziri, Wizara ya Fedha wasiondoe kodi zote za kuingiza dhahabu ili tukapata na watu wanaotoka Malawi, Congo, Zambia, Uganda na Burundi wakaleta dhahabu Tanzania kwa sababu hakuna ushuru, tuka-*deal* na asilimia moja tu ya kusafirisha tukapata hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Waziri aking'ang'ana na hizo kodi zake nilishasema humu ndani, hawezi kumshika msafirisha dhahabu tunajua tunavyobeba, kwa nini asilegeze masharti tukaweka *zero* halafu hii *one percent* atapata hela nyingi kuliko hizi milioni 88. Kwa hiyo, nashauri sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kufikiria na alione hili suala kwa macho mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na nimekuwa nikifuatilia taarifa zote hata alivyomtumbua Mheshimiwa Profesa Muhongo, sijui kama yumo humu ndani nina hamu naye kweli, alisema niliamini

vyeti, vyeti vimeniangusha! Juzi tena kasema mara tatu *PhD* 17. *BOTHii* ndiyo *return* yake *Ma-PhD*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali tuangalie uwezo wa mtu na ikiwezekana hata Mawaziri hawa wawe wanafanyiwa hata *interview*, haiwezekani unakuwa na watu wana *PhD* za kutisha, wanapogundua wezi hao wenye *PhD* wanaanza kututishia sisi ambao hatuna *PhD*. Hata hivyo, suala hili ni halali, ziko wapi *degree* tunazozitegemea hapa? Watu wamebeba Dokta, *PhD* sijui nini, halafu mwisho wa siku tunapopata matatizo wanatutisha wanatupeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Rais na wale wawekezaji wamekaa, watu wamekaa kimya, *PhD* tena zimerudi kwetu sisi *wajinga kusema tumuunge mkono*. Mimi nafikiria tufanye kitu cha msingi kama Wabunge. Hata kama ni kubadilisha sheria tusiadini hizi *degree*. Kuamini *degree* hizi... **(Maneo Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)**

## T A A R I F A

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba atumie angalau lugha ya staha, asiseme kwamba sasa zile *PhD* zimerudi kwetu wajinga. Sisi siyo wajinga humu ndani. Kila mmoja ana uelewa wake, kila mmoja yuko vizuri, kwa hiyo sisi siyo wajinga naomba awe na lugha ya kiasi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma endelea na lugha za Kibunge na hilo neno wajinga linatoka kwenye *Hansard*.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalitoa, lakini namshangaa kwanza yeye ana shule, amesoma ana *Degree*, niliyesema sikusoma ni mimi, sasa anawashwa kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Taifa hili, watu wengi hawana vyeti na watu wengi hawana elimu kwa kuwa Katiba ilisema watu kupata vyeo fulani inataka elimu kubwa wamefoji hizo digrii ambazo *input* yake tunaiona leo hapa. Kwa nini tusijifunze kwenye nchi zilizoendelea? Kuna nchi ambazo zimeweka watu ambao hawana hizo digrii na zinafanya vizuri. Tuking'ang'ana na hizo *degree* ndugu zangu tutakuja kupata matatizo, uwezo ni mdogo makaratasi ni makubwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kushauri kuhusiana na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano, hata kwenye ushauri wangu nilipochangia mwanzo nilisema.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi. Naipongeza Wizara ya Fedha, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wenzake kwa bajeti nzuri sana. Kwa kweli ukiangalia bajeti ya mwaka jana na bajeti ya mwaka huu tofauti naiona ni kubwa. Bajeti hii wametuskiliza vizuri sana, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, China wameanza miaka mingi sana, maendeleo unayoyaona leo China yameanza mwaka 1978 baada ya Deng kuchukua ile nchi. Deng amechukua nchi lakini kwenye Serikali zilizopita alikuwamo. Brazil unayoiona leo maendeleo yameanza mwaka 1998 baada la Lula kuchukua ile nchi, kabla ya hapo alikuwa ni Kiongozi. Malaysia unayoina leo maendeleo yameanza mwaka 1980 baada ya Mahathir Mohamad ambaye kule nyuma alikuwa ni kiongozi alipochukua nchi. Sohat wa Indonesia baada ya kuchukua nchi ndio tuameanza kuona maendeleo makubwa ya Indonesia. Ethiopia unayoina ya leo yameanza mwaka 1992 baada ya Meles Zenawi kuchukua nchi, naweza nikataja Mataifa mengi sana.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na hili kwa sababu gani Waheshimiwa Wabunge. Lazima Taifa lolote yuko mtu ambaye atakuja ndio atasababisha Taifa hilo liendelee. Nami naomba leo niseme kwamba ninayo hakika Rais Dkt. Magufuli atatupeleka kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marais wote hawa nimewataja ambao wamefanya vizuri sana kwenye Mataifa yao wana sifa kubwa tatu, wote kwa maana ya Singapore Malaysia, Indonesia kote, kazi ya kwanza walifanya waliwekeza kwenye elimu, unaona Rais Magufuli ameingia kazi ya kwanza aliwekeza kwenye elimu. Wote kazi ya pili ni kusimamia nidhamu ya utekelezaji wa kazi, tunaona leo Serikalini kuna nidhamu kubwa sana. Sifa ya tatu ya Marais hao waliobadilisha nchi zao ni suala la kusimamia mapato na rasilimali za nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Dkt. Magufuli ameamua kusimamia kwa uthabiti kabisa rasilimali na mapato ya nchi yetu kwa sababu naamini Rais anatupeleka kwenye Taifa la maendeleo. Hata hili la makinikia, hili la madini ni katika ule mwendelezo wa kusimamia mapato na kusimamia rasilimali za Tanzania. Nilisema siku ile Rais Magufuli, anaenda kubadilisha namna ambavyo uchimbaji wa madini duniani utakavyofanyika. Kwa hiyo, yeye ndio atakuwa chachu alichofanya Rais Magufuli atazisaidia Kenya, Mali, Guinea atasaidia nchi zote kwa sababu sasa wote wanakwenda kwa kuamka na ninayo hakika sasa tutapata *share* yetu na tutaendelea kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimewasilikiza sana Wapinzani. Hakuna hata Mpinzani mmoja ambaye amesema Rais Magufuli anakosea, hakuna! Hata hivyo, Wapinzani kama walivyo Wapinzani wao wameamua kuwa Thomaso. Wanataka waone yatapotokea. Kwa hiyo, nawaelewa, mashaka yao nayaelewa ni mashaka ya Thomaso. Yesu amefufuka, Thomaso anamwambia Yesu naomba niangalie mahali palipochomwa mkuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaelewa wenzetu na ndiyo maana nasema, wao wanaonesha wasiwasi lakini hawasemi kama tumekosea. Nami naamini kazi anayofanya Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli, anafanya kazi nzuri sana na Rais Mheshimiwa Magufuli anaendeleza pale walipoacha wenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kule nyuma kila Rais ataandika kitabu chake, Rais Dkt. Magufuli anaandika kitabu chake na kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Magufuli kitakuwa kitabu ambacho nina hakika kwenye historia ya nchi yetu ndio Rais tutakayesema alittoa *third world* kutupeleka kwenye uchumi wa kati kama Taifa. Jukumu letu kama wanasiasa, tumuunge mkono ili aweze kufanya vizuri zaidi huko anakokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nirudi kwenye bajeti. Naipongeza sana Serikali kwenye kubadili mfumo wa kukusanya *Road License*. Wako watu wanasema *Road License* imeondolewa; hapana, haijaondolewa. *Road License* imeletwa ili iwe rahisi kuikusanya na iwe rahisi kwa sisi tunaochangia lakini pia itozwe kwa magari yanayofanya kazi. Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naiomba Serikali tulikazanie, ni suala la deni la ndani. Leo hii ukienda nchini, malalamiko ni kwamba pesa hazipo, wanasema *liquidity* haiko kwenye *market*. *Liquidity* haipo kwa sababu watu wengi ambao wamefanya biashara na Serikali wanatudai. Naiomba Serikali ije na mkakati wa kulipa madeni ya ndani. Tukifanya hivyo, uchumi wetu utaanza kukua kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa suala la asilimia 18 ya *VAT* kwenye *auxiliary*. Sasa mnaisaidia bandari yetu, lakini naomba suala la *single custom* na *DRC* tuliiondoe ili *single custom* itusaidie na watu wengi watumie Bandari za Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Rais ameamua kwa dhati kufufua Shirika la Ndege la Tanzania na amenunua ndege kubwa. Zile ndege kubwa zitakuwa zinasafiri kwenda kwenye Mataifa makubwa duniani. Moja ya gharama kubwa ya ndege ni mafuta ya ndege. Tumeamua wenyewe kama Serikali; kama Afrika Mashariki, mafuta ya ndege yasitozwe kodi yoyote na yasitozwe *RDL*. Sisi bado tunang'ang'ania kuweka tozo hiyo. Tukiweka tozo hiyo, tunaongeza gharama za ndege. Tukiongeza gharama za ndege, tunaiumiza *tourism* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho naomba leo niseme, shirika ambalo linatoa mafuta haya ya ndege ni Puma. Puma, Serikali ina asilima 50. Ukiliongezea gharama maana yake ni nini? Maana yake, *profit and loss* yao inakuwa kubwa, maana yake *dividend* itapungua, *corporate tax* itapungua na yote haya yatapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali; na bahati nzuri Kamati ya Bajeti kwenye ukurasa wa 41 mmeliandika hili jambo; nawaombeni sana mwende kwenye *Finance Bill*. Hii ni *element* ndogo sana, tukaliondoe ili nasi tuweze kuwa *competitive* na sisi ndege nyingi ziweze kuja kunywa mafuta hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuikumbusha Serikali, kila wanapoongelea reli ya kati wanaongelea Dar es Salaam – Mwanza. Naombeni mkumbuke ni Dar es Salaam – Kigoma na matawi yake ya Mpanda na Mwanza lakini *central line* ni kwenda Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni kubwa sana, naombeni sana tuweke bajeti kubwa ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la soko la dhahabu. Musukuma amelisema hapa, tulisema mwaka 2016 na Bwana Kishimba, naombeni tuweke soko la dhahabu, halafu kwenye soko lile tuwaambie kila atakayeleta dhahabu msimwulize ameitoa wapi? Isipokuwa watakaokuja kununua ndio tuweke *export levy*. Tutakusanya pesa nyingi sana kama



Taifa. Wala siyo hii asilimia tano ya wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo watakwepa, hatutoikusanya hii hela; lakini tukiwafanya waje kwenye soko, wanunuzi wakaja, tutapata fedha nyingi sana kama Taifa. Naombeni mwende mkalifanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *ten percent ya crude oil*. Jamani, Kenya na Uganda hawana *crude oil*. Kitakachotokea, sisi tutakuwa soko la Kenya na Uganda, nasi hatuna mafuta mengi sana nchini jamani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kigoma tuna michikichi, lakini angalia mafuta ya michikichi yanayozaliwa Kigoma, huwezi kutumia hata kwa mwezi mmoja, ni machache. Nawaombeni sana tuwekeze kwenye mbegu na utafiti ili tuweze kuzalisha michikichi mingi na tuweze kuzalisha alizeti nyingi sana. Bila hivyo... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

**MWENYEKITI:** Umekwisha. Hoja zako ni nzito na muda umekwisha. Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Jasmine halafu Mheshimiwa Juma Hamad jiandae.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa tukio hili ambalo linaendelea katika harakati zile zile za kutetea na kulinda maslahi ya Watanzania ili maslahi haya, rasilimali zetu ziweze kuwatetea na kuwasaidia hawa wanyonge hasa

akinamama ambao tuna shida ya afya na maji. Mungu ambariki sana Mheshimiwa Rais wetu achape kazi, tupo pamoja naye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake kwa bajeti ambayo inatoa mwanga katika kumkomboa Mtanzania. Mambo hayawezi yakaja mara moja, ni taratibu, kwa hiyo, tuwape muda waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nijikite kwa kuondoa upotoshaji. Nimesikiliza michango mingi, upotoshaji ni mkubwa kwa kusema kwamba Marais waliopita na awamu hii wanaendeleza umaskini, kwamba wamechangia kulipeleka Taifa hili kwenye umaskini na Chama cha Mapinduzi ndiyo kinachangia katika kuletea umaskini Taifa hili. Siyo kweli, huu ni upotoshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwaambie wananchi, maendeleo yetu hadi yanafikia hapa, bajeti zetu hazitekezwi; mara asilimia 38, mara asilimia 40 ni kutokana na matatizo mbalimbali ambayo yamelikumba Taifa hili tangu tumepata uhuru hadi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu napenda nieleze kwamba viongozi hawa, tukimchukulia Baba wa Taifa amejitahidi sana kulitoa Taifa hili katika umasikini; juhudi zake wote tunazifahamu, lakini amekumbana na vikwazo vingi; vikwazo vya nje na vikwazo vya ndani. Kwa mfano, wakati tulipoanzisha Azimio la Arusha tumeona wafadhili wengi sana waki-*withdraw* misaada kwa sababu ya sera zetu. Wajerumani walitoa misaada na Waingereza walitoa misaada. Kwa hiyo, bajeti iliyumba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1970, suala la *oil* bei yake ilikuwa kubwa sana. *Export* tulizotegemea zilishuka; kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, vita ya Kagera na mambo mengine yote hayo yameyumbisha uchumi. Wakoloni nao hawakutuacha huru, wakaendeleza ukoloni

mambo leo; kila tunavyojitahidi kujikwamua na wenyewe wanatukwamisha. Kwa hiyo, haya yote yanachangia katika kufanya bajeti zetu zisiwe za kutekelezwa kiurahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1980 tukaachana na sera zetu, tukayumbishwa tena; tukaletewa zile sera za *structure adjustment policies*, tulikuwa hatutajiandaa ndiyo masuala ya ubinafsishaji, uwekezaji na hii mikataba mibovu ilipoanzia. Kwa hiyo, siyo kwamba ni mtu mmoja, ni timu ya wataalam mbalimbali. Wataalam hawa wanatoka wapi? Wanatoka kwenye vyama mbalimbali. Kwa hiyo, tusilaumiane, tuangalie tatizo ni nini? *What is the root cause* ambayo imetufikisha hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie tutawezaje kujikwamua kwa haya Mataifa makubwa na sera zake? Sasa hivi tunashindwa kutekeleza malengo yetu, tunatekeleza malengo haya ya kidunia; ile *Millennium Development Goals*, sijui kuna ile 2030, yote haya yanaharibu. Tunashindwa ku-*concentrate* kuwaletea watu wetu mahitaji ya msingi, tunafanya mambo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zote hizi ni *propaganda* za Kizungu, lazima tuzitambue ili tuweze kuleta mshikamano katika Taifa letu. Wameshatugawanya na mambo ya vyama vingi, mambo ya *NGOs* na nini; yote hii ni *divide and rule* ili waweze kutuharibia. Kwa hiyo, Serikali inapopanga, huyu anakataa, huyu anafanya hivi, kunakuwa na mvutano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni matatizo ya ndani. Tumeona mambo ni mengi lakini rushwa na ufisadi ndiyo imetupelekea Taifa hili kufikia bajeti ambayo tunashindwa kuitekeleza. Pesa zinatolewa, miradi haitekelezwi, miradi hewa na Watumishi hewa, kwa hiyo, mambo yanakuwa mazito. Je, fisadi huyu ni nani? Fisadi huyu siyo wa Chama cha Mapinduzi peke yake; sio Rais wala siyo nani; ni sisi Watanzania hasa viongozi ambao tumepewa dhamana ya kuongoza Taifa hili kwa umoja wetu ndio tumefikisha hili tatizo katika mkanganyiko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tufike mahali tujitambue. Hata kama wewe unakuwa kwenye Upinzani, hata kama wewe ni mwanaharakati, lakini kitu cha kwanza simamia maslahi ya Taifa hili, wasitugawanye. Kwa mfano, nilitegemea tungepongeza, maana wale wengine mnasema walikuwa wapole, walikuwa hivi; sasa tumempata Mheshimiwa Rais huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Bunge la Katiba kila mtu aliyesimama alisema tunataka Rais atakayethubutu, Rais sio mwoga, Rais mzalendo na anayesimamia watu na wengine mpaka wakatumia Rais mwenye kichwa cha mwendawazimu, maana yake haogopi; Rais huyo tumempata, ndio Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Anafanya kazi kutetea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea kwa mfano, juzi wakati anapambana na hili suala la madini ambalo limechukua *trillions of money* kwenda huko nje, nilitegemea Watanzania wote bila kujali itikadi zetu tungemuunga mkono. Hapa tunashuhudia Wabunge wengine wanaunga mkono na wengine wanakataa. Kwa nini? Kwa sababu tumeshagawanywa. Kwa hiyo, hali hii ikiendelea haitatuletea tija katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea wanasheria wa nchi hii wangeungana kumsaidia Mheshimiwa Rais ili kuweza kuiangalia upya hii mikataba. Hivi kama Mwanasheria anaweza akaungaunga aka-*forge* akamtetea yule muuaji kwa kutumia hizo sijui *technical* nini, kwa nini wasiungane ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kutengeneza na kutetea haki zetu ambazo zimepotea na tunazidai? Badala yake tunaanza kubeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili Taifa mimi nasema tukifikia mgawanyiko huu kwamba kwa sababu Serikali hii labda ni ya Chama cha Mapinduzi, mimi niko huku, hatutafika na hizi ni mbinu na *propaganda* za mabeberu ili watugawanye waendeleo kutunyanyasa na kuchukua rasilimali zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wenzangu, tuamke tujitambue sasa ili tuweze kuhakikisha rasilimali zetu tunazilinda. Tanzania kwanza mambo mengine baadaye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwa upande wa bajeti. Bajeti yetu ni nzuri, kwa mfano suala la kumkomboa mkulima na tozo mbalimbali. Mimi nitazungumzia suala la kodi ya majengo. Nia ni kuondoa umaskini, lakini sasa kidogo nina wasiwasi pale ambapo malipo yamewekwa kwa *flat rate* ya Sh.10,000/= na Sh.50,000/= kwa nyumba ambazo hazijathaminiwa. Naomba kuuliza, je, hizi zikithaminiwa ina maana kodi itakuwa juu zaidi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu nyumba za kuishi; leo mtu yupo kazini au amefanya biashara au leo ni Mbunge umepata mkopo ukatengeneza nyumba nzuri, baada ya hapo huna kazi, biashara ilikufa halafu nyumba ile sasa imethaminiwa ulipe labda Sh.300,000/= au Sh.400,000/=. Hii itaishia kwamba huyu mtu atanyang'anywa ile nyumba kwa sababu ile nyumba haizalishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, nyumba za kuishi zote, *contribution* ni lazima katika kuleta maendeleo; iwepo labda hata kati ya Sh.2,000/= kwa zile ambazo vigezo vyake ni vya chini, labda mwisho iwe ni Sh.50,000/= ili watu waweze ku-*afford*. *Otherwise* tutaenda tu kuuza nyumba za hawa wananchi ambao sasa hivi kazi hakuna. Unasema huyu ana mtoto, watoto wenyewe kazi hawana, tunao majumbani. Kwa hiyo, tutaishia kuendeleza umaskini. Bora mtu awe na nyumba yake, asubuhi anajua akagange vipi. Kwa hiyo, naishauri Serikali hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala maji ni muhimu sana katika ku-*stimulate* maendeleo, kwa hiyo, tunaomba sana, akinamama na watoto wetu wa kike wananyanyasika, wanapigwa, wanabakwa na ndoa zinavunjika kwa sababu ya maji. Kwa hiyo, naiomba Serikali, bajeti ya maji hii na nawaunga mkono wenzangu kwamba ile Sh.50/= iongezwe

ili akinamama waondolewe hii adha, kwa sababu pia watapunguziwa muda. *Time factor* ni muhimu sana katika suala la maendeleo. Watapata maji jirani, lakini watafanya na shughuli nyingine za uzalishaji na mambo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mazingira. Suala la mazingira linatu-*cost* sana katika nchi yetu hii. Wote tunashuhudia mazingira sasa hivi yanaharibiwa mno. Tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba... (Makofi)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Juma Hamad, halafu Mheshimiwa Kubenea jiandae.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna siku nilifarijika sana katika Bunge hili ka Kumi na Moja ni siku ambapo Katibu Mkuu wetu Maalim Seif Sharif Hamad alituita kwenda kutuasa sisi Wabunge. Hiyo alifanya baada ya kile kikao cha kuapa. Naomba ninukuu; alitueleza hivi:

“Mnapokuwa Bungeni jaribuni kuikosa Serikali ili ifanye vizuri na mnapoikosa, basi mkosoe kwa maana ya *constructive criticisms* kwamba muwashauri, kama hili halikufanyika vizuri, basi wafanye nini?” (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili akasema, “mnapokuwa Bungeni pale ambapo Serikali inafanya vizuri, basi muisifu.” Huo ndiyo ulikuwa wasia wa Maalim Seif Sharif Hamad. Wenzangu wa *CUF* kama nasema uongo wanisimamishe hapa wanipe utaratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Mama Lulida amesema, tuliapa na sisi wote ni waumini wa Mwenyezi

Mungu. Tuliapa kwa kutumia Biblia na *Quran* kwamba tutaitumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maslahi ya wananchi wetu ambao tumewawakilisha hapa. Kama hiyo haitoshi, kila siku hapa asubuhi tunasoma Dua ya kuliombea Bunge na kumwombea Rais wa Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Dua zetu za kila siku, maana nataka ninukuu kipande kidogo tu: "Ewe Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Ardhi, umeweka katika dunia yako hii au katika Ardhi yako hii Mabunge au Mabaraza ya kutunga sheria na Serikali za wanadamu ili haki itendeke kama upendavyo wewe Mwenyezi Mungu. Tunakuomba sisi Wajumbe wako utupe hekima na busara ili kujadili mambo yetu kadhaa, kadhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijadili hii bajeti ya mwaka 2017/2018 kwa mustakabali huu. Nafikiri ni vizuri kabla ya kujadili bajeti ya mwaka 2017/2018, tufanye tathmini ya bajeti iliyopita ili tujue *what went wrong in the 2016/2017 budget, what are the challenges that we faced?* Tukifanya hivyo tutakuwa tunaitendea mema bajeti ya 2017/2018. Bila hivyo, *no*, hatuitendei haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la bajeti ya mwaka 2016/2017 ni kuelekeza matumizi *in such a way* kwamba *development budget* tuitengee asilimia 40 na *recurrent budget* tuitengee asilimia 60. Sisi tulimpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa sababu kwa mara ya kwanza anazungumzia maendeleo ya watu na huko nyuma ilikuwa chini ya asilimia 40. Sasa tuje kwenye ukurasa wa 30 wa *budget speech* ya Mheshimiwa Waziri. Naomba sana kama mna vitabu mfungue ukurasa wa 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 30 kwenye *paragraph* ya 41, sitaki nisome ile *paragraph* yote, lakini kwa ufupi anachosema hapa ni kwamba *up to April, 2017* tumekusanya *20.03 trillion*. Sasa hivyo kwamba tumeweza kutekeleza *recurrent expenditure* kwa asilimia 87.4 na tumetekeleza *development expenditure* kwa asilimia 38.5.

Sasa Mheshimiwa Waziri waambie wataalam wako kule kwamba huku usifikiri Wabunge hawakusoma; sisi wengine tumeichambua neno kwa neno hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *if you add those two* ingetufanya tupate *100 percent* au tupate *less than 100 percent* kwa sababu hii ni mpaka Aprili lakini uki-*add 87.4 percent* na uka-*add* na 38.5 percent unapata *125.9 percent*. Maana yake nini? Ni kwamba kile kilichokuwa kadirio kutumika katika bajeti hii, kimetumika na tumeongeza fedha nyingine. *This is absolutely rubbish.* (*Makofi*) **(Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad hilo neno lako "*rubbish*" lifute. Lifute!

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Nimeshafuta, lakini hii takwimu siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *real* na *nominal terms*; maana kuna wakati nilisema hapa, kuna vitu viwili; kuna kitu kinaitwa *real terms and nominal terms*. *Is this budget real*, ya 2016/2017? *Is this real?* Sasa nafikiri bajeti ya mwkaa 2016/2017 *is not realistic*. Angalau hii ya 2017/2018 *now it is real*, lakini angalau ni nzuri, *it is healthier*. Uki-*compare* bajeti mbili hizi; ya 2016/2017 na 2017/2018, hii bajeti ya sasa ni *healthier* kwa sababu imewalenga wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishukuru sana Serikali kwa kubana matumizi, hilo wame-*achieve* vizuri, lazima tuwashukuru; lakini kwa maana ya mapato ambapo ndiyo msingi wa bajeti yote, bado tuna kazi kubwa. Nataka niwaambie, hakuna Serikali yoyote duniani inayoweza ku-*survive* bila *tax revenue*. Marekani imefika *stage* kwamba ikiwa wewe ni mgombea wa Urais kama ume-*evade taxes*, basi wanasema hufai kuwa Rais wa nchi hiyo. Kwa hiyo, naelewa umuhimu wa kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niseme, katika hili suala la kukusanya kodi kuna siri tatu; moja, *collect taxes*



*with minimum inconvenience to the tax payers; ya pili, kusanya kodi hizi rates za kodi ziwe affordable to the tax payers; lakini la tatu, kusanya kodi ili yule mlipa kodi aone kuna good returns katika maisha yake. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niipongeze Serikali; kwa maana ya *minimum inconvenience to the tax payers* Serikali imefanya vizuri sana. Tuna mifumo mbalimbali ya kielektroniki ambayo sasa hivi tunaitumia; juzi Kamati ya Bajeti tulikwenda kukagua ule mtambo wa *TTMS* ambao kwa kweli utawezesha kujua kodi za *operators* wa simu hawa *on timely basis*, lakini pia tuna mfumo pale katika Idara ya Forodha ambao unaitwa *TANCIS*; ni mfumo wa kielektroniki wa kujua ni nani aliyelipa kodi na wakati gani na kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba ule Mfumo wa *TANCIS* bado ni *TRA* ndiyo imekuwa nao, lakini kuna wadau wengine ambao wanapaswa kukusanya kodi kwa niaba ya *TRA*, ule mfumo hawana. Nadhani ni vizuri tuishauri Serikali hapa kwamba wale wadau wengine nao wa-*adhere to that TANCIS system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende haraka haraka. Kama kuna kitu ambacho kimesahaulika katika bajeti hii ya 2017/2018 ni suala la utalii. Mapato yatokanayo na utalii sasa hivi ndiyo mapato makubwa kwa maana ya *foreign exchange* tunayo-*earn*. Nafikiri kama sikosei, asilimia 17.5 ya mapato yetu ya nje yanatokana na utalii. Wenzetu wa Kenya wamechukua *comperative advantage*; wakati sisi tulikubaliana wote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba tutoze *VAT*, wao hawakutoza. Kwa hiyo, bei ya mtalii kuja Tanzania sasa hivi imekuwa ghali sana kuliko kwenda Hija. Tunakosa watalii wengi na huenda baada ya muda mdogo sana tukakuta mapato yetu yana-*decline* kabisa katika Sekta hii ya Utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna *comperative advantage* ukilinganisha na Kenya. *Over the years* kuanzia 2011 mpaka sasa hivi namba ya watalii *in* Kenya inapungua, sisi huku inaongezeka na inategemewa kwamba mwaka

unaokuja namba ya watalii itakuwa kama milioni moja na kitu *in* Kenya na milioni moja na kitu hapa kwetu. Kwa hiyo, kama tutajipanga vizuri, tutaondoa kodi hii *VAT on tourism*, basi nina uhakika tuna uwezo wa kukusanya mapato zaidi ya Kenya. Kwa hiyo, naiomba Serikali inapokuja na *Finance Bill* ilianganalie suala... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kubenea, halafu Mheshimiwa Cosato Chumi jiandae.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo hoja ndani ya Bunge na tokea jana na leo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wanazungumza mambo mengi juu yetu sisi upande wa pili ambao tunaambiwa hatuungi mkono juhudi za Serikali au za Rais za kutetea rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwamba sisi hatuhusiki kwa namna yoyote ile na mikataba yote ya madini iliyofungwa na Serikali hii. Hatujawahi kuwa kwenye Serikali hiyo na hatujawahi kuingia katika hiyo Serikali na kwa hiyo, hatujawahi kusaini mkataba wowote ule. Kwa hiyo, hiyo mikataba yote iliyofungwa ni ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yao. Wasichukue kesi isiyotuhusu wakatutupia sisi. Hiyo ni kesi yao, hilo ni dudu lao, wameliamsha, wamalizane nalo wenyewe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo hoja ya msingi sana kwamba eti tumeibiwa katika rasilimali zetu, kwamba tumeibiwa na watu waliokuja kuwekeza. Mikataba iliyofungwa imefungwa kwa mujibu wa sheria zilizopo. Waliofunga mikataba na ambao bahati njema mmoja wao amezungumza hakamatiki, anasema, mikataba hiyo imefungwa baada ya kikao cha Baraza la Mawaziri kukutana

na kuwepo *minutes* za vikao hivyo. Hatuwezi kusema tumeibiwa wakati tumeruhusu mali yetu wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningewaelewa sana kama tungesema mikataba iliyofungwa ni ya kinyonyaji, mimi hiyo ningewaelewa. Siyo wizi, hapa hakuna wizi! Wizi ni mtu anayeondoka ndani ya nchi yako, anagonga stempu, analipa ushuru, anakulipa hela yako, anaondoka unasema anakuibia! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kuthibitisha kwamba hakuna wizi, Rais amekaa na aliyemwita mwizi jana Ikulu. Mlango wa Ikulu jana ulifunguliwa ukawa wazi, mwizi akaingia Ikulu, Rais mwenye vyombo vya dola... (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

#### TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Kubenea, taarifa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kumpa taarifa msemaji anayeendelea kuzungumza kwamba Mheshimiwa Rais jana amekutana na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya *Barrick Gold*, sio Mkurugenzi Mkuu wa *Acacia*. Nataka nimrekebishe tu hapo.

**MWENYEKITI:** Hiyo ndiyo taarifa sahihi.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyo ndio mwizi aliyelitwa na Mheshimiwa Rais kwamba kampuni hii haikusajiliwa nchini, inatudhulumu, wamekaa naye Ikulu wakazungumza naye. Nilitegemea Mheshimiwa Rais angeenda kumweka ndani huyu mtu na akamzuia asizungumze.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma hebu kaa.

Mheshimiwa Kubenea, jenga hoja yako na *sentiments* ambazo unataka kuzitumia sasa hivi hazitasaidia hoja yako. Kwa hiyo, nakuomba elekeza hoja yako kwenye masuala muhimu ya uchumi na masuala muhimu ya mambo ambayo yako mbele yako leo. Sasa haya mambo yaliyopita tulishasema yamepita, tunakwenda mbele. (*Kicheko*)

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yako, naomba niliache hilo jambo, lakini *message* imefika. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kwenye Wizara ya Nishati na Madini nilizungumza juu ya kuwepo mgongano wa maslahi kwa baadhi ya viongozi wetu waandamizi kwenye Serikali. Bahati njema au bahati mbaya nilimtaja kaka yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa. Naye juzi akajibu hapa, akanieleza mimi binafsi nilivyo na akasema amenichangia matibabu, akasema ameninunulia kompyuta yeye na rafiki zake. Kwa kweli kama nisingelelewa katika misingi ya Uislamu ningerejesha fedha ya Mheshimiwa Mwambalaswa aliyonichangia matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikumwomba Mheshimiwa Mwambalaswa anichangie, nilikuwa kitandani ninaumwa, watu wakaomba mchango wakanichangia, lakini nimesikitika kwamba mchango alioutoa sirini amekuja kuusema hadharani ndani ya Bunge hili. Ni masikitiko makubwa sana, kwamba ukiwa na kiongozi wa namna hii siku akikuchangia maziko atakuja kukudai sanda au kuja kukudai jeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe onyo kwa Waheshimiwa Wabunge mnaochangisha michango ya harusi humu ndani ya Bunge, mkimchangisha Mheshimiwa Mwambalaswa, kuna siku atakuja kuwadai wake mnaooa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwambalaswa amesema kwenye Bunge,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea, tuendelee na bajeti, hayo ameyasema...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** *No, no, no*, Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu ziko *very clear*, kama Mheshimiwa Mwambalaswa ameyasema, kayasema yameshapita, nawe kama unavyosema ni Muislamu, huna haja tena ya kutaka kusema, atakulipia Mungu yako. Kwa hiyo, huna haja sasa ya kuanza ku-*throw back* yale ambayo amekutuhumu. Tuendelee na bajeti.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mgongano wa maslahi upo katika viongozi wetu wakubwa katika nchi hii. Mheshimiwa Ame Mpungwe alikuwa Balozi wetu wa Afrika Kusini, akawa dalali katika makampuni ya Makaburu yaliyonunua *NBC*, yaliyochimba *Tanzanite* na magazeti yaliandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la Rai lilihoji Balozi Mpungwe ni Balozi mzalendo au muuza nchi? Mara baada ya Balozi Mpungwe kustaafu akawa mmoja wa wamiliki wa makampuni makubwa ya uwekezaji wa madini katika nchi hii, *AFGEM* ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Daniel Yona aliyekuwa Waziri wetu wa Nishati na Madini alichukua dokezo akapeleka kwenye Baraza la Mawaziri la kuuza Kiwira. Kiwira ikauzwa akaanzisha Kampuni inaitwa *TanPower*, nayo ikaingia ubia na Kampuni nyingine inaitwa *ANBEN Limited*

wakauziana Kiwira. Ilivyoenda Kiwira, mnaijua. Leo tunakaa hapa tunazungumza kana kwamba hayo mambo hayapo! Eti tusijadili watu waliohusika kuingiza nchi hii katika migogoro ya kifisadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwambalaswa amesema kwenye Bunge hili kwamba yeye hakuwa na maslahi binafsi na mradi wa umeme wa upepo wa Singida, akiwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*, mimi natoa ushahidi hapa, alikuwa na mgongano wa maslahi. Mwaka 2011 kuna *invitation letter*, hii hapa, inatoka China inamwailika Mheshimiwa Victor Mwambalaswa mwenye *Passport number AD002021* iliyotolewa Januari, aliyezaliwa tarehe 08, *issued* Januari, 2006. Hii hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaliko huu anakwenda China akifuatana na William Mhando ambaye alikuwa Mkurugenzi wa *TANESCO*; na wengine ni Timothy Njunjua Kalinjuna na Machwa Kangoswe, hii hapa. Wanasema wanakwenda kufunga mkataba kati ya *TANESCO* na Kampuni ya China na Kampuni ya *Power East Africa Limited* ambayo ni yake. Anasafiri kwa fedha za Tanzania, anasafiri kwa *passport* ya Tanzania, analipwa posho ya *TANESCO*, anakwenda kufunga mkataba wa kampuni yake, halafu anakuja hapa anasema lile lilikuwa wazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa taarifa ya *NDC* inasema Mradi wa Umeme wa Upepo wa Singida *PT 33162*, mradi umeanza mwaka 2010. Maelekezo ya mradi; mradi unatekelezwa kwa Kampuni ya *Seawind Power Limited* na *NDC*; na hiyo *Power Pool East Africa Limited*, ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Mrindoko Bashiru anakuja kutoa barua hii ya kuipa kazi kampuni ya akina Mheshimiwa Mwambalaswa. Mwaka 2010, Mheshimiwa Sitta anafunga mjadala wa Richmond Bungeni kwa ubabe tu. Mwaka 2011 Mheshimiwa Mwambalaswa anakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, mwaka 2010 Mheshimiwa Mwambalaswa anakuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*. Jamani...

**MBUNGE FULANI:** Ayayayayaaaah!

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo, tunapozungumza mgongano wa maslahi ndiyo huu. Mnazungumza vitu gani humu ndani? Halafu watu wanasema hapa mnafikua makaburi, fukueni haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgongano mkubwa wa maslahi. Nina orodha ndefu ya viongozi wa Serikali hii ambao mikataba iliyofungwa nyuma yao wana mgongano wa maslahi. Hatuwezi kukaa hapa tunadanganyana kwamba Taifa hili ni letu wote wakati wengine wananufaika, wengine wanaliibia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja hapa amesimama asubuhi anasema nampongeza Mheshimiwa Rais. Namwomba Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli akaangalie fedha iliyotumika kulipa Kampuni ya *IPTL*; na Waziri wa Fedha na Mipango akaangalie. Mwaka 2010 kuelekea kipindi cha Uchaguzi Mkuu, shilingi bilioni 46 kulipia mafuta *IPTL*; kwa mwezi shilingi bilioni 15, Mheshimiwa Ngeleja akiwa Waziri wa Nishati na Madini na ndiye aliyesaini hiyo hoja; yule, Mheshimiwa William Ngeleja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka zipo, ushahidi upo! Aende, Mheshimiwa Rais ana faili huko Ikulu afungue faili la *IPTL* aangalie mwaka 2010 kipindi ambacho tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. *IPTL* imelipwa shilingi bilioni 15 kwa mwezi kuwasha mitambo ya *IPTL*. Halafu mnakaa hapa tunadanganyana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa, naviomba vyombo vya ulinzi na usalama viwachunguze hawa watu, hatuna maslahi binafsi, tunatetea maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, halafu Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Ester Mahawe. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Yatasha kwa leo. (*Makofi*)

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kupata nafasi. Napenda kuipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa jinsi ambavyo tulishirikiana wakati watu wa Halmashauri wa Mji wa Mafinga tulipopata msaada kutoka Ubalizi wa Japan. Kulikuwa na *some complications*, lakini kwa ushirikiano mkubwa tuliweza kufanikiwa kiasi kwamba tukafanikiwa kupata huo msaada baada ya Wizara kufanya marekebisho ya kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichangie katika bajeti hii kwa kuanza kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema ni wizi katika Sekta ya Madini, nilikuwa najaribu kupitia nyaraka mbalimbali, mojawapo, ni hii inasema *protecting your community against mining companies*. Katika *document* hii imeeleza kwa ufasaha namna gani makampuni makubwa ya madini yanavyofanya mbinu mbalimbali ambayo hitimisho lake ndiyo tunaita wizi. Katika utangulizi wa *document* hii anasema:

*“The company may deliberately try to disrupt and weaken a community’s ability to organize effectively against them.”* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maana yake ni nini? makampuni yanaweza yakatumia mbinu mbalimbali yakatugawa sisi ili tusiweze kushikamana katika kukabiliana na wizi mbalimbali ambao wanaufanya. Wizi huu unafanyikaje? Kwa sababu wenzetu wako mbali kwa teknolojia na mbinu mbalimbali za kufanya *international trading*. Moja, wanafanya kitu tunaita *trade mispricing*. Ndiyo ile wakileta *machinery* wanakuza bei baadaye wanadai *tax refund*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, wanafanya kitu kinaitwa *payment between parent companies and their*



*subsidiaries*, ndiyo maana tulikuwa tunagombana na *Acacia* lakini amekuja kuibuka Mwenyekiti wa Barrick ambayo ndiyo Kampuni Kuu. Pia wanafanya wizi huo kwa kutumia *profit shifting mechanism* ambayo imekuwa *designed* ku-hide revenue, ndiyo maana tunaita wizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, watatumia mbinu nyingi kutu-*divide*. Gazeti la *The East African* la wiki hii limeandika, "*Magufuli Fight for Mineral Revenue Splits Parliament*." Hiki siyo kitu kizuri kwetu kama Taifa. Lazima sisi tubaki kitu kama kimoja. Kama Bunge, kama Taifa, lazima tuwe nyuma ya Mheshimiwa Rais ambaye ameamua kuthubutu kukabiliana na huu wizi mkubwa wa Kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Director* wa *Global Justice* anasema kuwa Afrika siyo maskini na ukipitia ripoti mbalimbali za Taasisi za Kimataifa, zinasema kwamba kupitia makampuni haya, fedha inayoondoka ni zaidi ya mara kumi ya fedha wanayotupa sisi kama misaada. Maana yake ni nini? Ukienda kwenye bajeti yetu, karibu shilingi trilioni saba ni mikopo, misaada na fedha kutoka kwa wahisani; lakini inayoondoka kupitia wizi huu niliousema, maana yake ni mara kumi ya shilingi trilioni saba. Kwa hiyo, zinazoondoka hapa nchini kwetu ni shilingi trilioni 70, ndiyo maana tunasema wizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hizi zinazoondoka kwa mbinu hizi mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais ameamua kuwa na uthubutu ili tuweze kukabiliana na *multinational companies*, lazima sisi kama Taifa na kama Bunge tuwe *united*, tusigawanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa nini ameweza kuwa na uthubutu? Ukisoma gazeti la *Sunday Nation* la Jumapili linasema, "*Uhuru tycoons raise millions in two hours*" kwa ajili ya kampeni, lakini *we are lucky* Rais wetu ameingia pale hakuwa na *backing* ya watu wenye hela chafu, ndiyo maana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi subiri kidogo. Mheshimiwa Kubenea, tunaomba *documents* zote ulizoitaja zije Mezani sasa hivi.

Endelea Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, / *hope* utanilindia huo muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapopata kiongozi wa namna hii, lazima tuwe *united* kumuunga mkono, kwa sababu tunachozungumzia ni upotevu wa mapato ambayo yakipatikana wote tutafaidika. Wote hapa tunalia, nami nalia kuhusu kukosekana maji, umeme, huduma bora za afya, kuanzia Lumwago, Bumilanyinga, Isalavanu mpaka Itimbo na Mafinga kwa ujumla. Sasa anapotokea kiongozi mwenye uthubutu ni lazima sisi tushikamane kumuunga mkono kukabiliana na *multinational companies*. Haya madude ni hatari sana, nitawaambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hugo Chaves alipoingia madarakani tarehe 11 Aprili, 2002, alifurumua mikataba kama anavyojaribu kufanya Mheshimiwa Rais. Madude haya (*multinational companies*) yaliji-*organise* yakafanya hujuma kumwondoa madarakani lakini kwa sababu Bunge na wananchi wa Venezuela walikuwa *united*, baada ya masaa 47 alirudi Ofisini. Ndiyo maana nasisitiza ndugu zangu tuwe kitu kimoja kukabiliana na madude haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu siyo wakati wa kutafuta *personal recognition*. Kila mtu kwa nafasi yake alipaza sauti kuhusiana na hujuma na wizi huu. Wapo waliokuwa wanaharakati wakati huo kama Mheshimiwa Tundu Lissu, wapo waliokuwa Wabunge kama Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Kigwangalla ametajwa hapa, wapo akina Rugemeleza na Nshema wale wa *LEAT* wote walipaza sauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka 2008 Mawaziri wanaohusika na Sekta ya Madini walikutana kujadili katika

Afrika namna gani tutanufaika kutokana na madini. *AU Summit 2009* ilipitisha azimio ni kwa namna gani tutaendelea kunufaika na madini na kuachana na wizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 Mawaziri wa madini katika Afrika walikutana na kujadili na kuja kitu kinaitwa "*From Mission to Vision*"; na hiki ndicho Mheshimiwa Rais anachofanya. Ametoka *from mission to vision to action*. Sasa ameingia kwenye *action*. Anapoingia kwenye *action*, sisi tuna kila sababu ya kumuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka ujue wizi huu, nenda kasome kitabu hiki cha *Nicolaus Shakson; (Treasure Island), "Uncovering the Damage of Offshore Banking and Tax Havens."* Yote haya ni wizi unatumika. Vile vile kasome kitabu cha Mwandishi *the same; "Poisoned Worse; The Dirty Politics of African Oil."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kaangalie *document* inaitwa "*Stealing Africa.*" *Why is Africa so rich in resources, yet so poor?* Ni kwa sababu ya wizi wa namna hii ambao lazima tukubaliane tuwe *united* kama Taifa, tuwe pamoja kama Bunge na kwa maana hiyo, tutaweza sana kufanikiwa. Vinginevyo tukitafuta muda wa *recognition*, kila mtu *played his/her own part*. Viongozi wa dini walisema, wananchi wa kawaida walisema, wanaharakati walisema, Wabunge walisema. Kwa hiyo, ni wakati ambao tunatakiwa tukwepe sana kugawanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, wakati anaapishwa *Commissioner* wa *TRA*, Mheshimiwa Makamu wa Rais alisema, "Maafisa wako na Mameneja wa Mikoa waache kutoa kauli za kuigombanisha Serikali na wafanyabiashara, wakusanye kodi kwa kufuata sheria na taratibu na pia wawe na lugha nzuri."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa Mawakala wa *TRA*, lugha yao na *operation* namna wanafanya, ni kuigombanisha Serikali na wananchi. Naiomba *TRA*, pamoja na kutoa elimu ya mlipa kodi, ijaribu

kukaa na hawa Mawakala wao iwe inawapa hata *training* ya namna gani ya kufanya *customer care*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umeniishia naona unanikimbia; katika makinikia haya, yako mengi. Sisi kule Mufindi suala la misitu, nimeshaandika hata katika mchango wangu; *MPM* wanauziwa magogo mpaka leo nusu ya bei pasipo sababu. Hayo nayo ni makinikia. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kama ilivyoanza katika dhahabu, kuna makinikia kwenye misitu, kuna makinikia kwenye *fishing industry* kutoka bahari kuu, kuna makinikia kwenye mambo mengi, hata kwenye mchezo wetu wa soka kuna makinikia. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Esther Mahawe jiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hoja muhimu hii ya bajeti ya Serikali. Kwanza nianze kumshukuru sana Mungu kwa yote kwa afya na haya yote yanayoendelea, naamini mkono wa Mungu unaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Napongeza kwa dhati kabisa na wakati hotuba hii inasomwa, Waheshimiwa Wabunge wengi tulishangilia na yale tuliyokuwa tunayashangilia, naipongeza pia Kamati kwamba imeyazungumza. Sehemu ya tano ukisoma utaona namna Kamati imejaribu kuchambua na kuweka kielelezo namna bajeti hii ilivyoweza kukidhi mambo kadha wa kadha. Hii ni pamoja na kuiangalia hii sura ya bajeti. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme kwamba unaweza ukaangalia mafanikio ya bajeti hii na hususani bajeti iliyopita kwa kuangalia yale matokeo (*outcomes*) kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, lazima nishukuru sana kwa sababu Jimbo la kwetu ni jipya, Halmashauri ya kwetu ni mpya; hivi sasa tunaendelea kujenga Ofisi kwa kasi; fedha tunazo; tumejenga mashule; kuna maeneo ya maji, tunaendelea kupata huduma za maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi siwezi kuyasema yote, nashukuru kwamba hii hotuba ni nzuri kwa sababu ukiangalia bajeti zilizopita ukilinganisha na bajeti hii, utakubaliana nami kwamba kwa kweli hii ni hatua nzuri. Nami naipongeza Serikali iendelee na mwendo huu, tutafika mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nizungumze hili suala muhimu la madini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu tulikuwa na kiu ya kuyaona mengi na yako mengi ambayo pia yanakwenda kugusa Halmashauri zetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu kama ambavyo nilisema wakati uliopita nilipokuwa nachangia hapa, kwamba ile dhamira nzuri ya Mheshimiwa Rais ndiyo hasa itaweza kuleta msukumo huku chini ili tuweze kufika pale tunapotaka kwenda. Nina uhakika tunakwenda kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia baadhi ya *figures* za *report* hizi zilizotoka, nikawa najaribu kuona sisi kwenye Halmashauri zetu za Kahama tukiwa na Majimbo matatu ya Msalala, Kahama Mjini na Ushetu, utaona hapa *service levy* ambayo nikiitaja utajua tulikuwa tumepoteza mapato mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kwenye dhahabu peke yake kwa *report* hii, kwa kile kiwango cha chini cha upotevu wa mapato, tumepoteza *service levy* ya shilingi bilioni 324 kwenye dhahabu peke yake; lakini tukawa na shilingi bilioni 549 kwa kiwango cha juu kwenye dhahabu peke yake. Ukiangalia kwenye madini mengine 13

yaliyorodheshwa na Tume, utaona kabisa tulikuwa tumepoteza yapata kama shilingi bilioni 397 kwa upande wa madini yote na kwa kiwango cha chini; na kiwango cha juu tunakwenda kwenye shilingi bilioni 689. Nazungumza kwa upande wa hili zoezi lililofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kuangalia kwenye upande wa *service levy* tulizopoteza kwa wale waliotoa huduma kwenye migodi wakiwemo wale waliofanya *insurance*, wale waliofanya *consultation*, waliouza mafuta; naomba sasa hapa Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa sababu tulikuwa na shida ya kupata *information*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaweza kupata *financial statement* tangu migodi hii ilivyoanza itatusaidia nasi kwenye Halmashauri zetu kuona wale waliotoa huduma kwenye migodi kama tulipoteza. Tulishaanza hilo zoezi kutafuta hizo *information*. Tunajua kuna kiasi kikubwa ambacho kingeweza kusaidia Halmashauri zetu. Kuna kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uone kabisa kwamba Mheshimiwa Rais ameanza nasi huku tunaendelea kupigana. Hata alipotembelea Shinyanga wakati ule, nakumbuka ndugu yangu Mheshimiwa Kishimba, Mbunge wa Kahama Mjini alizungumza, tumwombe Mheshimiwa Rais atusaidie kwa sababu tunaona tumepoteza *service levy* nyingi. Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali mnaweza kutusaidia ili tuweze kukomboa na kupeleka maendeleo kwa watu wetu. Sura ya Kahama ilivyo, sivyo inavyotakiwa kuwa kwa fedha nyingi ambazo tunatakiwa kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumze kwa ufupi ni kuhusu hizi takwimu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, hata bajeti iliyopita nilikuwa nimeomba kwamba Ofisi ya Takwimu tuisaidie sana iwe na watu wa kutosha, iwe na vifaa vya kutosha ili tuweze kupata *data* muhimu za kutusaidia kuweza kufanya mambo mbalimbali, kwa sababu ukija kuona hapa, *data* nyingi ambazo tunazitumia kwenye *records* zetu za bajeti na

kadhalika, nyingi tunatumia ambazo ni wastani, tunatumia *average*, lakini sasa tukitumia *average* tunaacha *group* kubwa la watu nje ya hizo *data* ambazo tunazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati mwingine tunahitaji wataalam wasaidie Ofisi yako kwenda kwenye *measures* nyingine. Waangalie *measures of dispersion* ili tuweze kuona tunavyozungumza kwamba wastani wa kipato ni shilingi milioni mbili, lakini tumewaacha watu wangapi nje ya msitari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria kwamba Ofisi hii iboreshwe, itatusaidia pia kuweza kufanya *decision* nyingi, tuweze kuona pia tuna *income gap* ya namna gani? Bajeti iliyotangulia, tuliona pia hata Mikoa ambayo iliyokuwa chini ya mstari wa umaskini. Kwa hiyo, nashauri tu Mheshimiwa Waziri, hii Ofisi ni muhimu sana kuiangalia kwa jicho la kipekee itusaidie kupata *information* za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo suala la kodi kwenye *assessment*. Nataka nizungumze tu kwa sababu *Commissioner* naamini anaweza kuwa yuko hapa. Kwa miaka mingi tumechukua hii kwa kutumia *band*, tunachukua *blanket* tu kwenye maeneo fulani. Sasa nafikiri tuendeleo kufanya *analysis* ili mlipa kodi alipe *fair* kodi kulingana na kipato chake. Kwa sababu utakuja kuona kuna maeneo mengi tunatoza kodi kutokana na eneo, hatuendi kutoza kutokana na uhalisi wa mtu anavyopata kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, twende zaidi kuboresha taarifa zetu ili tutoze kwa usahihi. Kwa hiyo, utaona maeneo mengine kwa mfano, kwenye Mji tunasema labda wafanyabiashara wanaofanana kwenye Mji fulani watozwe kiasi hiki kwenye kodi ya mapato. Kwa hiyo, nafikiri twende zaidi ili tuweze kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hili kwenye zoezi la utozaji wa kodi ya majengo, tukisema tunakwenda kumtoza mtu mwenye ghorofa la Sh.50,000/=, lakini mwenye ghorofa kuna mwingine anaweza akawa ametengeneza kwa *leisure*

tu. Kwa mfano, ndugu zangu Wangoni kule nilikuwa nikienda naona wana maghorofa ambayo wameezeka kwa nyasi. Nilikuwa nakwenda Mbinga, nilishuhudia kuna watu wametengeza maghorofa hayo. Kwa hiyo, tuangalie ili tutoze kutokana na thamani. Vile vile wako watu wengine wana nyumba zao wamepangisha; tukitazama vizuri, tutaona kuna watu ambao wanaweza wakatupa kodi nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa sababu ya muda, nataka nizungumzie juu ya sura ya bajeti. Naona kabisa kwamba upande wa madeni hasa deni la Taifa, tuki-*manage* vizuri hili deni, utaona kabisa kwamba makusanyo yetu ukiwianisha na hali halisi ya matumizi, kidogo kuna uwiano mzuri. Kwa hiyo, tunakusanya shilingi trilioni 19.2 kwenye mapato ya *TRA*, kwenye *non-tax revenue* pamoja na Halmashauri, lakini matumizi yake bila kutoa madeni ambayo tunakwenda kulipa, tuko kwenye shilingi trilioni 22. Kwa hiyo, kuna *gap* kidogo la shilingi trilioni kama 2.9 hivi. Kwa hiyo, tunahitaji ku-*manage* vizuri hili deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sasa hivi tunakwenda kulipa deni lakini utaona tunakopa shilingi trilioni 11 mkopo wa ndani na nje, lakini tunakwenda kulipa shilingi trilioni tisa. Kwa hiyo, hili *gap* la deni litaendelea kuzidi. Kwa hiyo, naomba tufanye *effort* kupunguza hili deni ili siku za usoni tukope kidogo, tulipe kidogo ili tuweze kujenga uwezo mkubwa wa kupeleka fedha nyingi kwenye eneo la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuzungumzia juu ya upande huu wa nakisi ya bajeti. Nilikuwa najaribu kuangalia hapa kwamba tumepata nakisi ya bajeti ya 3.8 lakini hapa tumezingatia mapato ya mikopo nafuu kutoka nje, tumewianisha na *GDP*. Tumeacha pia hii mikopo mingine ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara ambayo ukijumlisha na mikopo ya ndani tunakuwa na shilingi trilioni 11. Sasa nikiwianisha na pato la Taifa, tunaona kwamba ule uwezo wetu wa ku-*deal* na *government spending* unakuwa uko *short* kwa asilimia 11.3.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria lazima tutazame yote kwamba tuna uwezo wa kukusanya kodi, tuna uwezo wa kukusanya mapato ya ndani mengine yale pamoja na Halmashauri zetu, lakini ule uwezo wa sisi kupata fedha kutoka nje ya makusanyo yetu tunapungukiwa asilimia 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri tulitazame kwa sababu tukitazama upande huu wa mapato ya mikopo nafuu kutoka nje pake yake ya shilingi trilionni tatu, nafikiri siyo sahihi kuweza kuona hii nakisi ya bajeti. Kwa sababu nilikuwa najaribu kuangalia nchi mbalimbali, nimeona Uholanzi wana-*shoot* kutoka 2.8 hadi 2.5, Marekani wana 3 - 3.5. Ukiona *range*, iko *within* lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mahawe, atafuatiwa na Mheshimiwa Kadutu na Mheshimiwa Massare.

**MHE. ESTHER A. MAHAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii iliyoko mbele yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba haiwezekani mtu mwenye nia ya dhati na mzalendo kwenye Bunge hili ukasimama bila kuanza kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa natazama kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, niliona jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais hakukurupuka kwenda kuzuia madini yetu kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Ilikua ni sehemu ya vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Rais alivizungumza alipokuwa hapa Bungeni akihutubia tarehe 20 Novemba, 2015 na habari ya madini ilikuwa kipaumbele chake Namba nne (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri aliyofanya. Hawa wanaosema jana amemkaribisha mwizi

Ikulu, yaani tunasema hiyo ni danganya toto, maana Mheshimiwa Rais alisema anakaribisha wahusika kwenye meza ya majadiliano, wala hakuandika *invitation letter* ya kumleta yule Mwenyekiti hapa. Watu walijipima wenyewe, wakaona jinsi gani tumetiwa hasara na Makampuni yao hayo, wakaona wabebe mzigo huo wa kuja ku-*negotiate* mambo yaliyofanyika ya kutia nchi hii hasara na Rais wetu na mambo haya yamefanyika hadharani. Kwa hiyo, hawa ndugu zetu wakikosa la kusema, ni bora wakati mwingine wakanyamaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme, watu hawa mara nyingi wanawasumbua hawa Waheshimiwa Mawaziri kwa maswali na vitu vingine vya namna hiyo na michango Bungeni humu wakihitaji Serikali kupeleka mahitaji kwenye Majimbo yao; wanahitaji elimu, maji na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa, kama siyo Mheshimiwa Rais ameamua kuchukua jukumu hili zito la kujitoa muhanga akaamua kutetea rasilimali kwa ajili ya wananchi wa nchi hii, hivi hawa watu hayo mahitaji muhimu ya watu wao watayatoa wapi? Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunaendelea kumwomba Mungu aendeleo kumpa maisha marefu, maana ana mpango wa kututoa mahali tulipo kwenda mahali pengine. Ni sawa na Musa alivyowatoa wana wa *Israel* kwenye nchi ya utumwa ya Misri na kuwapeleka Kanaani. Ndicho anachokifanya Mheshimiwa Rais kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa bajeti nzuri sana ambayo imekuja mbele yetu. Tunafahamu kwamba kazi kubwa inafanyika. Naipongeza na timu nzima ambayo iko chini ya Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza habari hii ya bajeti, naomba nianze na suala la makusanyo ya mapato. Naipongeza pia Serikali kwa sababu sasa imechukua hatua ya kuweza kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki ili kudhibiti upotevu wa fedha hasa katika Halmashauri na

maeneo mengine mbalimbali nchini. Ninachokiomba na kuishauri Serikali yangu ni kwamba, katika mgawanyo huu sasa wa ile Keki ya Taifa baada ya makusanyo haya kufanyika, basi mgawanyo wa Keki ya Taifa uweze kwenda sawia kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikizungumza hili, naomba nizunguzie suala zima la elimu. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kukubali kupeleka katika shule zetu shilingi bilioni 18 kila mwezi kwa ajili ya elimu bila malipo. Ni kweli na ni dhahiri kwamba watoto sasa wanasoma mashuleni na changamoto zilizokuwepo huko nyuma hazipo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumza hivi, karatasi niliyoibeba mkononi mwangu inaeleza orodha ya shule ambazo zitakarabatiwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa ile bajeti ya 2016/2017. Nitoe masikitiko yangu kwamba Mkoa wa Manyara shule inayokwenda kukarabatiwa ni moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetazama Mikoa mingi; Dar es salaam na Mikoa mingine, kila mtu aliiona hii karatasi. Kuna mikoa imepata bahati ya kukarabatiwa shule saba, sita, nane au nne lakini Mkoa wa Manyara tunakarabatiwa shule moja tu ya Nangwa iliyoko Wilayani Hanang. Naona kidogo hapa haijakaa sawa sawa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Ndalichako katika hili nalo atuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule kongwe, tuna shule inaitwa Endagikoti ambayo iko Wilayani Mbulu, ilianzishwa mwaka 1929, tuna shule iko Mbulu inaitwa Dawi, imeanzishwa mwaka 1917; hizi shule ni kongwe. Masikitiko mengine ni kwamba, hatuna *high schools* kwenye Mkoa wa Manyara. Tuna *high schools* chache mno, mfano Wilaya ya Simanjiro haina *high school* hata moja; Hanang haina *high school* hata moja; Wilaya ya Mbulu ina *high school* mbili. Kwa hiyo, naomba, kwa sababu kipaumbele cha kwanza cha Mtanzania ni elimu na tukimkamata huyu elimu tukaacha

kumwacha aende zake, watoto wetu watakombolewa. Naomba sana kwa hili tukumbukwe katika Mkoa wa Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza bajeti hii kwa kuwa inatambua akinamama; Mama Lishe, akinamama wanaofanya biashara zao ndogo ndogo na vijana hawa Wamachinga, hili ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu kutambua hili. Wakati haya ya kurasimisha biashara zao yanafanyika, naiomba Serikali iangalie namna gani itakusanya kodi kwenye Makampuni makubwa ambayo hayakusanyi kodi inavyotakiwa ili ikiwezekana hawa watu wapewe baada ya kutambuliwa na kupewa maeneo ya kufanyia biashara zao, waweze kupatiwa muda wa kutosha ili kwamba sasa ifikie mahali nao waweze kuchangia kodi. Siyo kwamba wanapewa maeneo na wakati huo huo basi wanaanza tena kutozwa kodi wakati wanakuwa hawajajijenga vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema bado tuna vyanzo vingi vya kodi vinavyoendelea kupotea; kuna Makampuni makubwa ambayo yanakwepa kodi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, juzi hapa alizindua *data center* kwa ajili ya *collection* ya mapato yote yanayotakiwa kukusanywa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya Makampuni makubwa kama ya simu, Makampuni ya uchimbaji ambayo yamehodhi vitalu vikubwa kwa ajili ya uchimbaji lakini hawachimbi, vitalu hivyo vimekaa tu. Naomba Serikali ifanye tathmini ya kutosha waone kwamba Serikali inakwenda kufaidika na nini. Najua Mheshimiwa Rais ameshaanza hili na nina hakika tunakwenda kufanikiwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusisahau pia kwamba tatizo kubwa la maji bado lipo pale pale. Hatukuona ile Sh.50/= ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameipigia kelele

humu ndani ya kuongezwa kwenye mafuta ili kwamba tuweze kumtua mama wa Kitanzania ndoo kichwani. Bado naendelea kuillia na kuiomba Serikali yangu itazame hili kwa jicho la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wengi ambao ni wazalishaji na wachangiaji wa uchumi wa mapato ya nchi hii, wanapoteza muda mwingi kwenye kutafuta maji. Tunaomba ile Sh.50/= iongezwe kwenye mafuta ili kwamba tuweze kumtua mama ndoo kichwani. Wakati huo huo, Mkoa wa Manyara ni Mkoa wa wafugaji; tuna Kata kama za Ndedo kule Kiteto; kata nyingi tu za pale Kiteto, Simanjiro, Kata za Dongo, Kijungu, Lolera, Olboloti; Kata hizi hazina maji kabisa ya bomba wala mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ikiwezekana watu hawa wapate kuchimbiwa mabwawa. Juzi tulikuwa na mafuriko ya kutosha hapa nchini. Naiomba Serikali yangu kupitia hizi Halmashauri zetu, wahakikishe hawa watu wanachimbiwa mabwawa wakati ambapo mvua imesimama kama hivi, ili nyakati za mvua tuweze ku-track yale maji yaende kwenye hayo mabwawa kupunguza hii changamoto ya maji. Mbona ni rahisi! Kwa hiyo, naomba hasa maeneo ya Kiteto na Simanjiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wilaya ya Hanang' tunahitaji mabwawa pia, maana nako katika zile Kata tuna wafugaji wengi tu. Tukiweza kuwawekea wafugaji hawa maji kupitia mabwawa, wataacha kuhamahama, watakaa kwenye maeneo yao, maana rasilimali za kutosha zitakuwepo pale, maji pamoja na mambo mengine wanayoyahitaji. Naomba sana Mkoa wa Manyara ukumbukwe katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna matatizo ya mawasiliano baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Kiteto, tuna shida katika Kata za Ndedo pamoja na Makame. Bado watu hawa wanaishi ile karne ya kupanda juu ya miti ili uweze kuzungumza na ndugu yako aliyeko upande mwingine. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri husika ama Mheshimiwa Waziri

katika bajeti hii aikumbuke Wilaya ya Kiteto na maeneo mengine mengi tu ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumze pia masuala mazima ya mazingira ya ulipaji kodi. Naishauri sana *TRA*; naishauri Wizara ya Fedha waweze...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Kadutu atafuatiwa na Mheshimiwa Massare.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja muhimu kwa maisha ya Serikali yetu pamoja na wananchi wetu, wakati huu tunapohangaika na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na timu ya uongozi wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko tofauti ya bajeti ya mwaka unaokwisha na hii iliyoletwa mwaka 2016 na mwaka huu wa 2017 kuna tofauti kubwa, kuna maboresho, lakini bado yapo mambo ambayo tunapaswa kuyatilia mkazo ili maisha ya wananchi wetu yaende vizuri na yawe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo huduma tunazozingumzia hasa barabara. Toka mwaka 2016 tumekuwa tunazungumzia barabara inayotoka Mpanda kupitia Kaliua, Uliyankulu hadi Kahama. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu itakuwa inaunganisha mikoa karibu mitatu au minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama azma ya Serikali yetu kuunganisha mkoa kwa lami, basi baada ya kipande cha Chaya na Nyahuwa kupata pesa, basi naomba Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi mwelekeze sasa nguvu zote kwenye barabara hii inayotoka Mpanda kupitia Uliyankulu mpaka Kahama. Ni kilomita 428 na nina imani wakipatiwa Wakandarasi kama watatu, kazi inaweza kwenda vizuri, badala ya kila mwaka kuizungumza kwenye Ilani lakini utekelezaji wake hakuna. Tunataka pia tupate *performance* ya utekelezaji wa mradi huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo tunalizingumza hapa, lakini Serikali bado inakuwa ipo kimya. Suala la Mfuko wa Maji; tumezungumza sana lakini Serikali ije basi na kauli, tunakubaliana au hatukubaliani? Maana unapozungumza halafu mwenzako kakaa kimya, maana yake labda unachozungumza ni msamiati wa Kichina au Kijapani, maneno ambayo ni michoro michoro ambayo huwezi kuelewa. Serikali ije hapa na majibu: Je, tumekubaliana juu ya mfuko wa maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, tatizo la maji vijijini ni kubwa kuliko tunavyodhani. Mpo wengine hapa ndani mkienda vijijini kwenu mnabeba maboksi ya maji. Hakuna mtu anayekwenda kunywa maji ya kijijini. Yawezekana mkaona hakuna haja kwa sababu huku ndani mjini mnaoga vizuri, mnakunywa vizuri, maji ya kupikia mazuri, hakuna anayejali. Kwa nini Serikali isije na majibu basi! Toka mwaka 2016 tunazungumzia Mfuko wa Maji, lakini tunaona kama vile mmeziba masikio. Njoooni na ufumbuzi wa tatizo la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wiki nzima nilikuwa Jimboni, kila eneo ukienda ni shida ya maji, lakini humu Bungeni kila mmoja akiulizwa swali la maji, maswali ya nyongeza Bunge zima linasimama, hata wewe Mwenyekiti unapata tabu sasa nani aulize na nani aache kuuliza? Hiyo ni kuonesha ni jinsi gani ambavyo swala la maji lina umuhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukamilishaji wa mradi wa umeme; tunakwenda tumeshaanzisha REA III. Naiomba sana Serikali, sasa tusiichie njiani, maana yake shida ni kwamba watu wote tunaelekea kenye madini; wote mazungumzo yamekuwa ni madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukamilisha REA III liende kweli likatatue matatizo yaishe. Siyo tena tuje tuambiwe kuna REA IV na V. Itafika wakati hata pesa hatutapeleka kwenye umeme, kwa sababu umeme utaonekana siyo tena jambo la umuhimu. Kwa hiyo, nashauri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala lingine juu ya suala la ujenzi wa Zahanati pamoja Vituo vya Afya. Jambo hili kama tunawaachia wananchi zaidi, hatuwezi kulikamilisha. Lazima Serikali ielekeze nguvu huko. Sasa tulisema kila Kata ijenge Kituo cha Afya; mabadiliko yamekuja, kila Kata mbili zijenge Kituo cha Afya; tunaanzisha tena migogoro kituo hicho kijengwe wapi? Kila Kata inapiga chepuo kujenga eneo lake. Kwa hiyo, nadhani Serikali kwa makusudi kabisa tuelekeze nguvu huko kwenye ujenzi wa Vituo vya Afya pamoja na *Dispensary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningumzie hili suala la madini, migodi na kodi; mimi kabla ya kuingia hapa Bungeni, nimekuwa mfanyakazi huko kwenye migodi. Mwaka 2008 wakati *issue* ya Buzwagi inaletwa hapa, mimi nilikuwa mgodini. Sisi wafanyakazi wa kule tumekuwa tukipaza sauti sana juu ya matatizo haya ya uibiwaji wa mali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazona ndege, tunasema, lakini watu walikuwa hawasikii. Tumezungumza sana juu ya mambo haya! Kule mgodini pia kuna mambo ya unyanyasaji, kuna ubaguzi mkubwa na hasa raia hawa wa Kizungu wanaotoka *South Africa*, wananyanyasa. Sasa wakati wafanyakazi mgodini wanaponyanyaswa, wanapaza sauti juu ya wizi wa mali hii, lakini hakuna aliyesikia. Leo hata tukisema, hao wanaokuja kufanya kazi mgodini, hawana elimu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kule nimeshuhudia watu wana vyeti vya semina ya siku tatu; na wenzetu wapo makini sana. Ukipiga semina hata ya siku moja, unapata cheti. Ukipiga semina ya siku mbili, unapata cheti; ndizo CV walizonazo. Ukienda Idara ya kazi, vibali vinatoka kila siku watu wafanye kazi, ambapo masharti yanataka mtu mwenye elimu zaidi, lakini awe na mpango wa kufundisha wazawa. Hakuna anayejali. Watu wapo migodini wanakamatwa na bangi, wanafikishwa Mahakamani, lakini kesho yake mtu huyo huyo anaomba kibali anaruhusiwa kufanya kazi ndani ya ardhi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie ukwepaji kodi. Wote hapa akili sasa ipo kwenye Barrick na Acacia, lakini migodini, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikie vizuri, zipo Kampuni nyingi zaidi kuliko kampuni tunayoizungumza, lakini hawa watu wanaiba, wanakwepa kodi kwa njia mbalimbali. Pesa zao wao wanalipana juu kwa juu, hakuna malipo ya moja kwa moja. Maana yake hata kodi haijulikani ni kiasi gani. Hata mifuko ya jamii hii hawachangii, kwa sababu wao wanarekodi mishahara midogo kuliko mishahara wanayolipwa kule nje. Mimi ni shahidi na niko tayari kueleza jinsi kodi inavyoibiwa kwa sababu nimekuwepo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajaribu kuangalia sana, tusijikite kwenye Kampuni moja tu kubwa, wakati mle mgodini kuna kampuni nyingi zinafanya shughuli hiyo. Kwa hiyo, nashauri, kuchunguza kwa makini zaidi wizi au ukwepaji wa kodi wa kampuni zile ndogo ndogo ambazo zimepewa kazi na makampuni ya migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la shilingi milioni 50. Imekuwa ni msumari huu, kila ukizunguka kwenye majimbo swali kubwa ni shilingi milioni 50, hatuna majibu! Serikali ije na majibu hapa. Siyo dhambi kusema kwamba tumeahirisha au tutafanya mara nyingine. Tuondokane na jambo hili au liletwe katika mpango mwingine kuliko kung'anga'na tutatoa shilingi milioni 50; huu ni mwaka wa pili sasa hatujatekeleza. Hatujafanya hata majaribio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla hata kengele haijanililia kama kawaida yangu, fedha za maendeleo zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu, hata mwaka 2016 nilisema, lazima tuhakikishe fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri ziende kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massare na Mheshimiwa Mipata ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kwa muhtasari tu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada kubwa na za dhati na za makusudi katika kuhakikisha nchi hii inafikia malengo yake ya kujitegemea kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuomeona hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ilivyoainisha na kuonesha makusudio mazima na dhamira nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutaka kufanya nchi hii wananchi wake waendeleo kukiadini Chama kinachotawala sasa, Chama cha Mapinduzi kwa maana ya CCM. Ndiyo chama ambacho huwezi kuacha kuihusisha nchi hii na chama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara ya Fedha kwa

kuona na kutambua wananchi wanyonge ambao walikuwa wananyanyasika kwa kusumbuliwa sana na hususan katika kodi mbalimbali hizi ndogo ndogo, ikiwemo ya kusafirisha mazao kidogo chini ya tani moja, kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine, lakini kutambua sekta isiyo rasmi ya akinamama Lishe na wajasiriamali wadogo wadogo ili nao wawe na mchango katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuishauri Serikali kidogo hasa katika kuhakikisha nchi inajitegemea katika suala zima la chakula. Ni vizuri sasa tukaanza kufikiria na kuondokana na utegemezi huu wa kilimo kinachotegemea mvua. Nchi hii tumekuwa tunategemea sana kilimo kinachotegemea mvua. Skimu za Umwagiliaji ziko kidogo sana na ziko maeneo ambayo yana uasilia wa mito labda na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa tukatengeneza miundombinu ya makusudi, yakiwemo mabwawa madogo madogo kwa maana ya malambo, kuhakikisha wananchi sasa wanalima kilimo cha umwagiliaji kutokana na hali ya hewa ambayo inabadilika badilika. Kumekuwa na changamoto ya tabia ya nchi, wananchi wetu na maeneo yetu mengi, ikiwemo mwaka huu maeneo mengi ya hali ya chakula siyo nzuri sana, ikiwemo Mikoa ya Kati, hata Mikoa ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya juhudi za makusudi za Serikali kuwekeza katika kilimo hiki cha umwagiliaji. Ni vizuri sasa na sisi tutoke tukajifunze kwa baadhi ya nchi zilizofanikiwa nchi ambazo zilikuwa maskini wenzetu lakini sasa wametoka kabisa huku ambako tupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusaidia wakulima ambao ndio wengi katika nchi hii, lazima tuhakikishe mbolea yetu inawekewa ruzuku. Kulikuwa na mpango hapa wa Waziri wa Kilimo aliyekuwa ametoka kwenye nafasi yake sasa amepewa Wizara nyingine ya kulinda watu wetu na mali zao; ni kwamba kulikuwa na mpango wa kuhakikisha

mbolea yote ambayo inaingia katika soko inawekewa ruzuku. Hii itaondoa kufuatana; kazi kubwa itakuwa ya kudhibiti kwamba hii mbolea sasa badala ya kutumika ndani isitoke tu nje ya mipaka yetu, iuzwe kama bidhaa nyingine ambazo mkulima anaweza kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na ruzuku ya mbegu iwe wazi iingie masokoni ili mkulima akienda kwenye duka, mbegu iwe tayari ina ruzuku. Kama Serikali haitathubutu bado wakulima wa nchi hii wataendelea kusumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi hii tuna tatizo la maji. Naomba Serikali ifanye juhudi za makusudi mazima kuhakikisha upatikanaji wa maji vijijini. Tumediriki sana katika miji yetu mingi, tumeona juhudi kubwa za Serikali kupitia Wizara ya Maji kuhakikisha miji inapata maji, lakini vijiji vingi vina tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sasa Serikali ifike mahali ione na ichukue mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. Wameongeza Sh.40/= katika kuhakikisha tunaziba mapengo ambayo yatatokana na misamaha ambayo wametoa. Naomba basi iongezeke hata Sh.10/= tu ambayo itasaidia kuongeza katika Mfuko wa Maji ili miaka hii iliyobaki tuweze kutekeleza vizuri ilani ya chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina dhamira njema ya kuunganisha Mkoa yote kwa lami, ukiwemo Mkoa wa Singida ambao natoka mimi. Tuna nia ya kuunganisha Mkoa wa Singida na Mbeya, kunabaki kilomita 413. Kilomita hizi ni nyingi. Naishukuru Serikali kwa kuanza kutaka kujenga sasa kilomita 56.9 kutoka Mkiwa, Itigi hadi Noranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hii ya Ujenzi, kwamba ukijenga kilomita 57 hizi takriban, bado utakuwa umebakiza kilomita 300 na zaidi. Ikiwezekana, ni vizuri basi *speed* ikaongezeka, lakini Waziri wa Fedha aone, awasaidie. Ule Mradi Mkandarasi hadi sasa hajafika, hatumjui mpaka sasa

hivi, lakini tunaambiwa tunajengewa kilomita 56.9 takriban kilomita 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Simiyu kupitia daraja la Simbiti ni jambo ambalo tunataka tuone sasa wananchi wa Mikoa hii wanasafiri lakini wanapita katika barabara kama wenzao wanaotoka maeneo mengine. Napongeza kwa sasa kumalizia kipande cha barabara ya kutoka pale Chaya mpakani kwenye Mkoa wa Tabora maeneo ya Nyahuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeze Serikali pia kwa kusimamia kutaka kujenga reli hii ya Kati, kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, lakini dhamira ni kufika Makutupora katika Mkoa wetu wa Singida. Vile vile kuna reli hii ya Kati ambayo ni kutoka Dar es Salaam, Kigoma na Mwanza, ina tawi lililoanzishwa na Mheshimiwa Mwalimu Nyerere Rais wa Awamu ya Kwanza, Baba wa Taifa hili kutoka Manyoni kwenda Singida, haizungumzwi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ilikuwa na msaada mkubwa katika uchumi wa nchi hii. Sisi ni wakulima na kulikuwa na mashamba ya *NAFCO*. Kule Basutu yalikuwa yakipita pale inarahisisha kufika kwa walaji wengi ambao ni miji mikubwa lakini kwenye viwanda kule Dar es Salaam. Ni vizuri sasa mkaanza kufikiria reli hii ya Manyoni – Singida nayo iwe katika kiwango kizuri; lakini wameanza kung’oa hadi mataruma. Sasa sijui uwekezaji ule nchi inaenda namna gani? Naiomba Serikali ijangalie kipande hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo kuhusu suala zima la hifadhi ya chakula. *NFRA* wametengewa hela mwaka huu, lakini hapa nyuma tumeshuhudia maeneo mengi yanapata upungufu wa chakula lakini msaada na namna ya kuwahami wananchi wetu unachelewa sana. Leo hii tumeanza kutoa eti chakula cha bei nafuu wakati tayari watu wameshavuna. Naiomba Serikali kwa makusudi mazima, panapokuwa na upungufu wa chakula, basi

zichukuliwe hatua za makusudi kusaidia watu wetu waweze kulima na kurudi tena mwaka mwingine usiwe na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapokutana na hali ya uhaba wa chakula, hawezi hata kufanya kazi zake za kila siku. Kwa hiyo, tunatengeneza mazingira ya janga kubwa zaidi kama hatutaweza kutumia akiba ya chakula ya Taifa kuwanusuru wananchi wanaokutana na tatizo hili. Hii imetokea sana miaka hii miwili ambapo nami nimeona nikiwa Mbunge kwamba hazichukuliwi hatua za haraka, wanaposaidia wananchi, wanapewa chakula kile wakati tayari wameshaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka niseme kuhusu ujenzi wa Zahanati kila kijiji na ujenzi wa Kituo cha Afya kila Kata; ni ahadi yetu ya uchaguzi. Sasa sijui tukirudi tutakuja kusema nini? Naomba sasa juhudi za makusudi angalau tufikie nusu ya yale ambayo tuliahidi.

*(Hapa kengele ilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame, ajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia uzima, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuja na hotuba nzuri sana. Hotuba hii ni nzuri sana, tofauti na wenzangu wanaosema ina matatizo. Mimi niko hapa Bungeni kwa muda wa kutosha, miaka sita, nasema hotuba hii ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanyia Tanzania. Rais huyu ni wa pekee! Waswahili wanasema, "Kila zama na kitabu chake." Kitabu cha Mheshimiwa Rais Magufuli kitaandikwa kwa wino wa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji huu ni *message* kwa wanasiasa wengine wanaotafuta nafasi kama ya kwake. Una kiatu cha kujaa hapo? Una mguu? Kiatu chako kinatosha? Mguu wako unatosha hicho kiatu? Ni *message* kwa Watendaji Serikalini, huyu Rais anataka Watendaji wa namna gani kwenye Serikali yake? Ni *message* kwa wananchi wote. Tumuunge mkono kwa sababu dhamira yake ameiweka wazi, ni ya kizalendo kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ni *message* kwa nchi nyingine kwamba Tanzania kuna viongozi wana macho na wanajua kulinda nchi yao. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye bajeti. Bajeti hii ni nzuri, imekonga mioyo ya Watanzania wengi. Imefuta ada ya *motor vehicle licence*, imepunguza ushuru wa mazao ya biashara kwa wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wadogo wadogo ambao mara nyingi wako kwenye wigo wa gunia 10 hizo hizo. Imemfanya mkulima sasa ajsikie kwamba kile anacholima kina thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia tuone kwenye ushuru kama dagaa na samaki na zenyewe tunaziachaje? Isiwe kimya namna hii, ili kama ni ushuru, basi tuwapunguzie wale wafanyabiashara wa samaki na dagaa katika kiwango kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inaenda kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais alizoziweka. Tena aliweka ahadi ya kwanza kabisa kwamba anataka nchi yetu iende kwenye uchumi wa kati. Bajeti hii imeweka mipango mizuri kabisa ya kuboresha ujenzi wa barabara zetu, ujenzi wa reli katika *standard gauge*, ujenzi wa mifumo ya usafiri wa anga, majini

lakini vile vile mfumo wa uendelezaji umeme ambao ni muhimu sana katika uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kushauri ni kwamba utendaji lazima uwe makini; tutumie fursa tulizonazo hasa za kijiografia kuhakikisha kwamba haya mazingira tunayoyaweka tunafanya uzalishaji mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mkoa wetu wa Rukwa ni wa kilimo. Leo hii hali ya hewa ni nzuri sana Mkoa wa Rukwa, lakini bado kilimo siyo kizuri sana vile tunavyotaka. Bado hatujaingia kwenye kilimo cha kutumia matrekta, kilimo cha kibiashara ambacho kinaweza kikatukombo na lazima watumishi waangalie, Mawaziri mjue kwamba kilimo kinabeba watu wengi; kinaajiri watu wengi. Ukiimarisha kilimo, kwa vyovyote vile unakuwa na wigo mpana wa kubadilisha uchumi wa nchi na kusaidia watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba bajeti hii ambayo naiunga sana mkono inisaidie mambo yafuatayo katika Jimbo langu. Vipo vijiji ambavyo vilisahaulika kupelekewa umeme na sikuviona kwenye orodha na niliweza kupata nafasi ya kumwona Mheshimiwa Waziri lakini na Mtendaji Mkuu wa REA. Vijiji hivi ni vijiji vya Katani, Malongwe, Nkana, Sintali, Ifundwa, Nkomachindo na Nchenje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umeme pia uende Kata ya Ninde iliyo na vijiji saba; Kata ya Kala ina vijiji saba, Kata ya Wampembe ambayo Waziri alitembelea mwenyewe ina vijiji vitano na hawa ni wavuvi wamekuwa wakivua samaki zao wanapeleka Zambia. Akiwapelekea umeme hawa amewakomboa na bajeti hii ni ya ukombozi. Kwa hiyo, naomba umeme ufike katika Kata hizi za mwambao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia bajeti ninayoiunga mkono sana iniunge mkono katika juhudi ya maji katika Jimbo langu la Nkasi Kusini. Tuna tatizo la maji katika Kata ya Nkhandasi ambayo ina Vijiji vya Kasu, Milundikwa, Malongwe, Katani na Kisula. Vijiji hivi vimekuwa na shida ya maji muda mrefu sana na juzi tumehamisha Shule ya



Milundikwa tukapeleka kwenye Kata hii hapa. Kwa hiyo, naomba...

## TAARIFA

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba miongoni mwa vijiji ambavyo vina kero kubwa ya maji katika Jimbo lake ni pamoja na Chonga, Katani, Talatila pamoja na Miyula. Kwa hiyo, nataka tu nimpe hiyo taarifa mchangiaji anayeongea.

**MWENYEKITI:** Mchangiaji, taarifa!

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naikubali sana taarifa yake na nilikuwa naendelea huko. Kwa hiyo, Vijiji vya Chonga, Makupa, Talatila na Miyula vina shida kubwa ya maji na ina mitambo na mtandao wa maji unafika pale. Kwa hiyo, ni suala la kufufua na kuanzisha. Namshukuru sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ipo miradi ya maji katika Vijiji vya Nkundi na Kalundi. Vijiji hivi vina bwawa la Kawa ambalo tumekuwa tukilizungumza muda mrefu. Hatua zake ni nzuri, naomba Serikali ikamilishe ili wananchi waweze kupata matunda ya jasho la Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mwingine ni mradi wa maji wa Zuma, Isale ambao utahudumia vijiji vya Ntemba, Kitosi na Ntuhuchi. Mradi huu uko katika hatua za mwanzo. Naomba Watendaji waharakishe ili pesa ambazo tulitengewa kwenye bajeti ya mwaka 2016 zisirudi kwa sababu zipo za kutekeleza mradi huu. Kwa taarifa nilizozipata sasa hivi, karibu utekelezaji uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, bajeti hii inisaidie kutenga pesa kwa ajili ya Vituo vya Afya. Kipo Kituo cha Afya cha Kandasi, wananchi wameamua kujenga wenyewe, tunachohitaji hapa ni nguvu za Serikali, mtusaide. Kipo Kituo cha Afya cha King'ombe, Kata ya Kala. Kata ya Kala iko na umbali wa zaidi ya kilometa 150 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Akinamama na Watoto wamepoteza maisha yao kwa sababu ya umbali wa barabara isiyofikika. Bajeti hii ninayoiunga mkono leo ikawe mkombozi kwa vifo vya akinamama na watoto kutoka Kata ya Kala na Kituo cha Afya cha King'ombe kiweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Kituo cha Afya kijengwe Kate na Ninde na wananchi tumewahimiza na wako na utayari wa kutosha katika kuanza kujenga majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ninayoiunga mkono, naomba ikawe mkombozi wa kuleta uchumi kwa wafanyabiashara wadogo waliotambuliwa leo, wasinyanyaswe tena ili pamoja na kutambuliwa kwao, basi Serikali ione namna ambavyo inaweza ikatumia vyombo vya fedha kuwasaidia watu hawa kwa kutoa mikopo midogo midogo ili waweze kupata mitaji na kuchangia katika uchumi wa Taifa pamoja na uchumi wa familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini ni miongoni mwa Jimbo ambalo liko kwenye maeneo ambayo yana changamoto nyingi. Zipo barabara za Kitosi - Wampembe; barabara ya Kana - Kala; na barabara ya Namanyere - Ninde. Barabara hizi zimekuwa na changamoto kubwa sana, ukiziachia Halmashauri peke yake haiwezi kumudu kuwasaidia wananchi. Nomba bajeti hii ninayoiunga mkono sana, mtutengee pesa pia ya kuweza kuhakikisha kwamba barabara zetu zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii naomba itusaidie pia kuhakikisha kwamba mazao ambayo tumelima sisi watu wa Rukwa yanapata ununuzi kwa bei nzuri kidogo. Sasa hivi bei siyo nzuri sana, lakini gharama ya uzalishaji imekuwa

kubwa. Mkipandisha bei mnatusaidia zaidi katika kuweka bei elekezi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Makame.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusiana na hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka niweke sawa *record* au *Hansard* kwamba wakati jana Mheshimiwa Ali Salim akichangia, alipewa taarifa na Mbunge mmoja kwamba kwenye Taifa hili haikumbukwi Tanganyika. Hili ni jambo la upotoshaji na tunajua kwamba Muungano wetu huu ni wa Watanganyika na Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tanganyika ipo. Hapa pia tukiwa Bungeni tunasema kuna mambo ambayo siyo ya Muungano. Hayo siyo mambo ya sehemu nyingine, ni mambo ya Tanganyika na hakuna jambo ambalo ni la Tanzania Bara. Hakuna Taifa lililozaliwa Tanzania Bara na hakuna uhuru tunaousherehekea ukawa wa Tanzania Bara, ni uhuru wa Tanganyika. Kwa hiyo, naomba tuweke *record* sawa katika hili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nilitaka niliseme leo hii ni hili suala la mchanga. Suala la mchanga kidogo limettoa kwenye ajenda kuu ya bajeti kwa Bunge zima. Sizungumzii Wapinzani wala sizungumzii watawala; nasema kwamba limettoa na pengine ni mkakati maalum, uliotengenezwa utoe katika ajenda ya msingi ya bajeti. Watu wengi kwa asilimia 70 bajeti hii, wanazungumzia makinikia ya mchanga, hawazungumzii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwenye kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini na nasema tena. Katika jambo ambalo linahitaji mshikamano na umoja wa Kitaifa ni hili, lakini mshikamano huo hauwezi kupatikana kwa maneno tu, tunahitaji kubadilisha sheria zetu na ikibidi twende juu zaidi kwenye Katiba yetu ya nchi kufanyia yale mapendekezo yaliyoletwa na Tume ya Jaji Warioba, yaletwe tena basi tuyapitie na tupitise Katiba mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili mnadhani kana kwamba linaongelewa kijuujuu. Kama neno alilolitumia Mheshimiwa Bilago, kama kuna watu wanaoenda na maandamano ya mioyo ni Wazanzibari. Suala la Muungano siyo suala la mchezo mchezo la kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia mikataba ya madini na tunazungumzia tume zilizoundwa. Leo tumempongeza Mheshimiwa Rais lakini tume zilizoundwa kuangalia masuala ya madini ni nyingi na *findings* zake zilisomwa, lakini utekelezaji wake haukufanyika. Leo Mheshimiwa Rais kaja, kazungumza aliyoyazungumza, kawa na ujasiri kafanya alichokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mungu katika Taifa hili kwamba aje Mheshimiwa Rais azione tume zilizopitia masuala ya Muungano au jambo hili la Muungano na mapendekezo yao, aje aseme kwamba sasa ipo haja ya kuunda Serikali tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jambo hili lipo na tume zote zaidi ya nane zilizoundwa kwenye nchi hii toka kipindi cha Mwalimu Nyerere mpaka leo zote zimependekeza Serikali tatu. Leo tukizungumzia suala la Muungano humu ndani ni kana kwamba unazungumzia kitu cha ajabu. Wapo waliozungumzia madini tunayoibiwa mkawaona wa ajabu; leo ndiyo mnaona hili jambo ni jema zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala wa sheria, haki na demokrasia; hatuwezi kuendesha bajeti zetu hizi kama hakuna haki, hakuna demokrasia ya kweli katika nchi

yetu. Hili jambo mnaweza mkaliona nila mchezo mchezo sana. Leo *Babu Ally* anaendesha Serikali Zanzibar, lakini amewakosesha Watanzania walio wengi ....**(Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)**

**MBUNGE FULANI:** Babu Ally gani?

**MBUNGE FULANI:** Shein.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekosa maji, wamekosa umeme, wamekosa na huduma nyingine muhimu kutoka misaada ya nje .....*(Kicheko)*

#### TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!  
*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mzungumzaji ambaye anazunguza, Zanzibar hakuna mtu anaitwa Babu Ali na Zanzibar kuna Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye anaitwa Dkt. Ali Mohamed Shein, ni Rais halali na yuko Kikatiba halali na amechaguliwa kihalali. Kwa hiyo, nimpe taarifa ndugu yangu aweke maneno yake sawa, afahamu kama Zanzibar kuna Rais makini ambaye amechaguliwa kihalali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf, hebu kaa kwanza.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kaa kwanza!

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri humu ndani kuna watu ni viongozi. Ninyi ni viongozi, wote sisi ni viongozi. Tuna viapo ndani ya Bunge ambavyo tumekula. Majina ya kuitana

mitaani siyo humu ndani. Sasa nakuomba futa jina hilo la Babu Ally na utam-*address* Rais wa Zanzibar kwa jina lake sahihi.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya Kiti chako mimi sina shida ya kufuta. Nimefuta hilo neno...

**MWENYEKITI:** Siyo shida, nakupa amri ufute. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Safi.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta hayo maneno. Nasema kwamba utawala wa sheria ambao unafuata haki na demokrasia, sawa sawa! Hapa tunachokizungumza hasa ni uchaguzi ule wa Zanzibar; na hapa mimi sizungumzii nini kinachoendelea Zanzibar, nazungumzia *impact* ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutokana na uchaguzi wa Zanzibar kwa kulazimisha viongozi ambao hawakuchaguliwa na wananchi kukaa katika madaraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa hivi ni karibu milioni 50. Sisi Wazanzibari hatufaidiki na *REA*, lakini wanaoathirika ni Majimbo yenu hayo mnayopigia kelele. Kwa hiyo, ili utekelezaji wa bajeti uende vizuri, ni lazima Serikali ikubali utawala wa sheria, haki na demokrasia katika nchi yetu kwa sababu tumekubali mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mfuko wa UKIMWI; ninachotaka kuzungumza hapa kuna Watanzania wenzetu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wengi sana. *Donors* wamejitoa au wengi wamejitoa kutoa misaada katika masuala haya ya UKIMWI. Pengine huko tunakoenda hali itakuwa mbaya zaidi. Sasa ninachotaka kushauri kwa Serikali hii, tuwa-*serve* Watanzania wenzetu kwa pesa zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza *percent* ya kuingia kwenye *REA*, basi tutengeneze *percent* ya kuingia

kwenye mfuko wa UKIMWI kwa ajili ya kuwa-serve Watanzania wenzetu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Mfano, tumeweka tozo ya Sh.40/= kwa kila lita ya mafuta, tunaweza aidha, kupandisha ikawa Sh.42/= ama kwa hiyo hiyo iliyowekwa tukaweka Sh.2/= kwa kila lita ikaingia kwenye Mfuko wa UKIMWI ili waweze kujiendesha wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Zimbabwe tumeambiwa hawategemei misaada kwenye suala hili. Kwenye suala la UKIMWI Wazimbabwe pamoja na kasoro zao walizonazo, suala la UKIMWI wanategemea fedha zao za ndani. Kwa hiyo, nasi tujitathmini katika hili, linapoteza nguvu kazi kubwa ya Taifa. Kwa hiyo, tuweke tozo japo ya Sh.2/= kwenye lita ya mafuta ama kwenye bia. Kwenye bia tumeongeza Sh.765/= kutoka Sh.729/=. Sasa hapa kwenye Sh.765/= tunaweza tukatoa Sh.5/= tukaingiza moja kwa moja kwenye Mfuko wa UKIMWI kwa ajili ya kwenda ku-serve Watanzania wenzetu. Hii itaenda na yale malengo ya kwamba 2030 UKIMWI uwe haupo tena Tanzania au katika dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ajira kwa vijana, bajeti hii haikuzungumza kabisa suala la ajira na Serikali hii haijazungumza kabisa toka iingie madarakani suala la ajira. Wanafunzi wanaomaliza vyuo ni *numbers...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Pascal Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia naomba nimshauri Mheshimiwa Rais kwamba afanye uteuzi wa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na hii nafasi ya Mheshimiwa Dkt. Possi, kwa sababu nimeona kuna baadhi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanashindana kutafuta nafasi hizo kwa kushambulia upande huu. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba afanye uteuzi huo haraka... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wewe changia Bajeti, acha haya mambo! (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Wewe Haonga (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo, naomba niendeleo sasa kuchangia bajeti ambayo iko mbele yetu. Naomba niseme tu kwamba katika bajeti hii, yako baadhi ya mambo ambayo nimeyaona kwa kweli hayatawasaidia Watanzania, naona tunaenda kuwaongezea Watanzania mzigo wa umaskini. Kwa mfano, liko jambo hili la ada ya leseni ya magari. Ada ya leseni ya magari kwenda kuihamisha kupeleka kwa wale watu wanaotumia mafuta ya taa, kupeleka kwa wanaotumia *petrol* na *diesel*, hapa hatujatatua tatizo tumeruka majivu na kukanyaga moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba Watanzania walio wengi wanaoishi mijini na vijijini, wanatumia mafuta ya taa na ndio wengi hao maskini. Leo tumeamua kuwatwisha magunia ya mawe kwa kuwaongezea bei kwenye nishati hii ya mafuta ya taa. Umeme mmewanyima, hali ni mbaya kweli kweli! Hali ni ngumu huko vijijini, lakini leo unaenda kumpandishia Sh.40/= kwenye mafuta ya taa. Hii siyo sahihi hata kidogo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii alipokuwa anaingia madarakani Mheshimiwa Rais alisema kwamba yeye anawaonea huruma maskini. Alizungumza akasema yeye ni rafiki wa maskini. Sasa urafiki na maskini, huyu unayemtisha mzigo huu wa kumwongezea Sh.40/= kwenye mafuta ya taa, ni masikini wa namna gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Tafsiri ni kwamba leo Tanzania wanaotumia magari hata asilimia 20 hawafiki. Unachukua asilimia 20 ya Watanzania wanaotumia magari unaenda kuwatwisha mzigo Watanzania zaidi ya asilimia 80 ambao hawana magari eti walipie hii *motor vehicle*. Hii siyo sahihi hata kidogo.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niwaambie Watanzania, najua tu japokuwa hawanisikilizi, lakini najua tu watasikia hata kwa njia nyingine, kwamba ile Serikali ya Awamu ya Tano waliyotegemea kwamba ingeweza kuwasaidia sasa imeshawasaliti haina msaada tena kwao na hapo waangalie mbadala mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni jambo la ushuru wa Sh.10,000/= kwa nyumba ambazo hazifanyiwa uthamini. Yaani leo Watanzania walio wengi wanaoishi kwenye nyumba ambazo siyo bora, ukienda Mkoa huu wa Dodoma, ukienda huko Mtera kwa Mheshimiwa Lusinde, ukienda huko Chemba na maeneo mengine; na mikoa mingine; nimetoa mfano Dodoma tu, lakini yako na maeneo mengine pia, utakuta nyumba ni ya nyasi, juu wameweka udongo, wamejengea miti, leo huyu mwananchi eti unamwambia eti akatoe Sh.10,000/=, kwa kweli naomba tafadhali atakapokuwa anahitimisha, Mheshimiwa Waziri naomba mwombe Watanzania msamaha kwamba tulikosea, tuliteleza kidogo tulikuwa hatumaanishi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaposema walipe Sh.10,000/= kwa kila nyumba, ni kuwatwisha mzigo mzito sana maskini hawa. Hofu yangu kubwa sana ni kwamba ipo siku tutaambiwa tuanze kulipia pumzi tunayoivuta. Kama leo mnasema tuanze kulipia vibanda vyetu vidogo vidogo ambavyo tunavyo, leo vifaa vya ujenzi ni gharama, kila kitu ni gharama, lakini wanaopata shida zaidi ni watu maskini zaidi hawa wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba kama mimi labda sikuelewa vizuri, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, atoe tamko kwamba hatukumaanisha tuichokiandika hapa, au wafute kabisa hiki kitu, kwa kweli watakuwa wamefanya jambo baya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ukuaji wa uchumi usiopunguza umaskini. Leo tunasema

kwamba uchumi wa Taifa letu unakuwa kwa asilimia saba. Uchumi huu ambao tunasema unakuwa kwa asilimia saba, lakini uchumi huu haupunguzi umaskini wa Watanzania wetu. Ni kwa nini uchumi haupunguzi umaskini wa Watanzania? Uchumi umebaki kukua kwenye makaratasi kwa sababu sekta ambazo zinachangia katika ukuaji wa uchumi ni sekta zile za utalii, sekta za mawasiliano, madini na fedha. Kwa hiyo, sekta hizi haziwagusi Watanzania walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuza uchumi wetu kupitia kilimo, naamini Watanzania wengi tungekuwa tumewasaidia kwa kiasi kikubwa sana. Mheshimiwa Waziri ninakuomba hii hotuba ya Upinzani tafadhali naomba uisome vizuri. Siku za nyuma mlikuwa mnasema hawa Wapinzani wanakuja na vihotuba vyao vidogo vidogo, makaratasi mawili, matatu; wengine wakaiita *toilet paper*, wengine wakafanya mambo ya ajabu ajabu; leo tumekuja na hii bajeti ya Upinzani mbadala. Mnasema mbona mmeweka kubwa sana? Mnaandika *thesis*, sijui mnafanya nini? Ninyi watu hamwaminiki! Naomba Waziri tafadhali, tumia hii hotuba ya Upinzani, hii ina vitu vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamechukua takwimu; kwa mfano takwimu zile za utafiti uliofanywa na *REPOA*. Ule utafiti unasema kwamba tukikuza kilimo kuanzia asilimia nane hadi kumi tutakuwa tumekata umaskini kwa asilimia 50 ndani ya miaka mitatu. Yaani ndani ya miaka mitatu tukikuza Sekta ya Kilimo kwa asilimia nane hadi asilimia kumi, ndani ya miaka mitatu tutakuwa tumeondoa umaskini kwa Tanzania zaidi ya asilimia 50. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Serikali hii ina nia njema naomba tafadhali chukueni bajeti hii ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba kwa kuwa kuna watu wamezungumza, nami naomba nichangie kidogo kuhusu suala hili la makinikia suala la madini. Naomba tujulize adui yetu ni nani? Adui yetu ni mwekezaji? Adui yetu ni sheria zetu? Adui yetu ni nani?

**MBUNGE FULANI:** Wewe hapo!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, adui yetu ni sheria tulizozitunga; Sheria za Madini na Sheria za rasilimali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, adui namba mbili ni yule aliyetunga sheria hizi ambaye ni Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi. Hii ndiyo iliyotunga sheria hizi. Huyu ndiyo adui. Leo ziko sheria mbalimbali na kuna watu hawasomi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kuna watu ambao hawasomi. Ziko Sheria za Madini; ninayo Sheria ya Madini hapa ya mwaka 1997. Mwaka 1997 kulikuwa na sheria mbili ambazo zilifanyiwa marekebisho. Iko Sheria ya mwaka 1997 ya Madini ambayo ni ya Uwekezaji kwenye Madini, lakini kuna Sheria nyingine ya Madini ya mwaka 1997 ambayo hii Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha ambayo ilifuta kodi kwa wawekezaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali imeamua kufuta kodi kwa wawekezaji wa madini inawatwisha mzigo Watanzania maskini. Hii siyo sahihi kabisa. Leo madini yetu tunapata mrabaha wa asilimia nne, kuna watu walishangilia Sheria hizi mbaya zinapotungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa hata kuona Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wale aliowaita wezi, anawaita Ikulu, anasema hawa jamaa ni jasiri sana. Leo wale wezi wamekuwa jasiri, anasema ni wanaume, lakini kuna wenzetu Wabunge wako humu ndani akina Mheshimiwa Ngeleja na wengine akina Chenge na wengine amesema wasisafiri, hawa watu wamezuiliwa *passport* zao kusafiri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ulikuwapo!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anakuja mtu ambaye ulisema ni mwizi, unasema ni

mwanaume. Kumbe ukilibia Taifa hili kama wewe ni Mwekezaji kutoka nje wewe ni mwanaume. Naomba niseme tu kwamba...

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Mheshimiwa Rais Magufuli hakumwita Mwenye *Barrick* baada ya Rais kushikilia utaratibu, wao wamekuja kukaa mezani kuzungumza na ndiyo ilikuwa *concern* ya Tanzania. Kwa hiyo, nampa taarifa kwamba Mheshimiwa Rais hakumwita Mwekezaji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo na ndiyo sahihi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba huyu bwana nadhani mara nyingi sana vyombo vya habari hafuatilii; taarifa ya habari hasikilizi, magazeti hasomi, *WhatsApp* haangalii. Kwa hiyo, naikataa taarifa yake ambayo ni ya kijinga kabisa na ya kitoto. Siwezi kuipokea taarifa kama hiyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba nchi yetu ilipofika...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu subiri. *Chief Whip!*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI (KAIMU MNADHIMU MKUU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64, naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuendelea lugha ya staha. Hiyo ni pamoja na masuala anayomzungumzia Mheshimiwa Rais kwa misingi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Tanzania ni kuona kwaba rasilimali ambazo tumezipoteza kwa kipindi hicho tunazipata. Hiyo ndiyo iwe *spirit* yetu kuwa-*encourage* wale

waweze kukubali na kutupa rasilimali iliyokuwa imepotea. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge achangeie lakini kwa kweli awe na staha, tuheshimiane na asitumie maneno kama hayo “kijinga” na vitu gani, siyo lugha sahihi. (*Makofi*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo, naomba niseme...

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, sishangai, mimi ndiyo Kiti. Mimi nasimama, nakaa ninapopenda. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais aliweka wazi kabisa wale wote waliohusika waje wakubali wenyewe na biashara. Sikilizeni, subirini. Nawe Ruge umeanza? Mama usifuate mkumbo, Bunge gumu hili! Unaweza ukakaa mwezi mmoja ukaondoka hapa. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alitoa kauli, watu wote wanaohusika ambao wanaona wamefanya makosa, waje waungame. Aliyekuja sio mtu wa *Acacia*, ni mtu wa *Barrick* ambaye ndiye *majority shareholders* wa hiyo kampuni. Msinjibu kitu, kaeni kimya, tulieni kimya hapo.

Jana nilitoa tangazo hapa, kama kuna mtu ana matatizo ya ugonjwa wa kusikia, wako Wauguzi pale wanapima masikio. Nendeni mkatibiwe, pande zote siyo upande huu tu, pande zote nendeni mkatibiwe ili msikie vizuri.

Endelea sasa Mheshimiwa Pascal . (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba Mwenyekiti wangu hata wewe hujui kwamba *Barrick* ndiyo hawa wana hisa zaidi ya asilimia 60 kwenye *Acacia*. Nasikitika kwamba hata hili pia hulifahamu. Sasa kama kuna mtu...

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nikasema kama watu wana matatizo ya masikio, nimesema *Barrick* ndiyo

*shareholders; Acacia ni minority ndani ya Barrick. Sasa nakushauri baadaye upitie kule Dispensary kidogo ukajitizame. (Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hao ndiyo Walimu wetu Tanzania. Hao ndiyo Walimu wetu hao!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia tujaribu kupitia *Dispensary* wote hata ambao hawajui kwamba *Acacia* na *Barrick* wame-*share* hisa. Naomba niendele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili niliache niendele sasa kwenye mambo mengine.

**MBUNGE FULANI:** Wewe hujui!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Watanzania wengi waliofungwa kwa kuiba kuku, ng'ombe na vitu vingine, tukawaite wale tufanye nao *negotiation* pia basi. Tuwaite Watanzania walioba tufanye nao *negotiation*. Kama tunasema huyu ni mwizi ,tukae mezani tufanye *negotiation*, tuwachukue na walioiba na wengine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu, kwamba haya mambo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, muda wako umekwisha, nakuongezea sekunde 30.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mnaona! Namwongezea muda, mnapiga makelele. Ndiyo maana nimewaambia mkatibiwe jamani! Nakuongezea muda sekunde 30. *(Kicheko)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumze suala la mwisho; hilo la madini nadhani na wengine pia wamezungumza nitazungumza baadaye. Niseme tu kwamba kwa kweli bajeti hii imewasahau wafanyakazi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi alisema kwamba mwaka huu anaajiri 56,000 lakini hatujaambiwa tarehe ya kuajiri ni lini? Nataka niseme tu kwamba *msaliti namba moja* wa Watumishi wa Umma ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ndio mtumishi namba moja. *(Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiwa Mtumishi namba moja, leo hajaajiri, watu wamehitimu vyyuo, hawaajiri kwa nini?

**MWENYEKITI:** Hebu kaa chini Mheshimiwa Pascal. Mheshimiwa Pascal, jamani hebu tufuate hizi Kanuni. Sikuombi, nakuagiza, futa hilo neno msaliti namba moja sasa hivi. Sasa hivi futa hilo neno. *(Makofi)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme nimefuta hii, lakini niseme amewasahau Watumishi hajawaajiri. Nimefuta hii kauli ya... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Futa, kaa chini. Umeshafuta kaa chini na muda wako umekwisha. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakaporudi saa 10.00, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Gibson Meiseyeki, Salum Rehani na Mashimba Ndaki.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza na majina tuliyoyatangaza asubuhi, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Gibson Meiseyeki, wajiandae Mheshimiwa Salum Rehani na Mashimba Ndaki. Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kuipongeza hotuba iliyowasilishwa na Kambi ya Upinzani hapa Bungeni. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri hata leo hayupo na wakati hotuba ile inawasilishwa hakuwepo lakini bahati nzuri kipindi chote Naibu Waziri amekuwepo. Kwa manufaa ya Taifa hili, naomba hiyo hotuba pamoja na kwamba ina kurasa nyingi hebu wajaribuni kuisoma, itawasaidia sana na itasaidia Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujisema mimi mwenyewe kwamba miaka ya 2000 niliwahi kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ndani ya Bunge hili nikiongoza vyama vitano. Kwa hiyo, bajeti zote ambazo zilipita wakati wa kipindi changu nikiwa Kiongozi (KUB) ni bajeti ambazo hata tukienda kutafuta kwenye *Hansard*, hakuna bajeti hata moja ambayo Wabunge wa CCM hawakuipitisha mia kwa mia, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hata nilipokuwa gerezani kwenye kesi feki ya ugaidi kwa kipindi cha miezi kama minne hivi, nampongeza Kamishna wa Magereza aliruhusu nika-*own radio* nikiwa gerezani na kipindi cha bajeti zilipitishwa kwa maneno matamu kweli na Wabunge wa CCM. Yale maneno haijawahi kutokea, hii ni bajeti ya kihistoria, hii ni bajeti ya kizazi kipya, kwangu mimi ambaye nina *experience* na Bunge hili chini ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake ni maneno ambayo mimi nayaona ni swaga za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nadanganya twende tu huko mbele, hakuchi, kutakucha hata hii bajeti utasikia



inapigwa mapiku hata bajeti zingine zijazo. Kwa hiyo, kwangu mimi nafikiri mvinyo ni ule ule kinachobadilika ni chupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waziri atakapokuja ku-*wind up* na najua atatanguliwa na baadhi ya Mawaziri ambao wako Serikalini kujibu katika maeneo yao, hebu tuambieni wananchi wa Kagera, Bukoba, Kanda ya Ziwa meli ambayo tumekuwa tunaahidiwa tangu *MV Bukoba* izame na watu wengine bado wamo humo humo ndani ya meli hiyo mpaka leo, inaonekana wapi katika nyaraka hizi, hotuba hii na bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametaja meli za Nyasa, viwanja vya ndege ambavyo vimekuja baada ya tukio la *MV Bukoba* na hata lugha ya kuizungumziazungumzia hii meli mpya ambayo tumekuwa tunaahidiwa na Awamu zote za uongozi wa nchi hii chini ya Chama cha Mapinduzi inaanza kueleaelea au kufutikafutika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, badala ya kueleza kijuujuu tuelezeni maandalizi ya hiyo meli yako wapi, inakuwa *designed* wapi, nchi gani na imetengewa hela kutoka wapi? Taarifa hizi zitasaidia wananchi wa Kagera, Bukoba na Kanda ya Ziwa kwa ujumla kufahamu moja nini kinachoendelea. Kama wametupotezea tu kijuujuu ni bora wakatamka bayana kwamba hamna hela na wala hamna nia ya kutupa meli mpya. Sasa hivi dunia ni kijiji, mimi naamini kuna watu wako nchi nyingine wanaweza kujitolea kutuletea meli wananchi wa Kagera, Bukoba ambao wanatambua mateso tunayoyapata kuliko kuendelea kuuziwa mbuzi kwenye gunia (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kahawa, tumesikia hapa kodi zimeondolewa. Nataka Waziri atakapokuja ku-*wind up* na kwa kuwa nafahamu hata Waziri wa Kilimo anaweza akachangia katika ku-*wind up* kwa upande wa Serikali atueleze maana sehemu kubwa ya kodi zilizoondolewa zinawazungumzia watu wa kati na wale ma-*processor*. Watu wa Kagera na Bukoba *Town* ambao tuna

vijiji vinavyolima kahawa pale *greenbelt* vijiji vya Kata za Kibete, Kitendagulo, Iduganyongo, Nyanga wanauza kahawa, wawaeleze kilo moja kwa kodi hizi zilizopungua inakwenda kupanda kwa kiasi gani? Hicho ndicho mkulima anachohitaji siyo maneno maneno haya ya jumla jumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nakubaliana na nawaunga mkono Waheshimiwa Wabunge waliochangia sana hapa kwamba katika suala la madini na vita ya rasilimali inayoendelea inahitaji uzalendo na mshikamano wetu wote. Hilo naliunga mkono na naweza nikalipigania mimi kama Lwakatare. Hata hivyo, uzalendo ni lazima utengenezewe mazingira. Huwezi kutoka hewani unazungumzia tuwe wazalendo, tuwe na mshikamano, lazima tutengeneze mazingira ambayo yatawezesha, kwanza tuheshimiane humu ndani, tutambuane umuhimu na tuheshimu hoja ambazo ni kinzani kwa nia ya kujifunza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi maana natoka Kagera mimi Mlangira mimi, sili chakula ambacho ni *half cooked*, ni kwamba mambo ya kubebeshana maiti ambapo hatujui marehemu kafia wapi tunakuja kubebeshana tu, mimi siko tayari kuibeba hiyo maiti. Tungetaka kutokea kwa viongozi wetu wakuu wawe *consistency* maana kiongozi anakwenda mahali fulani anasema mimi kwa *capacity* yangu siwezi kumteua Mpinzani kwenye Serikali yangu, haijapita kipindi anateua Wapinzani. Jamani dunia ni kijiji kuna wenzetu wanatushangaa kwa matamko tunayoyatoa. Hiyo inafanya tunashindwa kuwa na *consistency* ya matamko ya viongozi wetu na dunia wanashindwa kuelewa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kumalizia nalo, naomba bajeti hii Mheshimiwa Waziri leo yuko Naibu Waziri lakini Serikali iko pale pale, wamwongeze pesa Msajili wa Vyama vya Siasa na iende *purposely* kwa ajili ya kujenga *capacity* kwenye vyama vyetu, vyama vinapaswa kujengewa *capacity*. Chama cha kwanza ambacho kwa

kweli kutokana na michango na yale yanayoendelea naona kijengewe *capacity* ni Chama cha Mapinduzi. Haiwezekani kwa miaka 56 ya Uhuru tunaendesha Serikali kwa *individual capacity* badala ya taasisi. Matokeo yake Mheshimiwa Rais wamemuachia mzigu ndiye anaendesha Serikali wakati tuna Baraza la Mawaziri hewa, viongozi wa taasisi hewa, Wakurugenzi hewa kwa sababu wote wanakwenda kwa mtindo wa ndiyo mzee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani yanayoonekana sasa hivi na mimi namkubalia Ndugu yangu Mheshimiwa Bwege alisema sasa hivi inayoendesha Serikali ni Serikali ya Magufuli aliyoisema yeye mwenyewe, Watanzania chagueni Serikali ya Magufuli, hakuna Serikali ya CCM hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya hili inazaa suala la watu kujipendekeza, kila mmoja anajipendekeza kwa mtu mmoja anayeendesha Serikali. Msajili akijengee Chama cha Mapinduzi *capacity* ya kuendesha Serikali kitaasisi. Matokeo yake huyu Rais jamani tutamua bure, kubeba mizigo ya Wizara zote, taasisi zote, makontena ya madini anatembelea yeye, yeye ndiyo anapanga bajeti, akiamua sijui... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gibson, wajiandae Mheshimiwa Salum Rehani na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuunga mkono maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii. Kama alivyosema mwenzangu, Waziri achukue muda kwenda kupitia mapendekezo hayo kutoka Kambi hii,

wataalam wetu wamepitia na kuja na mapendekezo ambayo yangeweza kumsaidia sana kuweza kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuiasa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa kufuata utawala wa sheria. Tutapona sana na itakuwa na manufaa makubwa sana kwa nchi yetu kama tutaongozwa kisheria. Hivi karibuni tumekuwa tukiongelea sana masuala ya Sheria zetu za Madini, kumekuwa na maneno ya ajabu ajabu kupinga wengine ambao wanatoa mapendekezo lakini tunashukuru kwamba kwa namna fulani Serikali imechukua mapendekezo ya baadhi ya watu ambao wanaitwa waropokaji na sasa tunaona kwamba sheria hiyo inataka kuletwa hapa Bungeni kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa wataalam wetu wa sheria, Waziri wetu wa Sheria asisite kutumia rasilimaliwatu walioko upande huu katika kuleta marekebisho ya Sheria hiyo ya Madini ili tuweze kupata sheria ambayo italinusuru Taifa hili katika kutokupoteza rasilimali madini tuliyonayo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sitasita kumshukuru Mheshimiwa Lissu kwa uelewa wake katika eneo hili. Ningependa kama inawezekana Serikali bila kuona aibu isisite kuchukua maarifa ambayo wataalam au kwa watu ambao wamebobeza kwenye maeneo hayo wakatengenezea kitu ambacho tukija hapa kama ilivyo desturi yetu tutapitisha tu kwa 'ndiyo' tupitishie kitu ambacho kimefanyiwa kazi vizuri na kiko *balanced* ili tuweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Maazimio yalikuja hapa ya kumpongeza Rais, lakini mimi niseme kwa uelewa wangu msingi mkubwa wa hasara ambayo tumeipata kwenye madini na matatizo yote haya yamejikita kwenye Katiba yetu, ni sheria lakini na Katiba pia. Ningekuwa mtu wa kwanza kabisa, tena na kubeba mabango ikiwezekana nitaingia huku na vuvuzela kumpongeza Rais kama angetuletea

Mapendekezo ya Warioba, ile Rasimu ya Pili ya Warioba ikaletwa hapa Bungeni tukapitisha kama Katiba yetu. Tutakuwa tumelitatua hili tatizo pale kwenye kiini chake lakini haya mazingaombwe ambayo naona yanataka kufanyika hapa katikati hayatatufikisha popote kwa sababu msingi wa makosa yote umejikita sehemu ambayo hatutaki kuigusa. Kwa hiyo, mimi ningeomba tukali-*attempt* hili maana Wazungu wanasema *you can not solve a problem with the same mind that created it*. Nasema kwamba tulite Katiba, tuibadilishe hapa, tutakuwa tumetatua kwa kiasi kikubwa sana mlolongo wa haya matatizo ambayo yako kwenye sheria zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme hivi karibuni kumekuwa na kulipukalipuka kwa watu kutekeleza mapendekezo au tuseme sheria mbalimbali zilizopo. Hivi majuzi nimeona watu wakiingilia kwenye mashamba ya wawekezaji tena moja la Mwenyekiti wetu, wakaenda wakafanya uharibifu mkubwa. Nasema huko ni kukurupuka na tukikurupuka tutaipeleka nchi hii kama walivyosema wenzangu, wataipeleka kama ilivyo Zimbabwe sasa hivi ambako wote tunafahamu kwamba Zimbabwe haitumii *currency*yake sasa hivi kwa sababu, kwa bahati mbaya neno ambalo lilikuwa linakuja sio zuri, wamejiharibia wenyewe. Ilifika wakati wanaenda kununua kilo ya sukari kwa mfuko wa fedha na sasa hivi wanatumia fedha za kigeni kama *bill of exchange* kwenye nchi yao. Sasa tukikurupuka kurupuka na sisi kwenda kuvamiavamia watu nadhani tutaishia pabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ambayo yana sifa kama alilokuwa nalo Mheshimiwa Mbowe yako mengi sana na kama Wakuu wengine wa Wilaya wao hawatatekeleza kama alivyotekeleza yule pengine siku moja wendawazimu wengine kama sisi au mimi tutaenda kuwasaidia kuharibu. Maana katika Wilaya yetu ya Arumeru wawekezaji wenye mashamba ya maua ambayo yamekaa pembezoni mwa maji au mito ni karibu mashamba yote lakini sijui ni nani huyo na akili zake ziko vipi amekurupuka ameenda kuvunja shamba la Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mienendo kama hii haitatupeleka pazuri. Kama ni operesheni ya kuondoa mashamba ambayo yako pembezoni mwa mito basi mashamba mengine yote ya maua, miwa, mpunga nafikiri ni vyema yakahakikiwa na yenyewe ili hii kama ni sheria basi ile pande zote lakini tuwe na tahadhari, tusije tukaipeleka nchi yetu kwa akina Zimbabwe na Venezuela. Nilitaka niseme hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaka kwenda kwenye bajeti nianze kwa usemi wa mwanamuziki hayati Bob Marley maarufu kwa *taste* ile ya *reggae*, aliwahi kuimba kwenye wimbo wake wa *get up, stand up* akasema, *you can fool some people sometimes but you can not fool all the people all the time.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti iliyoletwa hapa inataka kututegatega. Watanzania wa sasa hivi ni werevu sana, tusidhani ni kama wale watu wa miaka ya 60, 70, watu wamezidi kujanjaruka kwa hiyo huwezi kutudanganya. Nimwombe tu Waziri wa Fedha hili suala mnalosema elimu bure kwa bajeti hii tuanze kulifuta kwa sababu umedanganya kwa upande huu halafu sasa kwa upande huu unakuja ku-*balance*. Watoto wengi ambao wanasoma kwenye shule zetu za msingi ni zile familia ambazo kiukweli hata umeme wanausia tu hawajawahi kuuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unapowawekea hizi Sh.40/= kwa kila lita moja ya mafuta hao ni kwamba unaenda kuwatoza zile hela zako ulizosema elimu bure, kwa hiyo tuifute. Utapitisha bajeti yako hii kwa Sh.40/= kwa kila lita moja ya mafuta ya taa, nazungumzia mafuta ya taa, petroli na dizeli tutajua huko mbele lakini mafuta ya taa, maana yake ni kwamba unakwenda kuwatoza Watanzania ile pesa ya ada ya shule waliyokwenda kuilipa, ndiyo maana yake na wajanja wameshajanjaruka. Kwa hiyo, hapa hamna elimu bure, *you are charging us.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Waziri mwaka jana tulizungumza mengi kuhusiana na bandari.

Walikwenda pale wakasema hata zikiingia meli mbili kama zile nyingine haziingii, sasa kule kumetetereka amekuja hapa anatuambia kwamba uchumi wa dunia umeyumba, sio kweli! Siku hizi tunakaa na simu zetu hapa, tunaangalia Beira, Mombasa, Tanzania sasa hivi Bandari yetu ya Dar es Salaam inakaribiana na Kismayo Somalia kule kwenye ma-*pirates* kwa jinsi ambavyo hakuna meli sasa hivi. Sasa wasituambie kwamba uchumi umetetereka, hapana! Walizinyima hizo meli jana kuja na tuliwaambia wakakataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaambia tena kuhusiana na VAT kwenye utalii, wameleta ndege sijui nani atazipanda hizo *Bombadier* ambayo tunajua moja tayari iko *grounded* na ilikuwa mpya. Hawawezi wakaleta ndege, apande nani wakati utalii huku kwao wana-*discourage*? Wenzetu wa nchi za jirani wamefuta VAT, wao wamekomalia. Sasa utalii utaanguka halafu mwakani atakuja kutudanganya kwamba kuna mtikisiko wa kiuchumi. Hii tunai-*note* na mwakani sijui atatuambiaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii naomba tunapo-*set priorities* tuzisimamie. Rais alipokuwa anaomba kura hata na sisi wote tatizo la maji tulliona tumeli-*address* na akasema anaenda kuleta suluhu ya shida ya maji nchini. Hata hivyo, wameingia madarakani cha ajabu ni kwamba hela nyingi wamezipeleka kwenye kuleta ndege mpya ukilinganisha na walizozipeleka kwenye maji. Pesa za kununua ndege zimezidi karibia bilioni 50 pesa walizopeleka kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida ya maji, Arumeru yangu tuna kiu sana ya maji tuangalie *priority* zetu, tunapopata fedha tusikengeuke, twende kwenye zile *areas* ambazo tulisema kwamba tunaenda ku-*accomplish*. Kwa hiyo, naomba tu-*stick* kwenye bajeti kama tulivyokuwa tumeipendekeza ili tuweze kumaliza kero nyingi ambazo wananchi wanazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida sana, tunahitaji barabara, mwaka jana swali langu moja lilijibiwa na Naibu

Waziri, nafikiri ni wa Ujenzi, akasema kwamba barabara yetu inayounganisha Arusha na Simanjiro inafanyiwa upembuzi yakinifu. Walisema shilingi milioni 600 imeshapelekwa pale isije ikawa tena miaka mitano. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum Rehani kama hayupo Mheshimiwa Ndaki na ajiandae Mheshimiwa Stephen Masele.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kutuletea bajeti nzuri lakini pia niwashukuru sana watendaji wao wakuu, Katibu Mkuu pamoja na timu yao hiyo nyingine iliyopo ofisini. Wamefanya kazi nzuri na wametuletea bajeti ambayo kila Mtanzania aliposikia alifurahia na alipongeza. Kwa hiyo, nawapongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwapongeze pia TRA kwa makusanyo yao mazuri ambayo kupitia hayo yametusaidia kufanya mambo makubwa kwa mwaka huu unaoisha na naamini hata kwa mwaka ujao tunaweza kuendelea kufanya mambo makubwa zaidi. Tumelipa mishahara sisi wenyewe, tumelipia reli sisi wenyewe, tumelipia ulinzi na usalama wa nchi yetu sisi wenyewe, tumelipia ndege ingawa watu wanazidharau lakini tumelipia sisi wenyewe, kwa hiyo imetusaidia kujitegemea kama nchi kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa watu wa *TRA* ni kwamba waweze tu kuongeza kujenga mazingira mazuri kwa walipa kodi wetu ili makusanyo yao yaweze kuongezeka. Wafanye juu chini kuwafanya walipa kodi wetu wajisike fahari kulipa kodi yao, waone kwamba wanastahili kulipa, waelewe kwamba kulipa kodi ni ustaarabu lakini wataona hivyo baada ya wao *TRA* pia kujenga mazingira mazuri kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba kodi za *TRA* zieleweke, mtu akitaka kuanza biashara fulani ajue kabisa atatakiwa kulipa kodi zipi. Kuwe na namna za kodi elekezi ambazo *TRA* wanakuwa nazo ili mimi nikitaka kufanya biashara nijue *TRA* watachukua hela yao kiasi gani hapa. Unajua wafanyabiashara wanataka mambo yao yajulikane, yawe wazi na wanataka uhakika ili atakapoingia kwenye biashara aweze kupata faida anayoitarajia. Uchumi wetu unakua, kwa hiyo lazima pia *TRA* wajenge mazingira ya biashara kukua, ya kilimo kukua na uchumi wetu kuendelea kupanda vinginevyo makusanyo yao yanaweza yasiwe endelevu sana kama biashara na kilimo havikui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie pia upande wa ajira pamoja na mzunguko wa fedha, hivi vitu vina uhusiano sana. Fedha au pesa inazo tabia nyingi lakini tabia mojawapo ni kwamba pesa ni adimu, *money must be scarce or limited in supply* na pesa inazunguka kwa mtu ambaye anafanya kazi, pesa haizunguki tu kwa zamu kwamba ni zamu yako imefika, inazunguka kwa mtu ambaye anafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naisihi Serikali itengeneza mazingira ya watu kufanya kazi ili kwamba waweze kupata pesa. Naiomba Serikali waanze kufikiria miradi ambayo itazalisha au itatoa mazao kwa haraka, inatoa faida kwa haraka, hiyo nayo watie nguvu hapo ili kwamba watu wafanye miradi kama hiyo waweze kupata pesa. Miradi ambayo tunaita ni *quick wins* au *low hanging fruits* ili watu waweze kujiingiza huko na kupata hela mzunguko wa pesa uweze kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi kama hiyo ni kama wachimbaji wadogo, viwanda vidogo vidogo vikitiwa nguvu na moyo vinaweza vikafanya mzunguko wa fedha ukawa mkubwa kwa sababu wengi wataingia huko. Pia miradi mikubwa ya kielelezo ambayo nchi yetu imekwishakuianza iajiri Watanzania. Najua kandarasi kubwa wamepewa watu wa nje lakini tuwe na utaratibu ambao hata nadhani sheria zetu unaukubali kwamba Watanzania waajiriwe wengi kwenye miradi hii, wanaweza kuajiriwa wale watu wakubwa wakubwa kule juu kidogo lakini hapa katikati na huku chini waajiriwe Watanzania ili waweze kupata pesa iweze kuzunguka hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *NGO's* zilizoko kwenye nchi yetu hii walazimishwe waajiri Watanzania. Hizi *NGO's* nazo wanapokuja hapa wanalazimisha kuleta watu wao kutoka nje. Nafikiri umefika wakati sasa kazi hizo zinazofanywa kwenye *NGO's* zifanywe na Watanzania kwa sababu tuna ujuzi na weledi wa kutosha kufanya kazi hizi ili pesa zinazokuja kwa sababu wanazileta kwa lengo la kusaidia umaskini wetu, basi umaskini wetu uwe ni fursa isiwe ni kitu ambacho ni balaa au kinatupita pembeni. Watanzania wengi waajiriwe kwenye hizi *NGO's* kuanzia chini, katikati na hata juu ili pesa zinazokuja zizunguke hapa na zitusaidie kweli kama wanataka kuondoa umaskini kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kazi za makampuni makubwa ya hapa nchini pia yapewe kazi kubwa kubwa. Nimesikia juzi Mheshimiwa Makamu wa Rais anasema wakandarasi wanaweza wakapata kazi isiyozidi shilingi bilioni 10, nadhani hili ni jambo zuri kwa sababu hawa wakandarasi wa ndani wakipewa pesa kama hiyo itafanya izunguke hapa ndani na kufanya mazunguko wa fedha uwe mkubwa hapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la kukuza viwanda kwenye nchi yetu. Kwanza nipongeze kabisa hotuba ya Mheshimiwa Waziri hasa kwa upande wa viwanda vinavyozalisha mafuta ya kula kwamba wameweka tozo/

ushuru kwenye mafuta ghafi yanayoingia kutoka nje hasa yanayotokana na mawese. Hongera sana kwa jambo hili kwa sababu tozo hii ilikuwa imeondolewa hapo nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tozo hii iongezwe badala ya asilimia 10 aliyoiweka Mheshimiwa Waziri iwe asilimia 15 ili kulinda viwanda vyetu vya mafuta ya kula hapa ndani lakini pia kulinda wafanyabiashara wetu. Kwa sababu hata hayo mafuta wanayosema wanaingiza mafuta ghafi lakini ukiyachunguza asilimia ya mafuta ghafi ni kama 10 tu, asilimia 90 ya mafuta haya yako kamili kabisa. Kwa hiyo, ili tuweze kujenga viwanda vyetu, ushuru kwa bidhaa zinazotoka nje lazima uongezeke ili tuweze kulinda viwanda vyetu hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie suala la wastaafu hasa wale wanaopata pesa zao kupitia Hazina, walio na *account* zao Benki ya Posta. Hawa wana dirisha la kupata mikopo huko Benki ya Posta lakini wanapoomba mikopo yao nyaraka zinachelewa sana kutoka Hazina tofauti na nyaraka au na wale ambao walikuwa kwenye Mifuko ya *PSPF* na *LAPF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri awafikirie hawa wastaafu maana na wenyewe bado maisha yanaendelea, kwa hiyo tuwasaidie wale wanaopata hela zao kutoka Hazina wakiomba mikopo kupitia Benki hii ya Posta wapewe mikopo yao mapema, hiki kisingizio cha nyaraka zinachelewa nadhani hakina sababu ya kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kama muda wangu pia utakuwa haujaisha niongelee suala la ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha. Mheshimiwa Rehani umerudi, baada ya Mheshimiwa Rehani jandae Mheshimiwa Shaabani Shekilindi.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi yangu. Nami nashukuru kupata fursa ya kuchangia kwenye bajeti hii kuu nikiwa nataka kujielekeza kwenye mambo manne ambayo nahisi yanaweza kuisaidia Serikali lakini kumsaidia Waziri sasa kuweza kujipanga zaidi katika kuhakikisha anapata mapato ya kutosha kutokana na vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwanzo ninalotaka kuzungumza ni suala zima la bandari bubu na magendo yanayofanyika kwa bandari zetu kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara. Biashara kubwa inayofanyika hapa ni mafuta ya kupikia. Hii biashara imekuwa ni kubwa na kama nchi hakujawa na utaratibu mzuri wa kudhibiti hizi bandari lakini kudhibiti zile bidhaa zinazolingia pale Zanzibar na kutawanywa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii inafanyika kupitia bandari ndogo ndogo mbalimbali na kushushwa katika bandari ndogo ndogo hapa Dar es Salaam na bidhaa nyingi zinazosafirishwa ni mchele, mafuta, sukari, mafriji yale *used*, redio, mipira *used* kitu ambacho kwa kiasi kikubwa kinaikosha Serikali mapato. Hii imetokana na mfumo mzima ule wa ukusanyaji mapato kule Zanzibar, *double tax*, ndicho kitu kinachosababisha wafanyabiashara kukimbia kulipa kodi mara mbili katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa sababu wao wanaleta bidhaa pale Zanzibar wakishashusha kwenye makontena wanalipishwa ushuru, *TRA* wanachukua chao na *ZRB* wanachukua chao, lakini mtu yule yule akisafirisha mzigo ule kuuleta bandari ya Dar es Salaam analipa tena kodi mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie wazi Mheshimiwa Waziri, kiwango kikubwa cha bidhaa zile au mafuta yanayoingia Tanzania Bara asilimia 80 yanapitia Zanzibar. Hiyo ni taarifa rasmi naomba aifanyie kazi na si hivyo tu, mipira *used* na vifaa vingine *used* vinavyoletwa kutoka nje vinashushwa tu Zanzibar lakini vinaishia Tanzania Bara na maeneo mengine kwa njia za panya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kujipanga sasa kuhakikisha hii kero inayotajwa kila siku kwamba tumemaliza tatizo la tozo ya ushuru wa mara mbili kwa biashara au kwa bidhaa zilizoko Zanzibar zinazolingia Bara bado halijamalizika na imekuwa maneno ya kila siku. Hili nimwombe Waziri ulifanyie kazi na tufike mahali iwe mwisho wa hili suala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia eneo lingine ambalo Serikali bado ina nafasi kubwa ya kuwekeza na kuweza kujipatia mapato mengi. Nimeangalia bajeti vya kutosha lakini bado wito wetu tunaoutoa na kulia kila kwenye suala zima la uvuvi wa bahari kuu na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata samaki halina kipaumbele. Nimwombe Waziri hesabu za haraka haraka, sasa hivi duniani mpaka juzi nilivyokuwa natembea kwenye mitandao ndani ya soko la dunia kuna mahitaji ya tani 271,000 kwa mwezi za samaki ambazo zinahitajika zikiwa *processed* ambao ni *cane fish*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama nchi ingeweza kuwa na hii tunaita *pot fish* moja tu au mbili zinaweza kutengeneza ajira zaidi ya watu 30,000 kwa kila meli inayo-*land* kwa kipindi cha miezi mitatu watu wale wanafanya kazi lakini pato linalopatikana kwa meli moja tumeshawaeleza mara nyingi pale ile *process* nzima ya meli moja ni zaidi ya dola 85,000, pesa zile zinakuwepo ndani ya nchi, zinasaidia Watanzania na watu wengine. Vilevile bahari yetu tumeshaeleza mara nyingi jamani, hivi sasa pamoja na mazingira mengine yaliyoko katika maeneo mengine *current* ya maji katika maeneo yetu ni *very conducive* kuliko maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Namibia *current* imechafuka, Mozambique *current* imechafuka, Tanzania *current* ni *conducive*. Kwa hiyo, *stock* kubwa ya samaki imekusanyika katika maeneo yetu na ndiyo maana meli nyingi za nje zinakimbilia kuvua katika maeneo yetu kwa sababu kuna mazingira rafiki ya kuishi. Si hivyo tu, wenzetu wa Philippine na Mataifa mengine ya nje yanakuja kumwaga vyakula

katika maeneo ya Tanzania ili kuwavuta samaki kuwepo kwa wingi na kuvuna samaki wale kwa njia ya kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu nyingine tuendeleze uvuvi mpya unaoingia hivi sasa wa kutengeneza uvuvi wa kutumia *cadge*. Utafiti tayari umeshafanyika na *cadge fishing* imeonekana kuwa na mafanikio makubwa. Leo hii wavuvi wetu wengi walikuwa wanavua majongoo kwa kutumia gesi lakini leo baada ya kufanyika utafiti, wavuvi hawa wanaweza kuvua kwa kutega *cadge* tu ndani ya *deep sea* na *cadge* moja ina uwezo wa kuingiza mpaka milioni 24 kwa mvuo mmoja tu wa kipindi ambacho utaweza kufuga wale samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kusiwe na mipango mahsusi kuwawezesha wananchi hawa, wakawa na vyombo vya kisasa wakaweza kwenda kuweka *cadge* zao katika *deep sea*, wakavua kwenye *deep sea* na tukaweza kupata samaki wa kutosha lakini tukaanzisha viwanda vya kuchakata samaki na kufunga na kusafirisha nje, wakati soko sasa hivi linatafuta bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisema ni kwamba bado tuna tatizo kwenye kilimo. Tunasema kilimo tumekipa kipaumbele lakini bado sijaona mikakati halisi ya kusaidia kilimo cha Tanzania kikaweza kuonesha mafanikio na kuwasaidia wakulima wengi katika nchi yetu. Nitoe mfano mmoja wa kahawa bado kuna urasimu katika soko la kahawa, soko la kahawa lazima uende Moshi, lakini tuna kiwanda kipo Mbinga kilianza kuchakata na kutengeneza Mbinga *Instant*, kahawa ile ikawa imepata soko kubwa tu katika nchi mbalimbali zikiwemo Ulaya hata Zanzibar na maeneo mengine lakini bado Serikali haikutoa msukumo wa kufanya eneo lile likaweza kuzalisha na kufanya *canning* ile kahawa iliyoko katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeweza kukianzisha kile kiwanda cha Mbinga kingehamasisha kilimo cha kahawa katika maeneo yote yale ya Mikoa ya Ruvuma lakini hata maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara yale ambayo

yanakubali kahawa ingeweza kuzalishwa, lakini Njombe ingepata fursa kubwa zaidi ya kuzalisha kahawa na ikaingia katika ramani ya maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa wa kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe vitu kama hivi Serikali itie mkono wake si tu kuiachia pengine kampuni au Halmashauri na wananchi wenyewe wakaweza kufanya kitu kama kile, lakini ile ile ingesaidia urasimu wa kutoa kahawa Mbinga kuipeleka sokoni Moshi. Vilevile ungesaidia urasimu wa kutoa kahawa Mbozi ukaipeleka Moshi, tunapoteza gharama kubwa ya uzalishaji bila ya sababu wakati huku tunasema Serikali inaondoa tozo lakini tunaanzisha tozo nyingine ambazo tunaweza kuzipunguza na... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, ajiandae Mheshimiwa Mussa Sima na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi kusimama kwenye Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kumpongeza Waziri wa Fedha na Naibu wake kwa hotuba nzuri ambayo siku ile ya kusoma hotuba Watanzania wote naamini walikuwa kwenye luninga na kwenye redio kusikiliza hotuba na walifurahi mno. Kwa hiyo, hotuba hii kwa kweli imejibu kiu ya Watanzania hususan wale wa hali ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais wangu, Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli kwa kazi anayoifanya kwani sisi katika upande wetu wa dini unasema kwamba Mwenyezi Mungu anapomchagua mtu wake anamtuma Jibril. Jibril anapeleka majibu kwa Mwenyezi

Mungu kwamba Mwenyezi Mungu nimeleta jina la Joseph John Pombe Magufuli kwamba huyu ndiyo anakubalika kwa watu, Mwenyezi Mungu anaidhinisha. Mwenyezi Mungu anapoidhinisha anatuma malaika, malaika wanakuja kwetu sasa kusambaza kwenye mioyo ya wananchi kwamba mchagueni John Pombe Magufuli huyu ndiyo Rais wa kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni tunu ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu ambaye hamuungi mkono Rais wetu kwa juhudi hizi anazozifanya, basi apimwe akili kwa sababu naamini kabisa huu ni ujumbe wa Mwenyezi Mungu, ameletwa na Mungu huyu. Kwa hiyo, kama mtu hatamuunga mkono tunaita ni kizazi cha shetani. Mara nyingi viongozi wazuri wanapofanya kazi vizuri basi wale ambao ni mlolongo wa shetani huwa wanapinga. Kwa hiyo, usione watu wanapinga ujue ni mlolongo wa shetani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendeleo kuchangia, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mpango na timu yake kwa ujumla hasa kwa kutoa hii tozo ya *Road Licence*. Hata hivyo, nimuombe tu sasa kwamba amekula ng'ombe mzima amebakisha mkia, kuna hii *fire extinguisher* na *sticker* zake ni kodi kandamizi ambayo kwa kweli naomba aiangalie na ikiwezekana nayo iondoke. Kwa sababu yeye mwenyewe naamini anakiri kwamba gari ikipata ajali ule mtungi wewe abiria, dereva au *turnboy* huwezi kuamka na kuzima gari ile au hao watu wanaokata *sticker* hizi za *fire extinguisher* hawawezi kuzunguka barabarani na kukuta gari inaungua na wakazima sijawahi kuwaona. Kwa hiyo, naona hii ni kodi kandamizi itolewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna hawa vijana wetu wa bodaboda wameamua kujajiri na hili ni kundi kubwa sana, nao ikiwezekana hii *SUMATRA* itoke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye suala zima la viwanda. Nashukuru kwenye hotuba ya Waziri amesainisha mikoa ya viwanda ikiwemo



Tanga lakini cha kushangaza Mheshimiwa Mpango kwenye hotuba yake anasema atatengeneza viwanda vipya wakati Tanga kuna viwanda vimekufa mfano Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha *Afritex* na Kiwanda cha Foma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna Kiwanda cha Chai cha Mponde hakifanyi kazi na hapa lazima niseme, tumeongea vya kutosha, kiwanda kile hakina tatizo lolote ni kizima kabisa, kinaendelea tu kulipiwa bili za umeme. Wananchi, wakulima wa Mponde wanapata tabu sana. Imefikia hatua sasa hata ule mlo mmoja kwa siku hawaupati, hawapeleki watoto wao shule, hawana ada, hata bili ya umeme wameshindwa kulipa. Kwa hiyo, nimwombe Waziri Mpango kwa unyenyekevu na heshima kubwa aliyokuwa nayo atenge hata shilingi bilioni nne akafungue kiwanda kile ili tuweze kuokoa maisha ya wananchi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la maji. MWewe ni shahidi wakati unaniona nimevaa mabuti niko kwenye barabara ya Soni – Mombo - Lushoto, kumenyesha mvua nyingi mno. Nashindwa kuelewa nimeshaongea sana mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Wizara sasa ipeleke wataalam wa kutujengea mabwawa ili yatumike kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji cha mboga mboga na kuwapa wananchi maji. Vilevile mabwawa haya yatazuia uharibifu wakati wa mafuriko hata kama yatashuka, yatashuka kidogo sana. Niiombe Serikali hebu itenge fedha za kutosha ili ipeleke vijijini ili wananchi wa vijijini waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, hizi fedha zinazoenda Halmashauri kwa ajili ya maji naomba sasa mfumo ubadilishwe. Kuna watu wanaitwa *DCCA* wapewe kazi hawa au kuundwe Mamlaka ya Maji Vijijini, naamini hawa wataenda sawia kabisa na kuboresha huduma na kwenda kwa kasi zaidi ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zangu zimeharibika mno. Nimeomba kwa muda mrefu sana

barabara ya kutoka Mlalo - Ngwelo – Mlola – Makanya - Milingano - Mashewa ipandishwe hadhi lakini mpaka sasa hivi bado haijapandishwa. Nimwombe Waziri Mheshimiwa Mpango ikiwezekana barabara ile sasa ipandishwe hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua barabara yetu ile inashuka matope na mawe, inafunikwa kutokana na mafuriko, kwa hiyo, ningepomba sasa tupate barabara mbadala. Kuna barabara inaanzia Dochi - Ngulwi - Mombo kilometa 16 tu, niombe Serikali yangu tukufu, sikivu iweze kunisaidia barabara ile ili wananchi wangu wa Lushoto wasiishi kisiwani. Pamoja na hayo, Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kilometa nne, nizikumbushie kwa Waziri Mheshimiwa Mpango aweze kutupa hizo kilometa ili tuweze kutengeneza Mji wetu wa Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vituo vya afya, wananchi wangu nimewahamasisha wamejenga vituo vya afya zaidi ya vinne, vimefikia hatua ya lenta lakini kama ilivyo ada Serikali imesema kwamba wananchi wakijenga ikifikia hatua ya lenta basi Serikali inachukua. Kwa hiyo, niombe Serikali sasa nimeshafikisha hatua ya lenta hebu wanipe pesa ili niweze kumaliza vituo vile ili wananchi wangu waweze kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji umeme vijijini. Nishukuru Serikali ya Awamu ya Tano ina kasi sana ya kusambaza umeme vijini lakini imetoa vijiji vichache sana. Niiombe sasa Serikali yangu, sisi tumeshaahidi kule kwamba jamani umeme unakuja kama Ilani ya chama inavyosema, sasa unapopata vijiji hata 10 havizidi sijui tutawajibu nini wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, milioni 50...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina wageni 15 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni Wataalam wa Afya ya Sikio kutoka *Tanzania Society for the Deaf* (uziwi), wakiongozwa na Mkurugenzi Yassin Mawe. Hawa ndiyo wataalam wetu wa kuchunguza masikio ya Waheshimiwa Wabunge, karibuni sana. Baadaye mtanipa taarifa mmepata wagonjwa wangapi na matatizo ambayo wanayo. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Sima, ajandae Mheshimiwa Stephen Masele

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu lakini nipongeze sana Wizara, Waziri na Naibu wake kwa kutuletea bajeti nzuri ambayo inajali maisha ya Watanzania wa hali ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli ameonsha dhamira yake ya dhati ya kuwatumikia Watanzania. Nimpe moyo tu hata Mitume nao wakati wanakuja walitokea watu ambao hawakuwanga mkono lakini leo bado tunaendelea kuwaabudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ni nzuri sana, kwa kweli inatufanya tutembeke kifuu mbele. Yako mambo machache ambayo nami napenda niyazungumzie. Nianze na eneo ambalo bajeti imelizungumzia na nipongeze sana Wizara kwa kuondoa kodi kwenye mazao ya biashara na kilimo. Kwenye eneo hili yametajwa mazao hapa kama vile chai, pamba na mengine lakini alizeti halijaangaliwa na Mkoa wa Singida sisi ni maarufu sana na ndiyo waasisi wa zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza nini hapa? Takwimu inatuambia Tanzania tunatumia karibu tani

laki nne za mafuta, lakini tani laki mbili na themanini ni (*importation*) yanatoka nje, *palm oil* zinazobaki ndizo tani ambazo sisi tunatumia kama laki moja na ishirini. Serikali leo tunazungumza kuwekeza katika viwanda vyetu vya ndani na lazima tujikite katika kuwakomboa wakulima wetu na ni lazima tuhakikishe kwamba mazao ya kwetu tunayapa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkulima akilima alizeti yake akishaisindika tu maana yake analipa VAT asilimia 18. Huyu huyo mkulima tunamtarajia aende akaongeze angalau heka moja, mbili hawezi, matokeo yake wakulima wote wa alizeti wanaiuza alizeti ikiwa shambani, ndiyo maana uzalishaji unakuwa mdogo. Mafuta ya alizeti tukiyaangalia na ndiyo mafuta bora yana *cholesterol* ndogo ya asilimia 17 kulinganisha na mafuta mengine yote ambayo yana zaidi ya *cholesterol* asilimia 60. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta yanayoagizwa nje ni asilimia 70, yanayobaki ni asilimia 30 mafuta yetu ya ndani. Sasa kama Serikali ina lengo la ku-*promote* tuweze kutumia mafuta yetu ya ndani hasa alizeti tulikuwa na kila sababu ya kuhakikisha tunaondoa hii kodi ya VAT. Serikali imeongeza asilimia 10 kwenye *importation* ya mafuta yanayotoka nje, mwenzangu aliyepita amesema iongezwe iwekwe hata asilimia 15 na mimi namuunga mkono kwenye hilo, kwa sababu kama tuna lengo la kulinda viwanda vyetu vya ndani basi niombe Serikali iondoe kodi hii ya asilimia kumi na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwomb sana Mheshimiwa Waziri, sisi tunaotoka kwenye maeneo haya alizeti ndiyo zao kuu Mkoa wa Singida ambalo uzalishaji wake unashuka kila kukicha, kwa sababu wametuwekea VAT bila sababu ya msingi. Mwaka 2010 tulikuwa na *zero rate* lakini tumekwenda mwaka 2014 wametuwekea VAT lakini hakuna sababu ya msingi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri awajali wakulima hawa wa zao hili la alizeti ili tuweze kuwasaidia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale Singida tunalima sana kitunguu na kitunguu bora kinatoka Singida. Wakati nauliza swali mwanzoni Serikali iliji-*commit* kwamba itakwenda kutujengea soko la kisasa la vitunguu. Sisi tumekwisha tanga eneo na Mheshimiwa Rais alianza ziara yake ya kwanza Mkoa wa Singida namshukuru sana na katika ziara ile aliwaahidi Wanasingida kwamba sasa anahitaji vile vitunguu tuweze kufanya *packing* pale pale Mkoani Singida badala ya kubeba kitunguu kikiwa *raw* kiende kufanyiwa *packing* Kenya na maeneo mengine. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, tumeshaandaa eneo, tuna vitunguu vya kutosha, waje mtusaidie kujenga lile soko liwe soko la kisasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali imewatambua wafanyabiashara wadogo wadogo, mama lishe, Wamachinga na wengine. Hata hivyo, nilikuwa najaribu kuangalia hawa bodaboda na bajaji ni wafanyabiashara wa namna gani? Mkoa wa Singida hususan Singida Mjini tunao vijana wengi sana na eneo hili la usafirishaji wameturahisishia sana sisi, lakini jambo la kushangaza, Mheshimiwa Waziri vijana wangu leo wanatozwa (*income tax*) kodi ya mapato ya Sh.150,000/= kwa mwaka bila sababu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naanza kulalamika kwa nini wanatozwa nilimwandikia barua Meneja wa *TRA*, nashukuru sana kijana yule ni msikivu, lakini ananijibu kwa pikipiki moja bwana tutaacha lakini mmiliki wa pikipiki mbili atalipa Sh.150,000, tunakwenda wapi? Tunataka vijana hao wajajiri na ajira Serikalini hamna, sasa leo kama watalipa *income tax* maana yake vijana wale watafanya kazi usiku, madhara ya usiku tunayajua, akishindwa kupata fedha ya kununua mafuta maana yake ataanza kufanya shughuli nyingine. Naomba tusiwaweke kwenye majaribu, Mheshimiwa Waziri hili ni eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sheria ya Mapato mwaka 2014 ya kukusanya kila mahali sidhani kama ina tija kwa vijana wa bodaboda. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri

vijana wangu pale mjini wako wengi, wamejiajiri na mimi ni sehemu ya shughuli zao na mimi ni mlezi wa eneo lao, niombe sana hili eneo kwa kweli kwangu wanatozwa Sh.150,000/= bodaboda na bajaji, hebu tuiondoe kodi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie eneo lingine la maji. Nami niungane na wenzangu kwa kuongeza Sh.50/= kwenye maji lakini tunayo miradi ya vijiji 10 ambayo imekuja Singida lakini utekelezaji wake ni hafifu sana. Niombe eneo hili pia mtaenda kuliangalia kwa sababu ya muda nisieleze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kwenye milioni 50, kila Mbunge anasimama na vitabu vinaandika milioni 50 kila kijiji. Mheshimiwa Waziri hebu tuliweke vizuri hili sisi wengine tuna mitaa, sasa ukizungumza milioni 50 kila kijiji, mimi naenda kusimama naambiwa naletewa milioni 50 na sheria imekuja inasema milioni 50 kila kijiji, mitaa haipo. Naomba tuiweke vizuri wala hapa hakuna mgogoro, tuweke milioni 50 kila kijiji na kila mtaa ili wananchi wangu kote wapate, kwa sababu hii *categorization* ya vijiji na mtaa ni ya Kiserikali wala siyo ya kwetu, Watanzania ni wale wale tu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hili pia nalo aliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *REA*, tunazungumzia umeme vijijini. Sisi tunaishi mjini maana yake ni kama unaambiwa wewe unaishi mjini umeme hauwezi kuja. Mimi nina vijiji 20 na mitaa havina umeme, Mheshimiwa Waziri hebu na jambo hili tuliangalie, tutazungumza lugha gani? Kama tunasema Serikali inaleta umeme lakini umeme unakwenda vijijini sisi tunaishi mjini, hatukuzaliwa kuishi mjini ili tukose hizi fursa ambazo Serikali inazitoa, wote tunaishi maisha sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni lazima Wizara iliangalie vizuri ituletee umeme, tusiwe watu wa kulalamika kwenye maeneo haya. Kama wenzetu wanapata umeme na sisi tupate umeme bila kujali vijijini wala mjini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida una rasilimali ya madini, eneo la Singida Mashariki, Singida Magharibi hali kadhalika Iramba kuna madini. Wako wawekezaji wanaitwa *Shanta Gold Mine*, wananchi kwa ridhaa yao wamepisha eneo lakini hawajalipwa fidia. Bahati mbaya sana kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu hili hakuliona lakini naomba mimi niliseme kwa sababu mimi naishi mjini nahitaji waje wawekeze mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wale wawekezaji, *Shanta Gold Mine* sasa wana miaka mingi, wananchi wangu sasa wamebaki kuvamia kuanza kuchimbachimba kidogo kidogo yale madini yako ya kutosha, wanahitaji kulipwa fidia na ule uchimbaji uweze kuonekana. Mheshimiwa Rais keshatuonyesha njia sasa hatuna sababu ya kurudi nyuma. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel, ajiandae Mheshimwa Stephen Masele.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwepo hapa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri na hasa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake. Nimpongeze sana pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa mshauri mzuri kwa Waziri na hatimaye kutuletea bajeti yenye tija na inayojali maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kondo a wana msem o usemao kwamba *mwana wa mukiva amanyire michungiro*. Usemi huu una maana kubwa sana na ndiyo maana nikampongeza Naibu Waziri kwa sababu ya ushauri wake mzuri na kuweza kumsaidia majukumu Mheshimiwa Waziri na hatimaye tumeletewa bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze sana Serikali kwa hatua zake katika kujali maslahi ya kundi la watu wenye ulemavu. Kubwa zaidi niipongeze Serikali, kuondoa kodi katika vifaa vya watu wenye ulemavu, ukurasa wa 71. Vifaa hivi ni muhimu sana. Vifaa hivi ndivyo vinavyowasaidia watu wenye ulemavu kuweza kutekeleza majukumu yao lakini pia ni sawa na miguu au mikono ya watu wengine ambayo wamepewa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, kwa kitendo hiki cha kuondoa kodi katika vifaa vya watu wenye ulemavu ni faraja kubwa sana kwa sababu hivi sasa vifaa hivi vitakuwa na bei angalau afadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, *calipers* ambazo zimekuwa zikitumiwa na watu wenye ulemavu zinafika kwenye Sh.400,000/= mpaka Sh.500,000/= lakini nina matarajio makubwa sana kwamba baada ya kuondolewa ushuru wa kodi kwa vifaa hivi, basi vitapungua na walemavu wengi wataweza ku-*afford* vifaa hivi. (*Makofi*)

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuchangia, *calipers* sasa hivi zinazwa kwa Sh.1,500,000/= mpaka Sh.1,900,000/= bei ambayo nilipewa mwezi February. Ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, taarifa hiyo.



**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na kwa sababu mwenzangu amekuwa akitumia sana vifaa hivi, kwa hiyo, anachokizungumza anakifahamu kwa undani zaidi. Kwa hiyo, niungane naye tu katika kuipongeza Serikali kwa maana kwamba sasa hiyo gharama ambayo imekuwa ikitozwa itapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika Hospitali ya CCBRT, Hospitali ya KCMC lakini pia Hospitali ya Seliani ambazo zimekuwa zikihudumia sana watu wenye ulemavu, naamini kabisa kwamba msamaha huu wa kodi uwatawasaidia. Kwa maana hiyo pia tutaweza kuboresha hospitali yetu ya Muhimbili ili basi na wenyewe waweze kuboresha zaidi kitengo hiki cha huduma ya vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza kwa moyo wa dhati kabisa Serikali na niendeleo tu kuipongeza Wizara, Mama yangu Ndalichako, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye pia hivi karibuni alipokea vifaa vya watu wenye ulemavu ambavyo vimesambazwa katika shule na vyo mbalimbali. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba Serikali hii imekuwa ikijali maslahi na kuangalia kundi hili la watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi na kuishukuru Serikali, nitoe tu pia ushauri kwa Serikali kwa sababu kuhusu Kitabu hiki cha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016. Pamoja na kwamba tumepunguza kodi lakini bado kuna mahitaji mengi ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, ni vyema katika bajeti ijayo tuone ni kwa jinsi gani tutasaidia zaidi kundi hili. Kwa mfano, maisha ya watu wenye ulemavu ni ya chini sana na hasa maeneo mengi ya vijijini hali zao za kiuchumi ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokuja na bajeti tuone kundi hili tunaliangalia vipi? Kwa mfano, kwa hivi sasa tulipo katika Sera ya Serikali katika kuhakikisha

kwamba inajikita zaidi katika viwanda, pia tuangalie hivyo viwanda ni kwa jinsi gani vitaweza kutoa ajira kwa watu wenye ulemavu, kuwasaidia na hali ngumu au maisha magumu waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambapo nilizungumza kwa undani zaidi na nimekuwa nikilipigia sana kelele suala la *TBC* kutokana na uchakavu wa mitambo. Kwa sababu ni Serikali sikivu Mheshimiwa Rais alifanya ziara katika shirika hili na kujionea hali jinsi ilivyo lakini pia akaweza kutatua baadhi ya changamoto zilizopo katika shirika hili, nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote haya, sasa ni wakati muafaka kabisa kwa wafanyakazi na watumishi wote wa Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) kutoa ushirikiano, kufanya kazi kwa bidii katika kuhakikisha kwamba shirika hili linarudi katika hali yake iliyokuwepo hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri aliyofanya ambayo hivi sasa Afrika inafahamu kwamba Tanzania inaye Rais anayeitwa Dokta John Pombe Magufuli. Kitendo alichokifanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kitendo cha kuungwa mkono na Watanzania wote, ni kitendo cha kuungwa mkono na wale wote wapenda maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu mimi katika kundi ninaloliwakilisha na naomba nijikite kulizungumzia hili, ni watu wenye maisha duni sana. Rasilimali hizi zikitumika ipasavyo ni dhahiri kabisa kwamba tutatatua changamoto nyingi za watu wenye ulemavu na kupunguza ukali wa maisha waliyonayo. Kwa maana hiyo, naomba sana nimpongeze Rais. Pia naamini kwanza ni fundisho ambalo tumejifunza lakini pia tutakuwa makini katika kupitisha mikataba ili mikataba hiyo isije ikatufunga sisi na ikatumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hivyo pia, ni wakati muafaka sasa na ningemwomba Mheshimiwa Rais aangalie mkataba na mwekezaji wa Pori la Loliondo ambao kwa muda mrefu umekuwa ni mgogoro unaomiza ndugu zangu wa jamii ya Kimasai. Kwa hiyo, namwomba pia kuangalia ni kwa jinsi gani watapitia mkataba huu ili kama kuna vipengele ambavyo vinawabana au vinawaumiza wananchi vifanyiwe marekebicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia ambalo napenda kuishauri Serikali, kwanza nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kuunda Kamati kupitia Mkataba wa *Sky Associate* pamoja na *State Mining Companies Limited (STAMICO)* ili kuweza kurekebisha upungufu uliopo. Kabla Mkoa wa Manyara haujagawanywa madini haya yalikuwa ndani ya Mkoa wa Arusha na nafahamu kabisa ni kwa jinsi gani yamekuwa yakisaidia wakazi wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ukienda hali ni ngumu sana kwa vijana wengi ambao walizoea kuchimba madini haya na kujipatia kipato, hali imekuwa tofauti. Kwa hiyo, kwa kitendo hiki cha Mheshimiwa Spika kuunda hii Kamati kupitia mkataba huu, ni faraja kubwa na naamini kabisa sasa mikataba hii itaangalia ni kwa jinsi gani itakwenda kuwanufaisha wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishauri Serikali katika Halmashauri na Mikoa yetu kuangalia kwa mfano, ndiyo, tumepunguza kodi katika vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu lakini tunawaandalia mazingira gani mazuri ya kuwawezesha watu hawa kufanya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stephen Masele, ajiandae Mheshimiwa Dokta Christine Ishengoma.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Serikali. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dokta Mpango, ama kweli ameonsha uwezo wake kwamba yeye ni mchumi aliyebobea kwa kutuletea bajeti ambayo kwa kweli imeandaliwa kisayansi sana. Pia nipongeze sana timu yake yote ya watendaji, ikiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Dotto James na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ya kutengeneza bajeti ambayo inatoa majawabu ya matatizo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasiasa na watu mbalimbali wamekuwa wakisema Serikali haisikilizi ushauri, Serikali haishauriwi, lakini nimesoma bajeti hii mambo mengi ambayo wananchi na Wabunge wamekuwa wakishauri yamezingatiwa. Kwa kweli, naomba sasa Mheshimiwa Mpango na timu yake waharakishe utekelezaji wa maamuzi ya kiseru waliyoyafanya. Wamepunguza ushuru kwenye baadhi ya maeneo hasa kwenye mazao kwenye Halmashauri na wametoa maelekezo kwa TRA ifanye kazi bila kubughudhi wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Shinyanga, Shinyanga tuna wafanyabiashara wadogowadogo na wakubwa, wafanyabiashara wanasumbuliwa, wanafuatwa na Polisi, wanafuatwa na PCCB. Maelekezo aheshimiwa Mpango naomba ayapeleke kule chini na ayasimamie kuhakikisha wafanyabiashara wanapewa mazingira wezeshi ili waweze kuzalisha na hatimaye Serikali iweze kupata kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia huu ushuru wa mama-ntilie, mama-lishe, wakulima wadogo wadogo wa bustani, yote ambayo wamepunguza maelekezo yaende kwenye Halmashauri zetu. Hatuwezi kujenga Taifa hili kwa kutegemea ushuru wa mama-lishe au wa mama anayeza

mboga. Kwa hiyo, nina imani na kazi yake, nina imani na uwezo wake, naamini atayazingatia haya na atapeleka maelekezo kwenye ngazi za chini za wananchi ili wasiweze kusumbuliwa na wananchi wangu wa Soko la Nguzo Nane kule Kamarage, Soko Kuu la Shinyanga waweze kufanya biashara zao bila kusumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wiki nzima hii nchi yetu imekuwa inazungumzia suala la mchanga wa dhahabu. Mimi nimewahi kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kama kuna vita yoyote duniani hivi leo ni vita ya uchumi. Yale yote mnayoyaona yanatokea Syria, watu wengi hawaelewi Syria ni nini kinatokea, pale kuna gesi ya Qatar inazalishwa na Wamarekani wanataka kusafirisha kwenda Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urusi ndiye muuzaji wa gesi mkubwa Ulaya, Marekani na Qatar wanataka wajenge bomba la gesi lipite Syria liende Ulaya, Urusi hataki lijengwe litaharibu soko lake, anamwambia Assad weka ngumu, hakuna bomba kupita mimi nitakusaidia. Marekani na yenyewe inaingiza nguvu zake kumng'oa Assad. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, tunapozungumzia masuala ya uchumi ni mazito na yanaingilia hadi na Mataifa. Leo hii Tanzania tumetoa maamuzi haya, Mataifa ya kibeberu na kibepari yatataka kutuingilia ndani. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa maamuzi aliyoyafanya kwa sababu atakumbana na vikwazo mbalimbali vingi na ili Taifa letu liendelee ni lazima tuwe na utulivu wa kisiasa, lazima wananchi tutulie na tuelewe nini tunataka kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unapata tabu Watanzania wanalalamika tunanyonywa, tunaibiwa, unapochukua maamuzi ya kudhibiti kunyonywa na kuibiwa ndipo watu wanaanza kugeuka tena. Mtu anaanza kusema ooh, kwa nini mnafanya hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa Naibu Waziri niliwahi kutoa tamko hapa Bungeni, nilitegemea Watanzania wenzangu na Wabunge wenzangu asilimia kubwa waunge mkono unyonyaji na unyanyasaji tuliokuwa tunafanyiwa na Mataifa ya kibeberu, lakini Wabunge wengine humu wakasimama kuanza kutetea mabeberu. Tulikuwa tunajenga bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar-es-Salaam kuongeza uwezo...

### TAARIFA

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili jambo liwe *clear* kwenye *statement* hapa ambazo watu wanatoa, hakuna Mbunge anayepinga wala anayesema tuendeleo kuibiwa. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Wapo.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Sisi wengine tunatoka kwenye maeneo yenye migodi na waliohusika wengine ndiyo hao wanaozungumza hapa.

**WABUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Watu wetu wameuawa, kwa hiyo, wasitu-*provoke* hapa. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, nimeruhusu taarifa moja tu. Mheshimiwa Masele, unaikubali taarifa?

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimsaidie rafiki yangu Mheshimiwa Heche. Cha kwanza jana kuna mtu amesema hapa ripoti ile ni *rubbish*.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hauwezi ukapinga ripoti ya kitaalam na ya kisayansi kwa maneno, unaipinga ripoti ya kisayansi kwa kuja na ripoti ku-counter ripoti iliyotolewa. (*Makofi*)

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimwambie...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu uliobaki ni mdogo sana, taarifa nimeuruhusu Mheshimiwa Heche, sasa Mheshimiwa Masele endelea. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine humu tumeshakuwa wakongwe. Nataka nimwambie mimi nikiwa Naibu Waziri, Halmashauri zote zenye migodi Tanzania zilikuwa zinalipwa dola laki moja, dola laki mbili. Nilisimamia kuhakikisha kwamba tunafuata sheria za nchi ambapo Halmashauri zetu zinapata asilimia 0.3 ya *turn over* ya migodi hii, leo Halmashauri ya Geita inapata zaidi ya bilioni tatu kwa mwaka, ilikuwa inapata dola laki mbili tu. Haya mambo yanawezekana, tukiwabana wawekezaji wanaonyonya kwa mikataba nyonyaji tunaweza kufanikiwa kupata mapato zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufanye *radical decisions*, hatuwezi tukakaa mezani tunachekeana tukitaka kupata mapato zaidi. Nchi za Afrika zinatia huruma, ukienda Kongo pale, leo Kongo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Wewe endelea tu.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kongo pale thamani ya madini ya Kongo kwa

takwimu inaonesha ina thamani zaidi ya *GDP* ya *European Union* lakini Kongo inaibiwa, watu wamekaa, wananchi wana shida. Leo Tanzania tumeweka mfano, Tanzania tumeset *standard* na wote tunatakiwa tumuunge mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoka kwenye Vikao vya Bunge la Afrika, nchi nyingine za Afrika zinatuliza, zinatusifia, zinamsifia Rais wetu na zina hamu aende akashiriki kwenye mikutano ya kimataifa ili waweze kujifunza nini anafanya Tanzania. Kwa hiyo, ndugu zangu nataka niwaambie muda wa kunyosheana vidole huyu kafanya nini, kafanya nini, utatupotezea muda kama Waheshimiwa Wabunge, ni vyema Waheshimiwa Wabunge tuanze kufikiria mapendekezo, maoni ambayo yataboresha ile *task force* iliyoundwa na Mheshimiwa Rais ya kuboresha mikataba hii. Kama una maoni mazuri yaandike yapeleke kwa Mheshimiwa Profesa Kabudi ili aweze kuyaingiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mikoa yote yenye rasilimali haipati chochote, pelekeni mapendekezo angalau asilimia moja kinachovunwa kibaki kwenye mikoa husika ili maisha ya wananchi yafanane na rasilimali zao. Leo ukienda Geita maisha ya wananchi hayafanani na rasilimali zao. Ukienda Shinyanga almasi ile, maisha ya watu wa Kishapu na Shinyanga hayafanani. Ni lazima Serikali iamue kwa makusudi asilimia moja ama asilimia yoyote ambayo itaonekana kitaalam ibaki kwenye maeneo ya wananchi ili kuboresha maisha yao yafanane na rasilimali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na nimshukuru Mheshimiwa Rais amelianshiza jambo, amelisimamia, amelifikisha mwisho. Kitendo cha watu wa *ACACIA* kuja kukaa naye mezani maana yake sasa tunapata muafaka wa matatizo tuliyokuwanayo. Unaweza ukalianzisha jambo na usiweze kulisimamia, unaweza ukalianzisha jambo na usiweze kulifikisha mwisho, lakini tuna Rais ambaye ni mtendaji, mtekelezaji, analianshiza jambo, analisimamia na analifikisha mwisho. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tumuunge mkono na tusimamie na tutambue kwamba hii vita tunayopigana siyo vita ndogo. Siyo vita ndogo kuanzia kwa makampuni, siyo vita ndogo kuanzia kwa Mataifa ya kibeberu kwa sababu kazi yao iliyobakia ni kunyonya rasilimali za Afrika. Wanakuja na mbinu mbalimbali lakini Waafrika lazima tusimame tuoneshe mfano na Tanzania imeonesha mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ishengoma, ajjandae Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Serikali. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia afya na kuweza kuchangia kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa sana anayoifanya. Kwa kweli, ni mtu anayestahili kufanya mambo anayoyafanya. Mheshimiwa Rais akisema anatenda, Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi kwa muda wa miezi 18 tu. Mheshimiwa Rais kwa kweli, kila mmoja anastahili kumpongeza kwa mambo yote anayowafanyia Watanzania. Amejitoa yeye mwenyewe na siyo yeye mwenyewe ni mkono wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana na namwombea Mwenyezi Mungu azidi kumlinda na azidi kumwongoza aweze kuishi maisha marefu. Hasa tendo hili la makinikia na kweli amelifanyia mambo mazuri, wengine wameanzisha lakini yeye mwenyewe nadhani atamalizia. Sasa hivi akikaa hivi karibuni mezani na hawa watu, fedha

zitakuja, kila mmoja atatamani kuzitumia kwenye miradi yake. Kwa hiyo, naomba wote tuwe kitu kimoja, nchi yetu ni nzuri, nchi yetu ya Tanzania ina amani, naomba tuwe kitu kimoja hasa kushughulikia mambo haya yaliyo mbele yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Makatibu wa Fedha na Manaibu wake. Kwa kweli, bajeti hii ni nzuri sana, inawajali Watanzania, inawajali wakulima...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge, *please*.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Inawajali watu wote kwa wastani. Kwa hiyo, tunashukuru kwa bajeti hii nzuri ambayo mmetuelelea ya shilingi trilioni 31.7 na kati ya hizo wamesema asilimia 38 ni fedha za maendeleo. Naomba hizi fedha za maendeleo ziweze kuja zote kama walivyozipanga kusudi miradi ya maendeleo ile ambayo ni viporo na ile ambayo bado iweze kutekelezeka. Kwa hiyo, naomba kitu kama hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kati kwa ujenzi wa *standard gauge*, tunashukuru sana imeanza na wakandarasi wako tayari pale na itajengwa kwani tayari mkataba umeshawekwa saini ya kutoka Dar-es-Salaam mpaka Morogoro. Wamesema bado mnatafuta wafadhili kwa reli kuanzia Morogoro – Makutupora – Kigoma - Mwanza, naomba wafanye bidii sana kwa sababu reli hii inawasaidia watu wote. Reli hii haitachagua chama gani itawabeba watu wote wa kanda hizo hizo, kwa hiyo, naomba Serikali waifanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kuliongelea ni tatizo la maji, kila mmoja humu anazungumzia tatizo la maji.

## TAARIFA

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge ambaye anaongea ambaye amesema kwamba anampongeza Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya takriban miezi kumi na nane ambayo ni sawa na miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa kwamba Mheshimiwa Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi ambaye alikuwa Rais wa Awamu ya Pili alikiri kwa kinywa chake kwamba kazi ambayo Mheshimiwa Magufuli ameifanya kwa mwaka mmoja ni sawasawa na miaka 30. Kwa kuwa muda alioutaja Mheshimiwa Mbunge ni takriban miaka miwili maana yake kwa kauli ya Mheshimiwa Mwinyi ni sawasawa na miaka 60. Kwa hiyo, naomba nimpe taarifa hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu hata Mheshimwa Lowassa na yeye amemkubali Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia tatizo la maji, uwe Mbunge wa chama chochote kila mmoja anakiri kuwa ana tatizo la maji. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema kuja kufikia mwaka 2020 asilimia 85 vijijini wawe wamepata maji safi na salama na asilimia 95 mijini nao wawe wamepata maji safi na salama ili kusudi tuweze kuwatua ndoo kichwani wanawake. Kwa hiyo, naomba sana tena sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha hii ahadi iweze kutimilika maji yaweze kwenda vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana kwa kufuta leseni ya magari. Hii bajeti imepokelewa na watu wengi...

### TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii ni ya mwisho.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpe taarifa mama pale kwa sababu...

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana utamwita jina lake la Kibunge.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Ishengoma kwamba Mheshimiwa Lowassa hajamkubali Magufuli ila alichokifanya ametoa taarifa kwamba Serikali ya CCM na sera zake ndizo zilizouza madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siikubali hiyo taarifa, kama hajui kusoma aende akasome aangalie ni kitu gani kinatendeka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia kufutwa kwa leseni ya magari. Nendeni kwenye mitandao ongea na watu wote, ongea na wasomi, ongea na kila mmoja, hii kweli anaiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kutoa ushuru wa Sh.40/= kwa kila lita ya mafuta...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tena upande huu, naona zogo limezidi huku na nitaanza kutaja majina.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha hizi hela ziweze kwenda kwenye Mfuko wa Maji. Nikiwa mwanamke nasisitiza hilo kwa sababu najua shida ya wanawake ambao wanatafuta maji pamoja na watoto wao, hizi hela ziweze kwenda kwenye Mfuko wa Maji. Nasisitiza kuwa asilimia 30 ya hizi fedha ziweze kwenda mjini pamoja na asilimia 70 ziende vijiji. Nasema hivi kwa sababu mjini inaweza kutokea taasisi zingine zikasaidia kugharamia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, asilimia 65 ya wananchi wanategemea kilimo na malighafi nyingi zinatoka kwenye kilimo. Kwa hiyo, namwomba sana sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fedha zilizotengwa kwenye kilimo ahakikishe zote zinakwenda kwenye kilimo kwa sababu bila ya kilimo hakuna viwanda, chakula na lishe ni duni. Kwa hiyo, naomba sana hizi hela ziweze kutoka zote tuweze kuinua pato la familia pamoja na pato la Taifa na hasa tukazanie kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa sababu wameweza kutoa tozo mbalimbali kwenye pembejeo na ushuru wa mazao asilimia tatu kwa bidhaa za biashara na asilimia tatu kwa bidhaa za chakula. Hata hivyo, katika mikoa mingine, kwa mfano, Morogoro tunalima mahindi, mpunga na viazi yote yanafanana ni biashara pamoja na chakula. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri tozo iwe moja kwa zao moja, iweze kufanana kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tani moja ambayo wamesema kuwa kama unasafirisha kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine ushuru umefutwa. Mheshimiwa Waziri akija kuwa-*wind up* hapo aweze kulifafanua kwa sababu kuna wakulima wengine kwa mfano nakaa Manispaa ya Morogoro lakini nalima Halmashauri ya Morogoro Vijijini na ukisema tani ni magunia kumi, magunia kumi kwa wakulima wa kisasa wanavuna mpaka magunia

ishirini, je, tozo itakuwaje na mimi ni mkulima siyo mfanyabiashara, nimevuna magunia yangu ishirini utanitoza ushuru? Naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie kusudi aweze kutushauri vizuri kama ushuru utakuwepo au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye ufugaji, wafugaji kusamehewa malighafi ambayo inatengeneza chakula cha kuku, naishukuru sana Serikali na naipa pongezi. Wananchi wote ambao wanafuga kuku na hasa wanawake itawasaidia sana katika kufuga kuku na itasaidia kuongeza kipato, lishe pamoja na ajira hasa kwa vijana ambao wanamaliza shule na hawana kazi. Ushauri wangu, naomba waangalie mazingira mazuri ya kukopa na hasa Benki ya Kilimo pamoja na Dirisha la *TIB*, hela zote hizo walizozitenga ziweze kutolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mayai yanayototoleshwa na yenyewe inasaidia sana wafugaji. Wale wafugaji vifaranga vilikuwa bei ya juu sasa kwa kufanya hivyo bei ya vifaranga itapungua na gharama pia itapungua, pato litapanda na lishe pia litapanda. Ushauri wangu ni kama huo huo waangalie mazingira mazuri ya ukopaji na hasa Benki ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea kuhusu shamba la kilimo Mkulazi na Mbigiri ambayo tayari yako kwenye mchakato wa kujenga viwanda vya sukari na kilimo cha sukari. Nashauri waangalie *out growers*, hawa wakulima wetu wa Morogoro ambao wanazunguka mashamba hayo watafaidikaje? Naomba waangalie kusudi na wenyewe waweze kuwa kwenye mpango wa kupata na ajira itaongeze kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato, kwa kweli nashukuru kuwa Sh.10,000/= ambayo wameiweka kwenye nyumba ambayo haijathaminishwa pamoja na Sh.50,000/= kwa nyumba ya ghorofa itasaidia kuongeza mapato yetu na hasa mapato ya ndani ambapo itasaidia kufanya mipango yetu ya maendeleo. Ila Mheshimiwa Waziri kama

maswali yalivyokuwa yanaulizwa akija ku-*wind-up* aelezee kuwa tumeanza na hizi za Manispaa na Halmashauri ni lini na ni nyumba ya aina gani ambayo itatozwa Sh.10,000/= kama Wabunge wenzangu walivyouliza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Rwakatare, ajiandae Bhagwanji Meisuria.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Pia nashukuru kwa kazi yako nzuri sana ya kiwango unayoifanya, Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa zawadi adimu ya Rais wetu wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa kweli Rais Magufuli anastahili pongezi za dhati. Kama mtu haoni alichokifanya basi hana macho, huyu ni kipofu. Kama kweli yeye ni Mtanzania anasimama hapa siku zote anapinga ufsadi, anapinga mambo mabaya, halafu tena haoni alichokifanya, basi huyu mtu siyo Mtanzania halisi anajifanya tu. Inabidi tumwombe Rais wetu kwa hali na mali. Katika Isaya 54:17, unasema; kila silaha itakayoinuka juu yake isifanikiwe kwa Jina la Yesu. Kila ulimi utakaosimama kumpinga, tunaupinga wenyewe kwa Jina la Yesu.

**WABUNGE FULANI:** Ameen, Haleluya.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa fupi Jumapili ni lbada Maalum ya kumwombea Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, kuombea

Taifa letu na Bunge letu. Tutakuwa Mikocheni B, Kanisa la Mlima wa Moto, njooni jamani tukutane na Mungu aliye hai.

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanabisha, wanapinga...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**MWENYEKITI:** Kaa chini, kaa chini, kaa chini.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Hata kama unabisha lakini Mzungu si mmemwona, Mzungu si amekuja, amekuja mwenyewe... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Bila kuitwa.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Ndiyo, bila kuitwa kwa tiketi yake. Amesema amekuja na ndege yake mwenyewe.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Taarifa tafadhali Mheshimiwa.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Sasa kama amekuja kukubali yaishe kuna ubaya gani?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna. (*Makofi*)

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Si lazima tujipongeze. Hata kwa yale mazuri jamani pia tunapingana kwa vipi? Amekutana Ikulu, kumbe ulitaka akutane naye wapi Feri, Kariakoo au Buguruni au wapi? Nyumbani kwake si Ikulu amekutana naye, ni vizuri na wote tunashukuru, Mungu amejibu maombi.

**WABUNGE FULANI:** Ameen. (*Makofi*)



**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Waseme wasiseme lakini hata nchi jirani wote wanasema, wanatupigia simu hongereni Tanzania, hongereni kwa kazi nzuri, hongereni kwa Rais mzuri. Kwa hiyo, lazima tumpongeze sana, amejitahidi kwa muda mfupi kaondoa wafanyakazi hewa, amegundua makontena ya mafisadi, amenunua ndege, amejenga barabara na kadhalka, si lazima tumshukuru. Mnataka nini jamani gunia la chawa au awabebe mgongoni? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa vifaa tiba Wilaya zote na *ambulance* amejitahidi kama mwanadamu. Elimu bure, jamani kazi alizofanya ni kama miaka 60, mimi naongeza na 30 kama miaka 90, Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye bajeti yetu, napenda kuipongeza bajeti kuu ya Wizara ya Fedha chini ya Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu Waziri wake, kwa kweli ni bajeti ya kihistoria iliyoacha simulizi mitaani. Ni bajeti iliyomjali hata mtu wa chini, mnyonge hadi mama lische hadi mfanyakabiashara ndogo ndogo, wote wameguswa. Nje wenzetu wanafurahia lakini hapa ndani watu wanabisha. Sasa walengwa wamefurahia lakini wewe kwa sababu siyo mlengwa ndiyo maana hata wala huoni umuhimu wake, pole. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama jinsi alivyoweza kufuta *road licence*, tazama jinsi ilivyoweza kupunguza kodi mbalimbali yaani ili mradi wamefanya walichoweza. Jamani kuna mabadiliko mabwa mwaka huu. Watu wanasema ni mwaka wa neema, ni bajeti ya neema wamefanya kile ambacho walichoweza kufanya, lazima tuwapongeze. Mheshimiwa Dkt. Mpango hongera sana, pongezi nyingi na mama pale, pongezi nyingi na Wizara nzima kwa kazi nzuri na mabadiliko makubwa waliyoyaleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie jambo moja ambalo ni kodi kwa ajili ya shule binafsi nikisema

kwamba mimi pia ni mdau mmojawapo, na- *declare interest*. Mheshimiwa Waziri Dokta Mpango kodi katika shule binafsi zimezidi. Kuna kodi zaidi ya 25, mpaka unashangaa sisi nasi tunachima madini au nini, wakati sisi tunafundisha watoto wenu. Waangalieni sana kodi ni nyingi hata akikaa na timu yake ingetakiwa wafute kodi zote katika shule kwa sababu shule ni huduma siyo biashara na huduma tunazofanya ni kwa faida ya Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa walikuwa wanakwenda Kenya, Uganda na nchi nyingine za jirani lakini sisi tumefanya hawa watoto wasome Tanzania, waweze kujifunza historia yao, wajifunze jiografia yao, wajue viongozi wao, lakini zamani walivyokuwa wanakwenda nchi jirani utakuta akiulizwa wewe Rais wako nani, inabidi aseme Uhuru Kenyatta. Kwa sababu akisema mimi Rais wangu Dokta John Pombe Magufuli atakoseshwa, japo yeye ni Mtanzania yuko nchi ya kigeni, lakini sisi tumeleta fikra za watoto kubadilika kwa kusoma wakiwa wadogo ndani ya nchi baadaye wakiwa wakubwa ndiyo waende siyo mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi mtusaidie yaani jamani tunachajiwa hata majengo, tunaambiwa *property tax*, hasa yale majengo si ya shule, si watoto wenu ndiyo wanasoma? Mbona shule za Serikali hawatozi kwa nini sisi tu ndiyo mtutoze? Unaambiwa hata vile viwanja tumejenga shule wanakuambia bwana lazima ulipe kodi kama vile kiwanja cha biashara yaani kama kiwanja umefanyia biashara kubwa fulani. Hakika wakitusaidia katika hilo itakuwa ni unafuu kwa ajili yetu na hata kwa ajili ya watoto wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiangalia wenyewe ile karo tunayotoa ni ndogo mno. Watoto hawa wanakunywa chai asubuhi, saa nne wanakunywa tena na wenzao wa *day scholars*, mchana wanakula chakula, jioni wale *boarders* wanakula mlo kamili, sasa hivi vyakula vyote ni gharama. Vilevile wanapewa magodoro na vitanda, wana *matron* na *patron* wanaowalinda, kuna daktari na manesi

wanaowatunza watoto wetu ili wakae vizuri. Waangalie watuhurumie, watusaidie tufanye kazi pamoja kwa sababu hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE J. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria, ajiandae Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Mungu akuweke. Nimepata nafasi hii kuzungumzia bajeti yetu ya Serikali. Nataka niseme sisi Wabunge wote hakuna ubaguzi wa rangi wala Kabila tunaunga mkono bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake. Hicho kitabu alichandika cha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, namuunga mkono, Mungu amweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana sana Mheshimiwa Rais wetu Dokta John Pombe Magufuli, amefanya kazi nzuri, kwa sababu tulikuwa tunadhulumiwa madini yetu yanakwenda nje. Mungu ameweka neema yake awamu yake akafanya vizuri na anasaidia kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu Magufuli amefanya mambo mengi, ujenzi wa barabara, uwanja wa ndege na ameleta ndege mbili na analeta ndege nyingine nne. Hayo yote yatasaidia kuondoa umaskini kwa sababu itaongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama wa Zanzibar pamoja na Watanzania wote wamechoka kubeba mizigo ya maji, pesa hizo zitasaidia wananchi wetu wa Tanzania tutoke kwenye umaskini twende katika hali nzuri. *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atampa nguvu Rais wetu Mheshimiwa Magufuli na ataondoa shida zetu zote na maji yatapatikana kwa kila mmoja wetu, Zanzibar pamoja na Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Halmashauri, Halmashauri zetu wanakusanya pesa, tuwasimamie vizuri lakini naomba Serikali zile pesa milioni 50 tuzipeleke kwenye Halmashauri. Wananchi wanangoja kwa hamu pesa zile kwani zitasaidia kuondosha umaskini na tutasaidia wale watu waliokuwa na shida kwenye ushirika, asilimia nne au tano walikuwa wanapata na kukopeshwa basi Serikali isaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pamoja na Rais wetu amefanya kazi nzuri kwa kuanzisha mabasi ya mwendokasi, Watanzania wamekuwa wakifaidika. Pia tunaingiza pesa chungu nzima na pesa hizo tutaziweka katika kilimo, maji pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni viwanda, kweli nasema Serikali inajitahidi kusimamia viwanda. Kwa kuwa na viwanda itasaidia sana wananchi na vijana wetu kupata ajira na ajira ni muhimu kwa Tanzania yetu. Kwa kuanzisha viwanda mbalimbali mapato ya Taifa yataongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* yetu lazima isimamie ukusanyaji wa mapato. Mapato yapo kwenye viwanda, sekta ya utalii na bandari, haya yote tuyasimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba Serikali yangu ya Muungano tuwasaidie watu wa Zanzibar. Mwenzangu Mheshimiwa Rehani amesema lakini mimi nazidi kusema sisi wote ni ndugu moja, hakuna upinzani wala ubaguzi. Wale watu wanyonge kutoka Zanzibar wanaleta biashara ndogo ndogo, wanatoa ushuru kule lakini ikifika hapa wanahangaishwa, basi tuwatazame na tuwaachie.

Wazanzibar tuwaache wafaidike kwa sababu kule Zanzibar unalipa ushuru namna mbili, ZRB pamoja na TRA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri tuboreshe biashara za viwanda. Kama tutasimamia kweli Tanzania yetu tutapata mapato mengi sana, asidharau. Vilevile tunataka tufufue viwanda vyetu, wale watu wanakuja kutoka nchi za nje wanataka kuanzisha viwanda tuwapokee. Hii ni kwa sababu vijana wetu watapata ajira na kuondokana na umaskini. Vijana wakifanya kazi na nyumbani akipeleka chochote itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kitu kimoja, sisi Zanzibar pamoja na Tanzania yetu tuna mambo mengi sana ya kusaidia kuingiza pesa. Tanzania tunazalisha mazao kama kunde, choroko na dengu, tunao watu kutoka nchi za nje kama India wanakuja kununua tuwakaribishe. Sisi tunataka maendeleo na mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri ameondoa kodi katika mazao ya kilimo kwa tani moja. Vilevile ameondoa kodi kwenye magari, tunamshukuru sana Mungu amweke. Serikali yetu inataka kufanya mambo, tumuunge mkono Rais wetu Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli kwa sababu Mheshimiwa Waziri... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bhagwanji, muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Lolesia.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya ndani ya Taifa letu hasa katika sekta ya madini, ameanza kuonyesha mfano. Kwa kipindi

kirefu sana kumekuwepo na malalamiko mengi kwa wananchi na watu mbalimbali na NGOs kuhusiana na suala la madini. Kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya kitu kikubwa cha ujasiri kuweza kuchukua hatua thabiti na kuweza kuona namna ya kukwamua mambo ya rasilimali katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ambao tunatoka maeneo ya madini tunaona jinsi ambavyo tunaachiwa mashimo. Ukienda kwa mfano GGM watu wanachimba madini kwa kiwango kikubwa lakini wananchi waliopo jirani na maeneo hayo hatuoni faida zaidi katika madini hayo. Kwa hiyo, kwa hatua ambazo Mheshimiwa Rais amechukua mimi binafsi pamoja na wananchi tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwimbaji mmoja alisema kwamba niseme nini Bwana. Kwa kweli hata mimi nasimama hapa leo kuimba kusema niseme nini Bwana kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendeleo sasa kuomba kwamba mikataba iendeleo kuletwa hapa Bungeni ili tuweze kuipitia kuona namna ya kuwezesha zaidi rasilimali za Taifa hili ili tuweze kufaidika sisi wananchi wa Taifa la Tanzania. Sambamba na mikataba lakini pia ziangaliwe sheria ambazo zipo pamoja na sera, kama hazitupeleki mahali ambapo tunastahili, tuweze kuzifanyia kazi na kuzirekebisha ili wananchi tuendeleo kufaidika zaidi na rasilimali ambazo Mungu ametupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa msisitizo pia kwenye usimamizi wa maliasili zetu. Mheshimiwa Rais ametuonesha mfano na viongozi wengine tuendeleo kuonyesha mfano, tuwe wazalendo kwa Taifa letu. Kwa hiyo, niombe tu kwa ujumla sisi sote kwa pamoja wananchi na Wabunge tusimame imara tukiendeleo kumuunga mkono Mheshimiwa Rais lakini pia hata sisi wenyewe tuweze kusimamia kwa dhati rasilimali za Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti ya mwaka huu 2017/2018. Kama ambavyo wenzangu wametangulia kusema ni bajeti ya mfano. Ni bajeti ambayo kwa kweli ukiisoma inafurahisha na wananchi wengi tumeifurahia bajeti hii. Mimi nasimama kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Busanda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani? Wananchi walio wengi hasa vijijini walikuwa wanateseka sana na vikodi vidogo vidogo lakini bajeti hii imeweza kuondoa hizi kero. Mwananchi alikuwa anaenda kuuza gunia lake la mahindi analipa kodi, lakini kwa jinsi ambavyo bajeti hii imeweza kuondoa kodi ndogo ndogo, kwa kweli nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya kwa wananchi wetu na kwa Taifa zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika bajeti tunaona jinsi ambavyo imejikita katika kuangalia miundombinu muhimu kwa ajili ya kujenga uchumi kuelekea kwenye viwanda. Tanzania ya viwanda inahitajika tuwe na reli na tayari kwenye bajeti imo, tunaenda kujenga reli ya *standard gauge*. Kwa hiyo, nipongeze kwa kweli kwa jinsi ambavyo ameangalia mifumo ya kiuchumi ikiwepo reli, maji na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu msisitizo zaidi katika suala la maji. Katika bajeti mmeonyesha jinsi ambavyo mtaangalia vyanzo vya maji kwa mfano kwenye maziwa makubwa kama Ziwa Viktoria, Tanganyika na maziwa mengine. Kwa hiyo, niombe sasa katika utekelezaji wa bajeti tuhakikishe wananchi walio kandokando ya maziwa, kwa mfano, mimi Jimbo langu la Busanda lipo kandokando ya Ziwa Viktoria lakini hatuna maji. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuomba sasa utekelezaji, wananchi waweze kupewa maji ya kutosha na ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuweza kutenga hizi fedha ikiwezekana tuwe na Mfuko Maalum wa Maji, kama jinsi ambavyo *REA* iko katika suala la umeme, inapeleka umeme vijijini, hata katika suala la maji tuangalie kuwa na Mfuko Maalum kwa ajili ya kusaidia upelekaji wa maji vijijini. Vijijini ndiyo kuna changamoto kubwa sana ya suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kumtua ndoo mwanamke ni hasa wanawake walilopo vijijini. Kwa hiyo, niombe Serikali sasa ituwezeshe kuwa na Mfuko Maalum kwa ajili ya maji ili utuwezeshe kutekeleza miradi ya maji katika vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umeme, mimi napenda kuishukuru Serikali kwa mipango thabiti na ndiyo maana nasema nitaiunga mkono bajeti hii ya Serikali. Hii ni kwa sababu katika upande wa umeme Serikali imejipanga vizuri kupeleka umeme vijijini na tayari tumeshapata wale wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sasa umeme huu tunapofikisha kwenye vijiji vyetu, tuhakikishe unafika kwenye taasisi muhimu za umma zikiwepo shule za sekondari, shule za msingi, vituo vya afya na zahanati ili kuwezesha wananchi kupata huduma vizuri kwa sababu kuna huduma muhimu ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika suala la umeme, naomba Serikali iangalie uwezekano miradi hii ianze mara moja, kwa sababu wananchi wamesubiri umeme kwa muda mrefu na wanahitaji umeme ili waweze kuwa na viwanda vidogo vidogo. Vilevile wachimbaji wa madini na wafanyabiashara wanahitaji umeme. Kwa hiyo, naomba sana utekelezaji mara tutakapopitisha hii bajeti uanze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika bajeti tumezungumzia suala la elimu kwamba tutatoa mikopo kwa watoto wetu kwa masomo ya elimu ya juu. Napenda



kuipongeza sana Serikali, tunaomba utekelezaji huo ufanyike ili watoto waweze kupata mikopo na waweze kuendelea na masomo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni vizuri kuwa na Vyuo vya VETA. Kwa mfano, kwenye Mkoa wa Geita hatuna Chuo hata kimoja cha VETA. Nitumie fursa hii kuiomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu, hebu hakikisheni basi tunakuwa na Chuo cha VETA katika Mkoa wa Geita. Wilaya zote tano hatuna VETA hata sehemu moja na pia katika mkoa hatuna hata VETA moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sasa Serikali iangalie kutoa kipaumbele kwa mikoa na sehemu ambazo hawana kabisa huduma ya VETA. Hapo tutawazeshwa vijana wetu ambao ni wengi wanamaliza sekondari kupata ujuzi na hatimaye kuweza kuanzisha biashara zao na kujimudu katika maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la zahanati pamoja na vituo vya afya, ni Sera ya Taifa inasema kwamba kila kijiji kiwe na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya. Ninachoomba sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuendelea kutimiza, kweli imetenga fedha, lakini tuhakikishe zinafika kwa wananchi kwa wakati hasa katika Halmashauri zetu ili kazi iweze kufanyika, wananchi tuweze kujenga zahanati kwenye kila kijiji kama ambavyo Sera ya Taifa inasema, lakini vilevile kuwa na kituo cha afya kwenye kila kata na hospitali kwenye kila wilaya. Vilevile kuboresha huduma zote ambazo ni za muhimu ili wananchi wetu waweze kuwa na huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kodi kwa wachimbaji wadogo wa madini. Napenda tu kuomba Wizara ya Fedha hebu tuiangalie hii kodi, haiwezekani hawa wachimbaji wetu wadogo tuanze kuwatoza kodi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ya vyama vyote iliyokuja mezani imekwisha na muda wetu umekwisha, niwashukuru kwa kazi nzuri. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.54 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 16 Juni, Saa Tatu Asubuhi)*